28 JUNI, 2018

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Hamsini na Tisa – Tarehe 28 Juni, 2013

(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):-

Hati za Uhamishaji Fedha Na. 1 na Na. 2 Kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 *(Statements of Reallocation Warrant No. 1 and No. 2 for Financial Year 2012/2013).*

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaanza aswali na Ofisi ya Waziri Mkuu na yule atakayeuliza swali letu la kwanza Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa.

Na. 481

Ombi la Kupatiwa Vijiji

MHE. VITA R. KAWAWA aliuliza:-

Ni Sera ya Serikali kuwasogezea wananchi shughuli za Kiutawala karibu na maeneo yao.

Je, ni lini Serikali itatangaza Vijiji vilivyoombwa huko Namtumbo ambavyo havikutangazwa lakini vilipotangazwa vingine, maombi mengine yalipelekwa kwa kufuata vigezo vyote stahiki?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vita Rashid Mfaume Kawawa, Mbunge wa Namtumbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010 Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo iliwasilisha mapendekezo ya kuanzisha Kata mpya 6 na vijiji 12. Baada ya uchambuzi, maombi ya Kata zote sita yalikubaliwa na maombi ya vijiji viwili vya Luhangao na Likuyumandele vilikubaliwa baada ya kuonekana yanakidhi vigezo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013, Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo imewasilisha upya maombi ya vijiji 10 vya Mnalawi, Nambehe, Misufini, Mtwarapachani, Namali, Nangero, Ruvuma, Mwinuko, Mhungano na Sasawala ambavyo havikupata usajili pamoja na viambatisho muhimu ambavyo vilikosekana wakati wa chambuzi wa kwanza na ofisi yangu inashughulika maombi hayo.

Mheshimiwa Spika, vijiji vyote 10 vitapatiwa usajili pamoja na maombi ya vijiji vingine ambayo yatakuwa yamewasilishwa katika ofisi hii kabla ya kipindi cha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2014.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza.

Kwanza kabisa naishukuru sana Serikali kwa awali kuyakubali maombi haya ya vijiji 10, lakini pia naomba nisahihishe sio Luhangao ni kijiji cha Luhangano. Naomba niwaambie pia wananchi wa vijiji hivi 10 vilivyotajwa na Mheshimiwa Waziri kwamba kauli ya Serikali vitapatiwa nafasi yao.

Mheshimiwa Spika, swali. Kwa kuwa pia katika Tarafa ya Sasawala ambayo Makao Makuu yake ni Mji wa Lusewa. Tulikuwa tumeomba tupatiwe mji mdogo na maombi hayo pia yaliambatana na haya yako katika Ofisi ya TAMISEMI.

Je, Serikali inawaeleza nini wananchi wa Lusewa Makao Makuu ya Tarafa ya Sasawala lini watapatiwa mji mdogo huo au watapatiwa pamoja na vijiji hivi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Nyongeza la Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo. Ni kweli anachosema Mheshimiwa Mbunge. Nilitaka nikiri mbele yako kwamba Mbunge huyo amekuwa anatusumbua sana pale Ofisini kila wakati anakuwa anakumbusha jambo hili na hatimaye limepata muhutasari huu ni huu hapa.

Humu ndani nimesoma ni kweli huu mamlaka ya mji mdogo anaozungumza hapa katika kikao chao walichokaa tarehe 29 Juni, 2009 walizungumzia jambo hili. Tumeangalia na tumejaribu kuzungumza na *RAS* pamoja na wale wengine wote wanaohusika ili kuona kwamba utaratibu mzima unaotafutiwa unakamilika, lakini nataka nimthibitishie Mheshimiwa Vita Kawawa kwamba hili jambo tunalifahamu liko katika huu muhtasari ambao nimeuitisha hapa tutashughulikia.

MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA: Mheshimiwa Spika,

nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi linafanana na mazingira yaliyopo katika jimbo la Biharamulo Magharibi ambalo lina Tarafa mbili tu na tulishawasilisha maombi ya kuomba Tarafa hizo mbili zigawanywe angalau ziwe nne kurahisisha shughuli za Kiutawala.

Je, Serikali ni lini itagawanya Tarafa mbili za jimbo la Biharamulo Magharibi kuwa mji? Ahsante sana.

SPIKA: Pamoja na kuwa ni swali jipya Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kama tulivyoeleza hapa ndani na hili ni kwa faida ya wale wengine wote zoezi lilifanyika wakati ule tulipokuwa tunakwenda kwenye Uchaguzi Mkuu lakini sasa hivi tumeanza kupokea tena maombi mengine mapya sambamba na haya anayosema Dkt. Mbassa. Kwa hiyo tutakwenda kuangalia na kama tukiona kuna mapungufu yoyote yanayojitokeza tutawaarifu ili waweze kujua ni nini cha kufanya, lakini tuna-*compile* na maombi haya yote yanaangaliwa kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, na mamlaka hapa ni Mheshimiwa Rais mwenyewe kwa sababu anazungumzia Tarafa.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Ningependa kumwuliza Waziri vijiji vya Ndende, Chumo ambapo yeye mwenyewe alifika mwaka huu na aliahidi mbele ya wananchi kwamba maombi yao yatashughulikiwa. Ni sababu zipi mpaka leo Serikali haijatoa majibu?

SPIKA: Na wewe ulikuwa unangoja mpaka leo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, nimekwenda kule na hii kwenda, kwanza nilikuwa nakwenda kujithibitishia tu, maombi yao hawa wa Kilwa wameleta na Mheshimiwa Murtaza kila siku anakuja pale ofisini, labda apunguze sasa kidogo kuja kwa sababu leo namjibu kabisa rasmi najua anataka iingie katika rekodi. Tunayo na haya maombi yapo sambamba na wale wengine wote ambao mmeleta maombi tunayaangalia.

Mheshimiwa Spika, nataka tu niseme si maombi yote yanayoletwa kwetu yote tunasema ndiyo. Kama unakumbuka vizuri *last time* tulileta orodha hapa Bungeni, Wabunge wakajithibitishia wenyewe wakaangalia tutafanya hivyo hivyo hata safari hii ndiyo maelekezo tuliyonayo na tutamshauri Waziri Mkuu *accordingly. (Makofi)*

Na. 482

Mradi wa Maji wa Lukululu

MHE. GODFREY W. ZAMBI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Mradi wa Maji wa Lukululu ambao utawezesha takribani vijiji 12 vya Kata za Mkugali, Myovizi, na Mlowo kupata maji ya uhakika?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Lukululu umeanza kutekelezwa mwaka 2012/2013 na umelenga kuhudumia vijiji 12 vya Lukululu, Mbewe, Mlangali, Shaji na Ndolezi vilivyopo Kata ya Mlangali na vijiji vya Ichesa, Ivugula,

Myovizi, Mbulu, Igunda, Mahenje na Shomola vilivyopo Kata ya Myowizi.

Kutokana na jiografia ya eneo la mradi, kijiji cha Lukululu kitatumia chanzo cha chemchem ya Lukululu na vijiji 11 vilivyobaki vitatumia chanzo cha mito midogo *(streams*) ya Manyota na Hasara. Hadi sasa, Serikali imetumia kiasi cha shilingi milioni 100 kati ya shilingi milioni 187 zinazohitajika kwa ajili ya vitongoji vitatu (3) kati ya vitongoji sita (6) vilivyopo katika kijiji cha Lukululu.

Kazi zilizofanyika ni kukamilisha kazi za ujenzi wa chanzo, ulazaji wa bomba kutoka kwenye chanzo hadi kwenye tanki urefu wa kilomita 7 na ujenzi wa tanki lenye mita za ujazo 50. Ili kupeleka huduma ya maji katika vijiji vyote 12 vya Mradi wa Maji Lukululu, mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imetenga shilingi bilioni 2.5.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuboresha huduma ya maji katika Mji Mdogo wa Mlowo, mwezi Julai 2012, Serikali imekamilisha usanifu wa mradi katika mji huo pamoja na miji mingine ya Tunduma, Mbozi, Mbeya, Vwawa, Rujewa, Chunya, Mbalizi, Kasumulu, Itumba/Isongole, Tukuyu na Kyela. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 700 kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa miji ya Tunduma, Chunya na Vwawa. Serikali itaendelea kutenga fedha mwaka hadi mwaka ili kukamilisha miji yote iliyobaki katika mkoa wa Mbeya ukiwemo mji mdogo wa Mlowo.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kwa dhati ya moyo wangu kabisa niishukuru Serikali kwa *commitment* yake katika kukamilisha mradi huu. Lakini pia naomba kabla sijauliza maswali ya nyongeza nifanye masahihisho kidogo kijiji cha Shomola ambacho kimetajwa kwamba kiko katika Kata ya Myovizi kipo Kata ya Mlangali. Kwa hiyo naomba kumbukumbu hiyo iwekwe sawasawa. Baada ya hayo naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Lukululu ni wa

muda mrefu sana na naishukuru Serikali kama ilivyosema kwamba imetenga hizi shilingi bilioni mbili na nusu. Nataka *commitment* ya Serikali mradi huu wa Lukululu utakamilika lini pamoja na kutenga fedha. Kwa sababu kutenga fedha na utekelezaji ni mambo mawili tofauti, naomba *commitment* ya Serikali?

Swali la pili, mji wa Mlowo ambao unakua kwa kasi sana kwa mchana unakuwa na zaidi ya watu laki moja, lakini una tatizo kubwa sana la maji. Ninaomba pia *commitment* ya Serikali iseme kwamba mji wa Mlowo ambao katika majibu ya Mheshimiwa Waziri hauko kwenye ile miji mitatu ambayo imepangwa kwamba utaanza kujengewa miradi ya maji. Ni lini mji huu pamoja na miji mingine ambayo imetajwa itapata maji ili wananchi wapate maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru kwa shukrani alizozitoa tunazipokea na tutaendelea kujitahidi kuhakikisha kwamba wananchi wa Mbeya na mahali pengine wanapata maji.

Ni kweli huu mradi wa Lukululu umechukua muda mrefu lakini sababu moja kubwa ambayo ilisababisha mradi huu na mingine ni ukosefu wa fedha za kutosha. Kwa hiyo, imekuwa ikitekeleza kwa awamu. Mimi nadhani sasa hivi nimhakikishie kwamba tumetenga fedha na hii ni matokeo ya kazi ya Wabunge ambayo ilifanywa hapa ya kupata fedha za nyongeza. Kwa hiyo, hizi shilingi bilioni mbili na nusu ni kati ya zile shilingi 184.5. Namhakikishia ujenzi ukianza mradi huu utakamilika na ili mradi huu ukamilike unahitaji shilingi bilioni 7.5. kwa hiyo ni fedha nyingi na tutaendelea kutekeleza.

Kuhusu mji wa Mlowo jambo la msingi nimefika pale Mbozi na nimetembelea huu mji wa Mlowo naufahamu na Vwawa naifahamu. Sasa suala hapa ni kugawana *resources* tulizonazo. Tumetenga shilingi milioni 700 na hizo shilingi milioni 700 zitatumika kwa Tunduma shilingi milioni 100, milioni 100 kwa ajili ya Chunya ambao walihitaji shilingi milioni 172 na shilingi milioni 500 kwa ajili ya mji wa Vwawa ambao huko

Mbozi kwa Mheshimiwa Zambi. Wilaya hiyo ya Mbozi imetengewa shilingi bilioni 1.8 katika miradi ya vijiji 10, kwa hizo shilingi bilioni mbili na nusu. Nimhakikishie tu kama tutaendelea kutenga fedha na huu mradi wa Mlowo nao utapata maji, lakini lazima tuhakikishe na maeneo mengine yanapata maji.

MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Jibu la Waziri limetaja mji wa Mbalizi kwamba ni miongoni mwa miji ambayo inatazamiwa kupata maji. Lakini mji huu kero yake ya maji imekuwa ya muda mrefu na hata Rais alipokuja aliwaahidi wananchi kwamba watapata maji kwa kipindi kifupi. Sasa nauliza ni lini kero hii ya maji pale Mbalizi itakwisha, ni lini Serikali itashughulikia au itaanza mradi huo? Ahsante sana.

SPIKA: Waheshimiwa mnauliza *very specific questions*, bahati nzuri tu Mawaziri wenyewe wanajua, hebu Mheshimiwa Naibu Waziri jibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli mji wa Mbalizi ni moja ya miji ambayo ina matatizo ya maji kama ilivyo miji mingine pale mjini Mbeya.

Naomba nisisitize kwamba suala la msingi hapa ni ugawanaji wa *resources* hatujaiacha Mbeya bila ya miradi mingine ya maji ikiwemo Mbalizi. Tuna mradi mkubwa tumefanya pale mjini Mbeya na tuna miradi ya vijiji 10 katika jimbo lake Mheshimiwa Mchungaji Manjale.

Kwa hiyo nataka nimhakikishie hata huu mji wa Mbalizi tutauingiza kwa awamu baada ya kukamilisha miradi ambayo nimeitaja katika mkoa wa Mbeya. Tuzingatie kama miji hii haipo Mbeya tu ipo katika Tanzania nzima na hatuwezi kuitekeleza yote kwa wakati mmoja. Kwa awamu hii tumeanza na miji kama arobaini ambayo tumeichukua hiyo ambayo nimeitaja.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, nashukuru,

kwa kuwa katika majibu ya Naibu Waziri amejaribu kuainisha vijiji 10 vya miradi ya Benki ya Dunia ambavyo vinaendelea. Na kwa kuwa katika moja ya Halmashauri yetu ya Mbozi ni mradi wa vijiji vitatu tu ndio ambao sasa hivi unajengewa visima na bado vijiji saba. Sasa ningependa kauli ya Serikali ni lini sasa miradi ya vijiji vyote vilivyobakia vitakamilika?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbozi imegawanyika kuna wilaya mpya ya Momba na kabla ya hapo walikuwa wanatekeleza vijiji vitano na katika vile vitano vijiji vitatu vilikuwa upande ambao sasa hivi ni Momba na viwili vilikuwa upande ambao ni Mbozi.

Katika vile vitatu vya upande wa Momba kijiji kimoja cha Namtambala kimekamilika na hivi viwili tunategemea vitakamilika mwezi Septemba na kimoja ambacho ni cha Mnangi kipo upande wa Mbozi kitakamilika wakati wowote mwezi Julai.

Kwa hiyo, tunategemea vile vitano pamoja na vile viwili vya upande wa Mbozi vyote vikamilike Septemba kwa sababu usanifu ulishafanyika na katika vikao vyetu na Wahandisi ambavyo tumefanya hapa Dodoma tumewaagiza vile vijiji vitangazwe na vikamilike Septemba.

Lakini kuna vile vitano ambavyo vinakuja kwenye Bajeti ya 2013/2014 navyo tumewaagiza wavitangaze kwa sababu tayari usanifu ulishafanyika. Kwa maana hiyo kwa upande wa Mbozi na Momba mtakuwa na vijiji 10 tu kwa sababu ndio vilivyoibuliwa ilipokuwa Wilaya moja.

SPIKA: Sasa tunaendelea hatuwezi kujibu maji. Kwanza mmepata fedha kwa hiyo mkafuatilie huko huko.

Mgogoro wa Vijiji vya Mwendakulima na Mmiliki wa Mgodi wa Barrick

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI (K.n.y. MHE. JAMES D. LEMBELI) aliuliza:-

Mgogoro kati ya baadhi ya Wananchi wa Vijiji vya Kata ya Mwendakulima na mmiliki wa Mgodi wa Dhahabu wa *Buzwagi African Gold (Barrick*) kuhusu fidia limedumu kwa muda mrefu sasa na kwa zaidi ya mara tatu Serikali imekuwa ikiahidi Bungeni kumaliza tatizo hilo lakini hadi sasa hakuna kilichofanyika:-

Je, Serikali inawaambia nini sasa Wananchi wa Vijiji vya Mwime, Mwendakulima na Chapulwa, juu ya hatima ya mgogoro huo?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inakiri kuwepo kwa malalamiko na mgogoro kati ya vijiji vya Kata ya Mwendakulima na mgodi wa dhahabu wa Buzwagi unaomilikiwa na Kampuni ya *African Barrick Gold* (ABG) unaotokana na suala la fidia, kupatiwa makazi mbadala, pamoja na njia mbadala ya kutoka Chapyulwa kwenda Mwendakulima baada ya kupisha ujenzi wa mgodi huo.

Malalamiko ya fidia yalifanyiwa kazi na walalamikaji walilipwa. Kwa sasa mkandarasi anaendelea na utengenezaji wa njia mbadala ya kutoka kijiji cha Mwendakulima kwenda Kijiji cha Mwime na inategemewa njia itakuwa imekamilika ifikapo mwishoni mwa mwezi Julai, 2013.

Aidha, njia mbadala ya kutoka Kijiji cha Chapulwa

kwenda Mwime kwa sasa inapita kando kando ya uzio wa mgodi, hali ambayo imekuwa ikilalamikiwa na wananchi wa kijiji hicho kwa kuwa wakati wa usiku kumekuwa na ukamataji wa wapita njia hiyo wakidhaniwa ni wahalifu wanaodhamiria kuiba ndani mgodi huo. Serikali inaagiza kwamba wale wote wanaojihusisha na unyanyasaji wa wananchi waache mara moja kabla hawajafikishwa kwenye vyombo vya kisheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo, Serikali inakiri kupokea malalamiko mapya kutoka kwa wananchi wa vijiji vya Kata za Mwendakulima. Katika kuyashughulikia malalamiko hayo, Mkuu wa Wilaya ya Kahama ameunda Kamati Ndogo ambayo imejumuisha wataalamu kutoka katika Idara mbalimbali za Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kahama pamoja na Ofisi ya Afisa Madini Mkazi – Kahama.

Kazi kubwa waliyopewa ni kubaini malalamiko zaidi yanayoendelea kutolewa na wananchi hawa ili kufahamu msingi wa malalamiko hayo na kutoa fursa kwa Serikali kutoa ufumbuzi wa kudumu. Kamati hii ilianza kazi tarehe 12 Machi, 2013 na kuwasilisha taarifa pamoja na mapendekezo yake kwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama mwezi Mei, 2013.

Kwa sasa Mkuu wa Wilaya anaichambua taarifa hiyo ili aweze kuitisha kikao cha wadau wote (wahusika) na kujadili kwa pamoja namna ya kutatua malalamiko hayo mapema iwezekanavyo.

MHE. DKT. TITUS M. KAMANI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Naishukuru Serikali kwa juhudi wanazochukua kutatua tatizo hili. Lakini tatizo la migogoro kwenye maeneo yanayozunguka migodi yetu mikubwa ni tatizo sugu katika nchi yetu kwenye migodi yote mikubwa ikiwemo *North Mara,* Mwadui na Bulyahgulu na wananchi hawa wamezungukwa na umaskini mkubwa.

Ni lini Serikali itachukua juhudi za makusudi kuondoa

migogoro hii kwenye maeneo yote na kuwaondolea umaskini wananchi hawa?

Swali la pili, kwa sababu kuna nchi ambazo zimepata manufaa makubwa sana kutokana na migodi ikiwemo Botswana. Ni lini Serikali itachukua hatua kwenda kujifunza namna migodi inaweza kunufaisha taifa letu na wananchi wake. Asante sana.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE): Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kutatua migogoro inayojitokeza kwenye maeneo yanayozunguka migodi ikiwemo kutafuta maeneo mbadala kwa ajili ya wachimbaji wadogo ambao wengi wamekuwa wakivamia maeneo ya migodi mikubwa kufanya shughuli za utafutaji.

Leo hii tarehe 28 kwenye Hoteli ya Kempiski Serikali pamoja na migodi mikubwa yote inasaini makubaliano ya kusaidiana namna bora ya kuwasaidia wachimbaji pamoja na jamii zinazozunguka migodi kazi ambayo tuliianza tangu mwezi Novemba mwaka kwa kuwa na majadiliano ya kina ya kutafuta suluhu ya pamoja na leo tumefikia tamati hiyo, tumekubaliana mambo mengi ikiwemo kutenga maeneo kutoka kwenye migodi mikubwa kuwaachia wachimbaji wadogo na kusaidaia shughuli za maendeleo katika maeneo yote yanayozunguka migodi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali kujifunza. Tumejifunza sana na ndiyo maana tumefanya mabadiliko makubwa ya Sheria zetu na hata sisi tunaozisimamia mnaweza kuona kwamba mambo mengi ambayo yalikuwa huko nyuma yanatutatiza sasa hivi tumeyakataa pamoja na maendeleo katika maeneo ya migodi ikiwemo Kahama yenyewe migodi inajitahidi sasa hivi kufanya shughuli za maendeleo. Kwa hiyo, tumejifunza na tume-*improve* sana na ukilinganisha na tulikotoka.

MHE. SULEMANI MASOUD NCHAMBI: Mheshimiwa

Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tatizo kubwa la maeneo yanayozunguka migodi ni kutokana na watu kutoridhika na rasilimali zile zinapoondoka na shughuli za maendeleo kuwa duni.

Je, Serikali iko tayari kuachia asilimia fulani ya *loyalty* ili kuharakisha shughuli za maendeleo kwenye maeneo yanayozunguka migodi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE): Mheshimiwa Spika, suala la kuachia asilimia kama *loyalty* kwenye maeneo yanayozunguka mgodi linahitaji mjadala mpana kwa kuwa taratibu zilizopo sasa makusanyo yote ya mapato yanayotokana na shughuli mbalimbali za uzalishaji kwenye nchi yetu yanakwenda kwenye mfuko mkuu wa Hazina na baada ya pale ndiyo fedha zile ndizo tunazogawana kupitia Bajeti kupeleka maendeleo kwenye maeneo mbalimbali ya nchi.

Ninachokifahamu kwa sasa Halmashauri au maeneo yenye migodi au miradi mbalimbali inapata mapato ambayo ni *service levy* ambayo ni asilimia 0.3 ya *turnover* katika uzalishaji wa migodi ikiwemo Halmashauri ya Kishapu Mheshimiwa Mbunge anafahamu tumefanya kazi kubwa sana kwa kipindi cha wiki mbili tatu hizi kuchambua mapato yote ambayo Halmashauri ya Kishapu inatakiwa kuyapata ikiwemo na kampuni zilizopewa mikataba midogo kwa maana ya *sub-contractors* katika mgodi wa Mwadui na tayari takwimu zile ziko tayari na Halmashauri ya Kishapu tumeshaiandikia barua ili iweze kupata mapato stahili kutoka kwenye makampuni hayo na maeneo mengine ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo suala hili la kuongeza asilimia kwenye maeneo ya migodi hatuwezi kulitolea maamuzi harakaharaka linahitaji mjadala mpana na wadau pamoja na Waheshimiwa Wabunge mtakapoona inafaa basi tutaweza kubadilisha Kanuni zetu na Sheria zetu ili kuongeza asilimia ambazo zitakwenda kwenye Halmashauri.

MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Spika,

asante. Naomba niulize swali dogo kwamba kwa kuwa Sheria ya Madini tuliyoirekebisha ilisema vizuri sana kuhusu kuwafidia watu kwa kuhakikisha kwamba inawajengea makazi na kuwahamishia kwenye eneo jipya kabla ya mgodi kuanza.

Je, Sheria ya Ardhi itarekebishwa lini ili kuweza kutekeleza hili takwa la Sheria ya Madini.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE): Mheshimiwa Spika, ni kweli Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 imeeleza kwamba mchimbaji yoyote ama kampuni yoyote ambayo imepewa leseni ya utafiti ambayo inafahamika *kama prospecting license* kabla hajaanza shughuli lazima apate idhini ya eneo husika na watu husika wenye maeneo yao kabla hajafanya shughuli zake. Hiyo inaelezwa kwenye *Section 95* ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010.

Baada ya kugundua mashapo ambayo yanatosheleza kuanzisha mradi mkubwa wa uchimbaji mtu yuleyule au kampuni ile inatakiwa sasa kupitia Sheria namba 4 ya Ardhi aweze kufanya fidia ya wakazi ambao wanaishi katika eneo lile ambao wanapaswa kupisha ujenzi wa mgodi.

Sheria hiyo imekuwa ikitekelezwa kwenye fidia lakini nafahamu kwamba *sentiments* za Wabunge wengi hawaridhiki na fidia inayofanyika kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ambayo tunayo kwa maana inafidia *surface* peke yake na haifidii kilichoko kule chini.

Sheria Ardhi inasema vingine vyote ni mali yako wewe unayemiliki pale lakini isipokuwa madini na *petroleum* hiyo ni mali ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo ninachoweza kusema tu bado suala hili linatakiwa lirudi kwa wadau wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge na kuiomba Serikali tuweze kubadilisha Sheria hii kama wote tunakubaliana kwamba Sheria hii ina mapungufu basi tuibadilishe na wenzetu wa ardhi waweze kutuletea mabadiliko ya Sheria ambayo yatawezesha wananchi wanaoishi kwenye maeneo yenye rasilimali za madini waweze kunufaika zaidi ya kile wanachokipata sasa hivi. Kama Sheria za sasa. *(Makofi)*

SPIKA: Naomba mujibu maswali kwa kifupi tafadhili muda unaisha. Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa David Zacharia Kafulila.

Na. 248

Lengo la Ubinafsishaji Katika Migodi na Mashirika

MHE. DAVID Z. KAFULILA aliuliza:-

Lengo la ubinafsishaji lilikuwa kutumia sekta binafsi kuendeleza migodi na mashirika:-

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kuwa faida inayotangazwa na wawekezaji hasa kwenye migodi ni ya kweli na hakuna mwanya wa kudanganya kukwepa kodi?

(b) Je, ni kwa nini Serikali inasita kurejesha migodi kwa mashirika yaliyovunja mikataba ikiwemo mgodi wa chumvi Uvinza?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa faida inayotangazwa na wawekezaji hasa kwenye migodi ni ya kweli, Serikali imekuwa ikifanya kaguzi za gharama ya uwekezaji, uendeshaji, wingi na ubora wa madini yanayopatikana na kuhakikisha kuwa shughuli za migodi zinaendeshwa kwa uwazi. Lengo la Serikali ni kuendelea kujenga uwezo katika kufanya ukaguzi wa gharama hizo kupitia *TMAA* kwa kushirikiana na Idara ya Madini.

Hadi sasa ukaguzi unaofanywa na *TMAA* umesaidia sana katika kuhakikisha kuwa hakuna udanganyifu katika shughuli za madini hususan katika migodi mikubwa na ya kati. Hali kadhalika *TANSORT* wanadhibiti uzalishaji wa almasi na vito hapa nchini ili kuhakikisha kuwa madini hayo yanathaminishwa kwa bei zinazoendana na bei halisi za wakati huo.

(b) Mheshimiwa Spika, katika miaka ya 1990, Serikali ilijiondoa kwenye shughuli zote za biashara katika sekta zote ikiwemo sekta ya madini na kuacha shughuli hizo zifanywe na sekta binafsi na Serikali kubaki kuwa msimamizi, mhamasishaji na mkusanyaji kodi.

Hata hivyo kulingana na Sera ya Madini ya mwaka 2009 Serikali kupitia *STAMICO* imeamua kushiriki kweye umiliki wa migodi kadiri itakavyoonekana inafaa ili iweze kuongeza manufaa yatokanayo na shughuli za uchimbaji madini. Ushiriki wa Serikali katika kupata hisa kwenye migodi unafanyika kwa mujibu wa kifungu Na. 10 cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010. Kutokana na mtazamo huo, Serikali iko tayari kurudisha umiliki wa mgodi iliyobinafsishwa kama vile mgodi wa chumvi Uvinza iwapo wawekezaji watashindwa kuiendeleza kama ilivyokusudiwa na Serikali kuona manufaa yake.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya migodi ambayo tayari Serikali imerudisha umiliki mikononi mwake ni pamoja na Kiwira na Buhemba. Miradi ambayo kwa sasa inamilikiwa kwa ubia kati ya wawekezaji na Serikali kupitia *STAMICO* na *NDC* ni kama ifuatavyo:-

(i) *Buckreef,* Seriali asilimia 45 kupitia *STAMICO* na asilimia 55 zilizobaki zinamilikiwa na *TANZAM 2000*.

(ii) Buhemba, Serikali asilimia 40 kupitia *STAMICO* na asilimia 60 zinamilikiwa na *Manjiro Resources Ltd.*

(iii) Mchuchuma na Liganga Serikali asilimia 20 kupitia *NDC* na asilimia 80 zinamilikiwa na *SICHWAN HOGDA;* na

(iv) Ngaka Serikali asilimia 30 kupitia *NDC* na asilimia 70 zinamilikiwa na *Intra Energy*.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, moja ya sababu ya kuanzishwa kwa Soko la Mitaji Tanzania mwaka 1996 ilikuwa ni kuhakikisha kwamba mashiriki yanayobinfsishwa yanakuwa *listed* kwenye Soko la Mitaji kwa maana ya *DSE* kwa lengo la kuhakikisha kwamba hesabu zao zinakuwa wazi ili kusudi faida yao ijulikane kwa uwazi, ili kusudi Serikali ipate kodi stahiki.

Mwaka 2010 Sheria ilitungwa na Bunge la kuhakikisha kwamba migodi yote na kampuni za simu zinakuwa listed kwenye Soko la Mitaji. Mpaka sasa Kanuni za kutekeleza Sheria hiyo hazijatungwa. Serikali inaweza kueleza watanzania ni kwanini kwa miaka mitatu imeshindwa kutengeneza Kanuni za kuhakikisha Sheria ya migodi na makampuni ya simu yanakuwa listed kwenye soko la mitaji? Hilo moja.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, mashirika yaliyobinafsishwa yaliyo mengi yameshindwa kutekeleza *investment plan* kwa maana ya makubaliano ya uwekezaji ukiwemo mgodi wa chumvi Uvinza na Mheshimiwa Naibu

Waziri wewe ni shahidi tulikwenda Uvinza ukaona mgodi umeng'olewa na *TMAA* ambayo iko chini yako ikathibitisha kwamba mgodi ule uling'olewa na ukauzwa nje ya nchi Iran lakini mpaka sasa Serikali imeshindwa kuchukua hatua. Waziri wa Uwekezaji amelala, Waziri wa Fedha hachukui hatua.

SPIKA: Bwana wewe kila siku tunagombana hebu uliza swali.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Naomba kujua ni kwanini Serikali imeshindwa kuchukua hatua mpaka sasa na wakati ushahidi wote inao?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la mwanzo la Mheshimiwa Kafulila kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli imechukua muda mrefu sana miaka mitatu ya kutengeneza Kanuni kwa sababu eneo hili ni eneo ambalo liko *very complex* eneo ambalo *fragile* na eneo ambalo ndilo litatupa reference kwa ajili ya makampuni mengine sasa kuingia katika soko la mitaji. Ni *its very first time* kuweza kufanya zoezi hili. Kwa hiyo, ukiangalia complexity ya eneo lenyewe ni *very fragile.*

Lakini tumhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba katika mwaka ujao wa fedha 2013/2014 Kanuni hizi zote zitakamilika na hiyo kazi itaanza kama vile ambavyo tunataka. Ahsante sana.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kuongeza majibu kwa swali ambalo limejibiwa Manaibu Mawaziri, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Kafulila kwamba Mawaziri hawakulala na wanafanya kazi yao ipasavyo.

Pili Mheshimiwa Kafulila lazima ajue kwamba tunavyobinafsisha makampuni ama tunayauza kama biashara ama tunauza kama mali na Uvinza iliuzwa kama mali.

Lakini hata hivyo haina maana kwamba mwekezaji aliyenunua mali zile alipaswa kuuza nje. Yeye mwenyewe ameniletea suala hilo na nikamhakikishia kwamba nalifanyia kazi ninaomba Mheshimiwa Kafulila awe mkweli ndani ya Bunge hili badala ya kutulaumu bila ya haki na awe na subira jambo zuri lazima lifanyiwe kazi vizuri na tutamrudishia majibu yake kwa manufaa ya taifa letu na manufaa ya watu wa Uvinza. *(Makofi)*

Na. 485

Madini ya Chokaa – Wilaya ya Kisarawe

MHE. SELEMANI S. JAFO aliuliza:-

Maeneo mengi ya Kisarawe hususani Kata yam ARUI na Kisarawe yana utajiri mkubwa sana wa chokaa

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kiwanda cha kutengeneza *Tiles, Gypsum* na vyombo vya udongo ili kuleta ajira kwa vijana na kukuza uchumi wa Kisarawe na Taifa kwa ujumla?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kufanya juhudi za kuvutia wawekezaji katika sekta mbalimbali za kiuchumi hapa nchini. Katika Wilaya ya Kisarawe, kampuni ya NITORI toka Japan imejitokeza kutaka kuwekeza katika utengenezaji wa bidhaa za kauri *(ceramics products)* na vifaa vingine kwa kutumia madini ya kaolini na chokaa yaliyopo katika Wilaya hiyo.

Mazungumzo yanaendelea kati ya kampuni ya NITORI ya Japan na Kampuni ya Pugu Kaolin ambayo ndiyo inayomiliki leseni ya uchimbaji wa madini hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine hususan Kituo cha Uwekezaji Tanzania *(TIC)* na Mamlaka ya Maeneo Huru kwa Mauzo Nje *(EPZA)* inaendelea kuweka vivutio na kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika maeneo yote ya kiuchumi kwa kutumia fursa mbalimbali zilizopo ili kuleta ajira za uhakika na kuongeza kipato cha wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, tunapenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaendelea kuhamasisha uwekezaji katika maeneo yote yenye malighafi ya kutosha ikiwemo matumizi ya madini ya chokaa yaliyoko katika Wilaya ya Kisarawe na sehemu zingine nchini.

MHE. SELEMANI S. JAFO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nchi yetu sasa hivi ni *importers* wakubwa sana wa *Gypsum* kwa ajili ya kujengea majumba yetu. Sasa Serikali ina mpango gani wa makusudi kwa sababu Kisarawe iko karibu sana na Jiji kubwa la kibiashara la Dar es Salaam, kutengeneza mpango mkakati wa haraka wa kuanzisha kiwanda cha *Gypsum* kwa sababu tunautajiri huo wa chokaa hasa pale Kisarawe Mjini na maeneo ya Malui?

Swali la pili, kwa kuwa tuna kila sababu ya kuwawezesha vijana na Kisarawe kuna vikundi vya vijana hivi sasa wanaendelea na uchimbaji mdogomdogo wa madini ya chokaa.

Je, Serikali inampango gani wa kuhakikisha vijana wa Kisarawe walioko katika vikundi kuwajengea uwezo wa jinsi gani wataweza ku-*process* ile chokaa hali kadhalika kuwatafutia masoko ili kukuza uchimi wao?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza ningependa kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge au Mwakilishi wetu katika *SADEC* ni heshima kwake binafsi na kwetu na hata jimboni kwake.

SPIKA: Helo! Jibu swali.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Suala la kwanza la kusema kuwa Serikali ilete wawekezaji wa kuwekeza katika kiwanda au kutengeneza *Gypsum* ninapenda niwahakikishie Wabunge wote kwa ujumla kwamba jinsi ilivyo yenyewe inatumika zaidi kutengeneza simenti. Kwa hiyo, unaposema kwa Kisarawe, Kisarawe ni maarufu sana kwa kuwa na gypsum nyingi pamoja na chokaa nyingi,pamoja na *cauline* nyingi.

Kwa hiyo, kusema kiwanda kitengeneze *Gypsum* siyo haki labda tuseme kuwa *Gypsum* hiyo itumike ili itengeneze simenti maana *gypsum* ni malighafi ya kutengeneza simenti. Huwezi kutengeneza kiwanda cha *gypsum* yenyewe ila tu unaweza kutumia *gypsum* kwa kutengeneza simenti, chokaa kutengeneza simenti, unaweza kutumia *cauline kutengeneza ceramic products.*

Kwa hiyo, ninashauri Wabunge wote na Mbunge wa Kisarawe kuwa *gypsum* yenyewe inatumika zaidi kwenye kutengeneza viwanda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakae sawasawa kwa sababu kuna mpango wa kutengeneza kiwanda cha simenti kama tulivyosikia jana kuwa Mheshimiwa Turky ana mpango wa kutengeneza kiwanda cha simenti kule Kisarawe. Kwa hiyo, atataumia *gypsum* kutengeneza simenti au atatatumia chokaa kutengeneza simenti.

Kwa hiyo, watu wote wa Kisarawe hasa vijana wajiunge pamoja, wafahamike wako wapi, wako wangapi, wanafanya nini ili waweze kunufaika na kiwanda cha saruji ambacho kitaweza kutumia *gypsum* au chokaa kule Kisarawe.

SPIKA: *(hapa mic ilizimwa)* ..... ungeweza kumpelekea kiwanda kumbe hakuna kitu. Mheshimiwa Anne Kilango, atafuatiwa na Mheshimiwa Amour.

MHE. ANNE K. MALECELA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kuuliza swali la nyongeza kwa sababu huu utajiri ulioko Wilaya ya Kisarawe katika Kata ya Marui ndiyo utajiri uliopo katika Kata ya Makanya Wilaya ya Same. Je, Serikali haioni umuhimu wa kwenda Kata ya Makanya Wilaya ya Same ili ikatafiti na kuona kuwa kuna umuhimu wa Serikali kututafutia mapato kutoka kwenye ile ya *gypsum* ya Makanya?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi sana maana ni swali *direct.*

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, Kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Makanya nako iko *gypsum* na tutafanya utafiti tuangalie jinsi ya kuweza kusaidia ili *gypsum* hiyo iweze kutumika kikamilifu kama nilivyosema inaweza kutumika kuweka kutengeneza simenti kwa hiyo tutafanya utafiti huko ili tuangalie jinsi ya kuweza kusaidia *gypsum* itumike ipasavyo.

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana suala langu ni moja tu. Je, viwanda vidogovidogo vimechangia kiasi gani katika pato la Taifa.

SPIKA: Swali jipya lakini haya, *SIDO* basi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Nyongeza la Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, kama ifuatavyo:-

Kuna utafiti ambao ulifanyika na Wizara yangu mwaka 2012/2013, Wizara ilifanya utafiti wa kuangalia viwanda vidogovidogo kama vinazalisha kiasi gani na utafiti huo ulibaini kuwa viwanda vidogovidogo na biashara ndogo nchini uliofanyika mwaka 2010, matokeo hayo yalionyesha kuwa sekta binafsi inaweza kusaidia 27.9% katika pato la Taifa na inaweza kuajiri Watanzania wengi ambao inapata milioni 5.2 wanaofanya kazi katika jasiliamali ndogondogo zipatazo milioni 3 hapa nchini.

SPIKA: Ahsante sana kwa kujibu kwa kifupi sasa tunakwenda Wizara ya Uchukuzi Mheshimiwa Omar Rashid Nundu, atauliza swali.

MHE. OMAR R. NUNDU: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, kabla ya kuuliza swali ninaomba nifanye marekebisho kufuatana na swali nilivyoliuliza swali (a) lilitakiwa lisomeke kama ifuatavyo:-

Je, kwa nini *ATC* ilipokonywa karakana na hiyo na ikakabidhiwa kwa kampuni binafsi ya kiwanja cha ndege cha Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba swali langu namba 486 lipate majibu ahsante sana.

Na. 486

Karakana ya Ndege katika Kiwanja cha Kia

MHE. OMAR R. NUNDU aliuliza:-

Katika miaka ya 1979 Serikali kwa wa Uholanzi ilijenga Karakana ya matengenezo ya ndege kwenye Uwanja wa *KIA* kwa lengo la kulipatia Taifa mapato kutokana na kutengeneza ndege na za ndani na nje ya nchi.

(a) Je, kwa nini *ATC* ilipokonywa karakana na hiyo na ikakabidhiwa kwa kampuni binafsi ya kiwanja cha ndege cha Kilimanjaro *(KADCO)?*

(b) Je, ndege ngapi zinakusudia kutengenezwa katika karakana hiyo tangu kukamilika kwa ujenzi wake hadi leo na Serikali imepata kiasi gani kwa kazi hiyo?

(c) Je, Karakana hiyo inatumikaje hivi sasa na Serikali ina mpango gani wa kuboresha matumizi yake?

WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari Rashid Nundu, Mbunge wa Tanga Mjini, lenye sehemu (a),(b) na (c) pamoja na marekebisho kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza siyo sahihi kwamba Shirika la Ndege la Tanzania kwa wakati huo *ATC,* lilipokonywa karakana iliyoko katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (*KIA).*

Ukweli ni kwamba uendeshaji wa karakana hiyo ulihamishwa *ATC* kwenda kampuni ya *Kilimanjaro Airports Development Company (KADCO)* mwaka 2000 ambayo Mheshimiwa Mbunge anaiita Kampuni binafsi hii ni Shirika la Umma vilevile, na hii ilikuwa kama sehemu ya maandalizi ya kubinafsisha *ATC.*

Kuhamishwa huko kulitokana na Sera ya Serikali ya kujiondoa kwenye uendeshaji wa moja kwa moja wa biashara na shughuili hizo kuachiwa sekta binafsi. Karakana hiyo bado ni mali ya Serikali, ilitoka mkono wa kushoto kwenda kulia.

(b) Mheshimiwa Spika, karakana ya Kilimanjaro ina uwezo wa kuhudumia ndege tatu (3) kubwa aina ya Boeing 737 kwa wakati mmoja. Wakati karakana hiyo ya *KIA* ikijengwa *ATC* ilikuwa na karakana yake nyingine katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere. Hivyo, *ATC* ikashindwa kuitumia karakana ya *KIA* kikamilifu. Karakana ilitumika chini ya uwezo wake na kwa hasara.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa sasa karakana hiyo inatumika kutoa huduma za *fixed Base Operation (FBO)* ambazo zinajumuisha kutoa huduma za ndege za watu mashuhuri. Karakana hiyo imekodishwa kwa kampuni inayomilikiwa na Watanzania ya *TANJET* kwa kipindi cha miaka kumi kuanzia mwaka 2006 na inalipa kiasi cha dola 46,900 kwa mwaka kama kodi ya pango na asilimia tano ya mapato ghafi kama tozo la biashara kwa *KADCO.*

MHE. OMAR R. NUNDU: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri ambayo hayaridhishi wala hayatoi ukweli kwanza inaonekana Wizara haielewi tuna nini pale Kilimanjaro.

Kwanza karakana ile siyo ya kutengeneza ndege 737 ni yakutengeneza ndege 747 ndege kubwa kuliko zote wakati ule wakati karakana hii inajengwa. *KADCO* imerudi Serikalini miaka miwili iliyopita kabla ya hapo ilikuwa kampuni Binafsi kwa hiyo, ilipopewa karakana ile ilikuwa ni kampuni binafsi.

Mheshimiwa Spika, karakana hiyo ilijengwa kwa Dola milioni 24 sasa hivi tunapata Dola 46.900 kwa mwaka maana yake kurudisha zile milioni 24 za *marketing*.

SPIKA: Waheshimiwa,niligombana na mtu hotuba hizo nyie mlikuwa hukohuko mnajuana kwa vilemba tuulizeni maswali tu. *(Vicheko).*

MHE. OMAR R. NUNDU: Itachukua miaka 1,000 swali la kwanza kwa nini karakana hii isiwekewe mipango ikafanya kazi ile iliyopangiwa badala ya *FBO,* pili, kwa kuwa huyo ambaye amekodisha sasa hivi amebakiza miaka mitatu ni taratibu gani zinazofanywa ili karakana hii ifanye kazi kama ilivyotakiwa pamoja na kuikabidhi jeshi ili itumie kwa *research* na *development* asante sana.

SPIKA: Sasa hiyo safi, Mheshimiwa ninaomba ujibu maswali na wewe usijibu maneno yenu hayo wewe jibu maswali.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Omar Rashid Nundu, Mbunge wa Tanga Mjini, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kuwa uwekezaji katika mradi huo wa hanga ya Kilimanjaro hauridhishi mimi mwenyewe ninaona mkataba huo kwa kweli hatukutengeneza vizuri mwaka 1976 na Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi aliyenitangulia alichukua juhudi kuwaita *TANJET* ambao ni kampuni sasa hivi ambayo inamiliki hilo eneo Mjini Dodoma mwaka 2011 tarehe 30 mwezi wa saba na kuamua mkataba upitiwe upya, ukapitiwa upya lakini *TANJET* wakakataa kushiriki katika kuupitia upya tena huo mkataba na baadaye wakaenda Mahakamani.

Suala zima likakwama kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri aliyenitangulia alifikia hapo na sisi wenzake tunaendelea kulimalizia hilo suala na nina uhakika katika kipindi siyo kirefu tutakuwa tumelimaliza. *(Makofi)*

Na. 487

Kiwanja cha Ndege cha Tunduru Kufunguliwa

MHE. ENG. RAMO M.MAKANI aliuliza:-

Wilaya ya Tunduru inaendelea kufunguka kwa fursa za kiuchumi na kijamii kufuatia Serikali kuboresha miundombinu ya barabara na reli inayopita Wilayani humo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi wa kati na mrefu wa kurudisha huduma ya Kiwanja cha Ndege katika Mji wa Tunduru ili kuboresha huduma za usafiri?

WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Ramo Matala Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kiwanja cha Ndege cha Tunduru kilifungwa mwaka 2005, kwa uamuzi wa pamoja kati ya Mamlaka ya Viwanja vya ndege *(TAA)* na uongozi wa Wilaya ya Tunduru kutokana na sababu za kiusalama.

Kiwanja hicho wakati huo kilikuwa kimezungukwa na majengo mbalimbali yakiwemo makazi ya wananchi na hivyo kutishia usalama kwa abiria, ndege na hata wananchi wenyewe.

Aidha, iliamuliwa kuwa huduma za usafiri wa anga zilizokuwa zinatolewa katika kiwanja hicho zihamishwe kwa muda katika kiwanja cha ndege cha Misheni ya Matemanga ambacho kinamilikiwa na taasisi ya dini ya Kiuma (Kanisa la Upendo Kristo Masihi).

Mheshimiwa Spika, kwa muda wa kati, Serikali kupitia Mamlaka ya viwanja vya ndege ilifanya mazungumzo na Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru na kukubaliana kuwa kiwanja kipya sasa kijengwe katika eneo jipya liitwalo 'Sisi kwa Sisi'na tayari Halmashauri imetoa eneo hilo kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja hicho.

Halmashauri ya Wilaya ya pia ilichukua jukumu la kukamilisha maandalizi ya awali kufanya tathimini ya mali za wananchi katika eneo la ujenzi ili walipwe na kupisha utekelezaji wa mradi huo. *(Makofi)*

MHE. ENG. RAMO M. MAKANI: Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini pia ninaipongeza Serikali kwa kuonyesha nia njema ya kuweza kusaidia Mji wa Tunduru na Wilaya ya Tunduru kwa ujumla kuweza kwenda kasi na shughuli zote za kimaendeleo zinazo elekea katika Wilaya ya Tunduru, hasa kuhusiana na program ya *Mtwara corridor.* Kwa kuwa tangu mwaka 2005, mpaka ni miaka minane na kwa kuwa kwa taarifa niliyo nao ni kwamba tayari tathmini imeshapelekwa Serikalini.

Mheshimiwa ninapenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Je, nikiwasilisha nakala ya taarifa ya tathmini Wizarani wiki ya kwanza baada ya kukamilika kwa Bunge Serikali itakuwa tayari kutoa ratiba ya utekelezaji wa mradi wa kiwanja cha ndege Tunduru kwa kasi itakayoendana na *speed* ya maendeleo inayoendelea Tunduru?

(b) Chini ya mradi wa *Mtwara Corridor* kuna mradi wa barabara inayotoka Mtwara mpaka *Mbamba Bay* na mradi wa reli inayotoka vilevile bandari ya Mtwara kwenda mpaka *Mbamba Bay,* mahali ambapo Mji wa Tunduru uko katikakati ya maeneo hayo kwa hiyo kufanya Tunduru kuwa ni *strategic location.*

(c) Je, katika mradi wa reli Mji wa Tunduru umeunganishwa na reli hiyo ambayo inatazamiwa kutoka Mtwara kwenda *Mbamba Bay* na kama haujaunganishwa aidha, reli imepita katika Mji wa Tunduru ama kuna *connection road* inayounganishwa Mji wa Tunduru na reli inayopita Tunduru ikiwa inaenda *Mbamba Bay* ikiwa inatokea Mtwara.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri jibu kwa kifupi.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mhandisi Ramo Makani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimefurahi kusikia kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ilishakamilisha zoezi la uthamini wa mali zilizopo katika eneo la Sisi kwa Sisi na tulikuwa hatuna taarifa tulipokuwa hapa kwenye Bunge hili, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge kama atatukabidhi hiyo taarifa tutashukuru sana.

Ningependa kumuhakikishia kuwa baada ya kupata Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nitaiagiza ianze uchambuzi wa awali kujua gharama za kutekeleza mradi huo.

Kuhusu reli sisi kama Wizara tunaona umuhimu mkubwa wa Tunduru katika *Mtwara Corridor* na tutakapofikia *design stage* ya hiyo reli kutoka Mtwara kwenda Mchuchuma, Liganga mpaka *Mbamba Bay* tutahakikisha Tunduru nayo inakumbukwa katika mtandao huo. *(Makofi)*

SPIKA: Tunaendelea kwa sababu kiwanja cha Tunduru ni kimoja tu Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo swali linalofuata.

Na. 488

Kuboresha Miundombinu ya Reli na Kupiga Marufuku Utumiaji wa Barabara Kama Mbadala wa Reli

MHE. SUSAN A. J. LYIMO aliuliza:-

Tanzania imejaliwa Bandari/Bahari na hivyo kufanya uwepo wa reli kuwa muhimu sana kwa usafirishaji wa bidhaa kwa nchi hizo.

(a) Je, ni lini Serikali itaboresha Miundombinu ya reli na kupiga marufuku utumiaji wa barabara kama mbadala wa reli hata pale inapokuwepo?

(b) Kwa kuwa barabara nyingi zimeharibika kutokana na matumizi mabaya ikiwemo kubeba mizigo mizito. Je, Serikali ina mpango gani?

WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati wa muda mrefu na mrefu kuboresha miundombinu ya reli nchini. Mkakati wa muda mfupi ni kuimarisha mtandao mzima wa reli iliyopo kwa kuondoa reli nyepesi za ratiri 56 hadi 60 kwa yadi zilizochoka na kutandika reli mpya na nzito zaidi za ratiri 80 kwa yadi.

Ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imeshafanya mkakati huo kutoka Pugu hadi Mpiji (km 22), Munisigara hadi Kitaraka (km 336), Malongwe hadi Igalula (km 73) na sasa tunalifanyia ukarabati eneo kati ya Kitaraka na Malongwe (km 89).

(b) Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zinazoendelea ni ujenzi wa madaraja mapya mawili kati ya Kilosa na Gulwe pamoja na daraja la tatu kati ya Bahi na Kintinku.Katika mwaka wa fedha 2013/2014 Benki ya Dunia imetenga kiasi cha dola milioni 3 kwa ajili ya kuyaongezea uwezo madaraja yote ya reli ya kati ili yafikie uwezo wa kupitisha injini za ekseli *(Axle Load)* kati ya tani 15-20 kutoka tani 13.7 za sasa.

Mheshimiwa Spika, mbali na uimarishaji wa njia ya reli, *TRL* katika mpango wake wa mwaka 2012/2013 imefanya manunuzi ya mabehewa ya kubeba mizigo na abiria, kujenga upya vichwa vya zamani vya treni na kununua vipya, kukarabati mabehewa, vichwa vya treni. Katika mwaka 2013/2014 *TRL* imetengewa shilingi 113.12 bilioni ili kukamilika manunuzi ya vichwa vya treni, mabehewa, mashine ya nyakua, kukarabati majengo ya stesheni.

(c) Mheshimiwa Spika, mpango wa muda mrefu ni kutandika reli mpya ya kiwango cha Kimataifa kutoka Dar es salaam hadi Isaka, kutoka Isaka hadi Kigali (Rwanda) na Musongati (Burundi) kwa kushirikiana na Serikali za Rwanda na Burundi.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza, kwa sababau swali langu lilihusu *strategic position/ geographical position,* tuliyo nayo na umuhimu wa Bandari pamoja na reli nilitaka kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwa kuwa Mombasa wanapanua Bandari yao sasa hivi na kwa maana hiyo mizigo mingi itakuwa inapitia Mombasa.

Je, Serikali kwa kuona hilo ina mikakati gani sasa kuhakikisha kuwa Bandari yetu ya Dar es salaam inapanuliwa haraka sana. Vilevile kuondoa matatizo makubwa yaliyopo kwa mfano ucheleweshaji wa kupakua mizigo na wizi uliko bandarini?

Ni wazi kuwa katika mkakati wa Mheshimiwa Waziri katika majibu yake hajaelezea umuhimu wa reli ya Kaskazini ambao pia inatoka Dar es salaam kwenda mpaka Arusha ili kuweza kupeleka mizigo katika Mikoa ya jirani ya Kaskazini na nchi jirani ya Uganda na Kenya.

Je, wana mkakati gani kwa hilo?

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunaelewa kuwa Mombasa inapanua Bandari yake na siyo Mombasa tu lakini nchi nyingi Barani Afrika zinapanua Bandari zao na sisi Bandari ya Dar es salaam tunaipanua.

Sasa hivi kampuni mpya ambayo tumeiteua baada ya kuiondoa CCC imeshaanza kazi kwenye bandari ya Dar es Salaam, wamemaliza *study* yao wiki hii na kuanzia wiki ijayo tunaanza kazi ya ujenzi wa gati Na. 13 na 14.

Siyo hivyo tu, tumeamua kuangalia upya gati Na. 1 mpaka 7 ambazo zilijengwa miaka ya 1950 na 1960, tayari upembuzi yakinifu na *design* imefanyika na *Trade Mark East Africa*, tumetangaza kazi na tunaanza kuzipanua pia hizo gati na kuzifanya ziwe *modern* zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi sina wasiwasi na ushindani na Kenya, suala la wizi tumeshalidhibiti kwa kiasi kikubwa. Mwaka jana na mwaka juzi kulikuwa na mchezo wa kuibuwa kontena zinapotea, kuanzia mwaka jana mpaka leo hakuna kontena hata moja limepotea Dar es Salaam na usalama bandari ya Dar es Salaam umeshadhibitiwa kiasi ambacho sasa hivi nchi kama Zimbabwe kwa mara ya kwanza sasa zinapitisha shehena za magari katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umuhimu wa reli ya Kaskazini kwamba katika jibu langu sikuonesha, ninapoongelea mtandao wa reli ina maana ni mtandao wote wa reli hata hiyo reli ya Kaskazini.

Lakini reli ya Kaskazini sijaiweka katika uboreshaji kwa sababu ipo katika mpango mahsusi wa ujenzi wa reli ya kudumu, *standard gauge* kutoka bandari ya Mwambani mpaka Musoma mradi ambao tayari tumeanza kuufanyia kazi kwa *studies* kukamilika na vilevile kuna pesa mmepitisha wenyewe kwa ajili ya reli hiyo. *(Makofi)*

SPIKA: Majibu mazuri, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Dkt. Henry Shekifu.

Ahadi za Ruzuku ya Pembejeo kwa Wakulima wa Mboga Mboga

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU aliuliza:-

Serikali iliahidi kutoa ruzuku ya pembejeo kwa wakulima wa mboga mboga wanaoishi katika maeneo yenye uhaba wa ardhi kama Lushoto ili waboreshe uzalishaji:-

(a) Je, Serikali imefikia hatua gani katika kutimiza ahadi hiyo inayosubiriwa na vijana wengi?

(b) Je, Serikali itasaidia kufufua mifereji ambayo ilikuwa ikitumika kwa umwagiliaji maeneo ambayo yanatumika kwa kilimo cha Mboga Mboga na matunda?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Henry Daffa Shekifu, Mbunge wa Lushoto, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kutoa ruzuku ya pembejeo kwa muda utakavyoruhusu kulingana na mazingira ya kiuchumi na kijamii kwa mazao ya chakula na biashara ili kujenga uzoefu wa matumizi ya pembejeo hususani mbolea na mbegu bora kwa Wakulima nchini.

Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa Bajeti, ruzuku ya pembejeo kwa sasa inatolewa kwa baadhi ya mazao kama pamba, korosho, alizeti, mtama, mahindi, mpunga, miche bora ya kahawa na miche bora ya chai.

Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ni kupanua wigo wa utoaji wa ruzuku hiyo ya pembejeo kwa wakulima wengi zaidi ikiwemo wakulima wa mboga mboga wa Wilaya ya Lushoto hatua kwa hatua kulingana na upatikanaji wa fedha.

Aidha, katika kukabiliana na changamoto ya mazao ya bustani, kuharibika baada ya kuvunwa, Serikali katika mwaka 2012/2013 ilitenga shilingi bilioni 1.48 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya kukusanyia mazao na miundombinu ya kuhifadhia mazao (*cold rooms*) katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro Mbeya na Tanga ambapo wakulima wa Wilaya ya Lushoto pia watanufaika.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa mifereji ya umwagiliaji katika kilimo cha mboga mboga, Serikali imekuwa ikitekeleza mipango na mikakati mbalimbali ili kuwezesha matumizi ya kilimo cha umwagiliaji wa mboga mboga nchini.

Mipango hiyo ni pamoja mradi wa uboreshaji wa mifereji ya Asili *(Traditional Irrigation Improvement Project- TIIP 1987-1997)* uliojitokeza kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Uholanzi (*SNV*), Mradi shirikishi wa maendeleo ya Kilimo *PADEP* na programu ya kuendeleza sekta ya kilimo *ASDP* kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *DADPS* kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya mifereji ya umwagiliaji. *(Makofi)*

MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usipingika kwamba eneo la kilimo la mbogamboga na matunda huajiri vijana wengi, tatizo kubwa ni ubora wa mazao na ukosefu wa soko, pamoja na kujengewa miundombinu ya kuhifadhi mazao.

Je, Serikali inaonaje kupeleka mbolea pamoja na pembejeo nyingine kwa ajili ya vijana kuweza kuboresha zao hili la kilimo?

Swali la pili, mradi ya *TIIP* ni mradi ambao ulikuwa muhimu sana kwa ajili ya mifereji, mradi huu baada ya wafadhili kuondoka haukuendelea, Serikali inachukua hatua gani kuendeleza mradi huu?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane moja kwa moja kwamba tatizo kwenye mazao ya *horticulture* kwa maana ya mazao ya mbogamboga ni ule ukosefu wa soko, mara nyingi hili tatizo la ubora wa mazao si tatizo sana lakini kwa sababu masoko ya nje yanakuwa *very specific* yanapotaka mazao yawe na *specification* fulani, lakini hili kwa upande wa *TAHA* ambalo lipo chini ya Wizara ya Kilimo tumekubaliana kwamba sasa hivi wanafanya mkakati wa maksudi tumewapa hela kidogo ili wazunguke.

Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane na Mbunge kwa kuwa mkakati huu utahamasisha vikundi vya Vijana na akina Mama kuzalisha mazao ya mbogamboga lakini kwa kiasi kikubwa tumekuwa tunazunguka huko kote EU na maeneo mengine ili kuwapatia masoko. Kwa hiyo hili linafanyiwa kazi na ninamshukuru Mbunge kwa kuliweka sawa.

Mheshimiwa Spika, hili lingine la mradi wa *TIIP* ni kweli kwamba mradi huu ulikuwa baina ya mwaka 1987 na 1997 kwa hiyo mradi huu una miaka kama 15 hivi tangu ulipomalizika, na Serikali haikuingiza pesa tena katika hili. Lakini naomba nimwambie kwamba katika mfumo mzima wa kurekebisha umwagiliaji na hili la mifereji ya asili tutalifikiria namna ya kulikabili.

SPIKA: Ahsante sana, tuendelee na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed.

Na. 490

Kuanzisha Kitengo cha Wagonjwa wa Kansa Mikoani

MHE. RUKIA KASSIM AHMED aliuliza:-

Hospitali ya *Ocean Road* ndiyo hospitali pekee inayohudumia wagonjwa wenye maradhi ya kansa nchini na wapo wengi ambao husafiri kutoka Mikoani kufuata matibabu hospitalini hapo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kitengo cha wagonjwa wa kansa katika Mikoa mingine nchini?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (K.n.y WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii jibu la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum kutoka *CUF,* ni kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, huduma kwa wagonjwa wa kansa zinatolewa katika kila hospitali za Mikoa na Wilaya ingawa ni kwa viwango tofauti. Wagonjwa ambao hawawezi kutibiwa katika hospitali za Mkoa hupewa rufaa kwenda kutibiwa katika hospitali za kanda na endapo mgonjwa atahitaji huduma zaidi hupewa rufaa kwenda katika hospitali ya ngazi ya Taifa. Ni kweli kuwa, kwa sasa hospitali ya ngazi ya Taifa inayotoa matibabu kwa wagonjwa wenye kansa za aina zote ni Taasisi ya *Ocean Road* tu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kupeleka huduma hizi karibu na wananchi, Serikali kwa kushirikiana na Hospitali ya Rufaa ya Bugando imeanzisha huduma za ngazi ya kitaifa katika hospitali hiyo. Awamu ya kwanza ya ujenzi wa majengo na uagizaji wa vifaa vya mashine za tiba pamoja na ile ya mionzi umekamilika.

Mpaka sasa Wagongwa karibu 4000 wameshatibiwa, na mashine za kutibu kansa kwa kutumia mionzi zilitegemewa kuwasili mwezi Juni, lakini kwa sababu ya matatizo ya usafiri zinategemewa kuwasili sasa mwezi Agosti, 2013.

Hii itakuwa ni hatua muhimu sana katika kusogeza huduma kwa wagonjwa karibu na wanapoishi, wagonjwa wenye matatizo ya kansa kutoka Kanda ya Ziwa wanaohitaji tiba za mionzi hawatalazimika tena kusafiri kwenda Dar es Salaam kupata huduma hiyo kama ilivyokuwa awali.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na juhudi za kusogeza huduma za afya za rufaa karibu na wanapoishi wananchi katika kanda nyingine zote kadiri ya hali ya uchumi itakavyoruhusu. *(Makofi)*

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Spika ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa, katika jibu lake la msingi alisema kuwa kuna vifaa vitapelekwa katika hospitali ya Bugando. Je, huko Bugando wafanyakazi mmewajengea vipi uwezo wa kuweza kuvitumia vifaa hivyo?

Mheshimiwa Spika, pili, Je, Serikali ina mkakati gani endelevu wa kukinga na kutibu maradhi haya hasa ukizingatia kuwa kinga ni bora kuliko tiba.

SPIKA: Ahsante, Naibu Waziri majibu. Uzuri wa Naibu huyu alishakuwa pia mtalaam pia wa afya, ni Daktari kabisa. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII): Mheshimiwa Spika, kweli kinga ni bora kuliko tiba na jitihada za Serikali zinaonekana wazi katika kuwasilisha huduma hizi na kutengeneza mikakati juu ya kupinga maradhi ambayo tunaita maradhi yasiyoambukizwa kansa ikiwemo.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, kwa upande wa kansa kumeshatayarishwa kitengo maalum pale Wizarani tangu mwaka 1988, kuna *Steering Committee* imeshatengenezwa na hivi sasa taaluma imeshatolewa katika hospitali za Mikoa ili huduma hizi ziweze kufika kule kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile nichukue nafasi hii kupongeza makundi yasiyo ya kiserikali ambayo yanashirikiana na Serikali katika ku-*screen* kumulika wale ambao wana kansa na wale ambao hawana kansa, jitihada zao pia tunazipongeza.

Lakini pia taaluma inayotolewa katika vyombo vya habari, magazeti kwamba kwa yale ambayo yanaweza kuepukika kwa mfano kufanya mazoezi, kutokuvuta sigara, kutokuwa na wapenzi wengi wa mara kwa mara.

SPIKA: Wapenzi lukuki. *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII): Mheshimiwa Spika, yote haya ni taaluma ambayo inatolewa na ninaomba Wabunge na wananchi wafuatilie.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Bugando, wakati kunapofanyika manunuzi makubwa kama haya, vipengele vitatu huwa vinahusishwa na hivyo vimehusika katika jambo hili la kuweka hizi nyenzo zetu pale Bugando.

Kwanza *specification* ya zile mashine zimetazamwa kwamba ziwe zinakidhi muda mrefu tena isije kuwa kama miaka miwili halafu ikabidi tukose *spare* kutokana na matatizo ya utandawazi na mbadiliko ya teknolojia yanavyoendelea. Lakini la pili ni kuwa na *guarantee* ndefu kwa ajili ya kutoa huduma vile vifaa ambavyo vitaingia mwezi Agosti.

Lakini tatu, ndiyo ambalo Mbunge amelitaka ni kwamba wakati tunaagizia hivi vifaa na mikataba yake, basi huwa kuna *component* ya kuwaelimisha, pamoja na kwamba tunao watalaam wetu wa ndani lakini kuwaelimisha

wale watendaji wa pale namna ya kugundua, namna ya kufuatilia na namna ya kutengeneza pamoja na kutumia *biomedical engineering team* ambayo ipo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge muda umekwisha sana, niwashukuru sana kwa maswali mazuri.

Waheshimiwa Wabunge naomba niwatambulishe wageni wetu leo, mnapoangalia *Speakers Gallery* tuna wageni wetu waliovalia rasmi, hawa si wengine ni Wabunge na Spika wanatoka Oman. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge mnakumbuka kama wiki tatu zilizopita nilitangaza wale wanaotaka kuanzisha kikundi cha urafiki na Wabunge wa Oman wajiandikishe, nakumbuka mlikutana na mkawa pia mme-*draft* ile *Memorandum of Understand* ambayo tumeweka saini.

Kwa hiyo Tume yangu ya Utumishi wa Bunge walikwenda Oman mwezi Februari, 2013 wakawa wamepokelewa vizuri na wenzetu na Naibu Spika aliongoza msafara huo.

Pamoja nao alikuwepo pia Katibu wa Bunge, walikwenda huko walipokelewa vizuri sana. Kwa hiyo na wao sasa wamerudisha ujumbe huu kwetu, wamefika kuanzia juzi, jana walifika hapa jioni. Wameweza kupata nafasi ya kuonana na Rais, ilikuwa waonane na Waziri Mkuu lakini mnajua mambo ndiyo haya tunamaliza haiwezekani.

Lakini wakitoka hapa wanaenda kutembelea *Kongwa Ranch,* wataondoka watakwenda Arusha baada ya Arusha watakwenda Zanzibar na watakuwa wanamaliza safari yao tarehe 2 Julai, 2013.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo marafiki zetu asubuhi hii mimi nimesaini *MOU* yaani maelewano ya urafiki. Kwa hiyo kikundi chetu cha urafiki mtaendelea kujiunga wengine ambao hamkusikia kwa sababu tutakuwa tunatembeleana sisi wenyewe, lakini pia tutakuwa ni chanzo cha kuwafanya wananchi wetu wazidi kushirikiana na wenzetu kwa sababu uhusiano wa Mbunge yeyote ni uhusiano wa wananchi. Kwa hiyo, hilo ndilo nataka tulifanye. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge pamoja na hayo naomba niwatambue. Ujumbe huu unaongozwa na Spika, Spika kijana kabisa katika Maspika wa Dunia, halafu kwa Bunge la Oman ndiye Spika wa kwanza aliyechaguliwa kidemokrasia wengine walikuwa wanateuliwa na Sultan.

Mheshimiwa Sheikh Khalid Bin Hilal Bin Nasir Al Maawal, Spika wa Bunge la Oman, Huyu ndiye Spika kijana lakini ameambatana na Waheshimiwa Wabunge kutoka Bunge hilo ambao ni Mheshimiwa Sheikh Ali Bin Nasir Al Mohrouqi ambaye ni Katibu wa Bunge, *the problem here the pronunciation may be very wrong. (Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge pia, wameongozana na Mbunge Mheshimiwa Khalid Bin Hilal Bin Hamed Al Nabhani, Yupo Mheshimiwa Mbunge Mheshimiwa Salim Bin Humood Bin Nassir Al Shulkal, tuna Mbunge mwingine Mheshimiwa Salim Bin Said Bin Musallam Al Hiraiz ahsante sana, tuna Mbunge Mheshimiwa Abdullah Bin Mohammed Bin Khair Al Bulush, Mbunge mwingine ni Mheshimiwa Mohamed Abdul Said, ahsante sana. (*Makofi*)

Wamefuatana na mtalaam wa masuala ya uhusiano ya Umma Ndugu Said Al Majid, Kuna Mkurugenzi katika Ofisi ya Spika Ndugu Abdul Salam Bin Abdullah Bin Yusuf Al Rashid, Tuna mwandishi wao wa Habari Ndugu Saif Bin Khalifa Bin Abdullah Al Kidy, Ahsante sana. (*Makofi*)

Tumefurahi sana kwamba mmepata nafasi ya kuja na kama tulivyokubaliana uhusiano wetu utajengeka, kwanza tunao uhusiano wa kihistoria toka zamani. Kwa Taifa la sasa tunaboresha utaratibu huo.

WABUNGE FULANI: *Gender*?

SPIKA: *Gender* kuna Mbunge mmoja kule mwanamke lakini hakuja. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna Wabunge 85 katika Bunge lake, Mbunge aliyechaguliwa kihalali mwanamke ni mmoja tu, sasa kwa sababu ni mmoja lazima alikuwa na shughuli nyingi kwa hiyo hakuja.

Baada ya utambulisho huu naomba wageni wetu watakwenda katika Ukumbi wa Msekwa pamoja nao naomba Wenyeviti wote wa Kamati za Bunge watakwenda kule, Kamati ya Mambo ya Nje na Wanachama rafiki wale mliojiandikisha juzi.

Kwa hiyo, baada ya utambulisho huo Kamati ya Mambo ya Nje watakwenda kule pia Kamati ya Uongozi na Tume pia watakwenda kule kuongea pia. Kwa hiyo, naomba niwakaribishe tena, ahsante sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge baada ya hayo pia nitangaze shughuli za kazi, Mwenyekiti wa Kamati, Haki, Maadili na Maadaraka ya Bunge, Mheshimiwa Brigedia Gen. Mstaafu Hassan Ngwilizi, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba saa saba na robo watakuwa na mkutano wao Chumba Na. 219.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Ulinzi na Usalama Mheshimiwa Anna Magreth Abdallah, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwmaba Saa Saba na Robo wakutane katika Ukumbi Na. 133.

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa *caucus* ya CCM anaomba niwakumbushe Wabunge wote wa CCM kuwa kesho Jumamosi, Saa Tatu Asubuhi, kutakuwa na kikao muhimu cha Chama katika Ukumbi wa Pius Msekwa, kuna wengine niliwaruhusu waende safari ninaomba waanze safari zao siku ya Jumapili ili kesho waweze kukutana.

Waheshimiwa Wabunge baada ya matangazo hayo, tuendelee, Katibu.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadilikoya Katiba ya Mwaka, 2013 *(The Constitutional Review (Amendment) Bill, 2013*

SPIKA: Kule nyuma msianze kuongea jamani, tuko ndani ya Bunge. Mstari anaokaa Komba. Mnaongea mno.

Muswada wa Sheria ya Kuraya Maoni wa Mwaka *2013 (The Referendum Bill, 2013)*

Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Akiba wa GEPF wa Mafao ya Wastaafu wa Mwaka, 2013 *(The GEPF Retirement Benefits Bill, 2013)*

Muswada wa Sheria ya Takwimu wa Mwaka 2013 *(The Statistics Bill, 2013)*

Muswada wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji wa Mwaka, 2013 *(The National Irrigation Bill, 2013)*

(Miswada yote mitano iliyotajwa hapo juu ilisomwa kwa Mara ya Kwanza)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nakala za Muswada uliotangazwa zipo, sasa ninachowaomba Waheshimiwa Muswada ukishasomwa mara ya kwanza maana yake uko *public.* Kwa wale wanaopenda kujifunza kuhusu hiyo Miswada na kuuliza Wataalam mbalimbali wanakokuwepo huko Miswada iko *public.*

Kwa hiyo, mnaweza kuanza na mingine kama hii ya *Referendum* na hii ya Marekebisho nini ya *The Constitutional Review Amendments* tutakuja, itakuja mwezi wa nane. Kwa hiyo, mkijiandaa vizuri huko tukifika hapa basi kazi inakuwa nzuri. Siyo tu na nyie mnakuja kuiona hapa hapa wakati imetangazwa.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2013
(The Finance Bill, 2013)

(Kusomwa mara ya Pili)
(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nilisema jana kwamba mazungumzo tulishamaliza kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge na nikawa nimeagiza kwamba wote walioleta Majedwali ya kufanya *amendments* wakakutane kwenye Kamati ya Bajeti na Wizara ya Fedha na Kamati ya Bajeti na wale wenye madokezo ya *amendments.*

Nawashukuru sana wote waliohusika. Naambiwa wamefanya kazi mpaka sijui saa ngapi usiku na wameamka asubuhi hii kuendelea kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, ili tuweze kupata mrejesho basi namwomba Mwenyekiti wa Bajeti atoe taarifa. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Bajeti. *(Makofi)*

SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. FELIX F. MKOSAMALI, MEMBER OF PARLIAMENT FOR MUHAMBWE CONSTITUENCY, AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE WRITTEN LAWS (MISCELLANEOUS AMENDMENTS) ACT, 2013"

Made Under S.O 86(9) & (11)

The Bill entitled "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2013" is amended as follows:-

A: By deleting Part II.

B: By re-numbering Part III and IV as Part II and III respectively.

C: By deleting the proposed Clause 8.

D: By deleting the word "may" appearing between the words "secretary" and "by" in the proposed Clause 29A and substituting for it the word "shall".

Dodoma
10th June, 2013

HON. FELIX F. MKOSAMALI (MB.)
MUHAMBWE CONSTITUENCY

SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HONORABLE MURTAZA MANGUNGU (MP.) DURING THE SECOND READING OF FINANCE ACT, 2013

Order 86(11)

Amendment
of Section 56The Bill entitled "the Finance Act 2013" is hereby amended -

(a) In Clause 56 by amending the proposed paragraph (c) as follows- deleting the words "sugar', "beverage", "spirits" and "petroleum products."

(b) In subsection (4), by retaining the figures 90% and 10%.

(c) By adding immediately after paragraph (c) the followingnew paragraph as follows:

(d) "Tanneries, ginneries, spinning mills, edible oil milling & refineries, fishing processing plants, sisal processing plants should be zero rated."

Dodoma
27th June, 2013

HON. MURTAZA MANGUNGU (MB.)
KILWA KASKAZINI CONSTITUENCY

SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HONOURABLE DR. HAMISI ANDREA KIGWANGALLA (MP.), DURING THE SECOND READING OF FINANCE ACT, 2013
S.O. 86(11)

Part VIII and X of the Finance Act 2013 be amended by removing the provisions of section 30, 31, 33, 34 and 35 and replacing them with the following words.

(a) Part VIII and IX propose to amend the National Parks Act (Cap. 182) and the Ngorongoro Conservation Area Act, (Cap.284) with the view not to impose any requirement on the Agencies, Authorities or Government Institution, to submit 10% of its annual gross revenue to the government.

(b) The government shall sell its shares on the National Bank of Commerce equivalent to the amount of revenue affected by the Amendment on part VIII and IX of the Finance Act, 2013.

(c) Part X and XI propose to amend Ports Act (Cap. 166) and the Public Finance Act (Cap. 348) respectively with the view to impose a requirement on agencies, Authorities or government institutions to submit 10 percent of its annual gross revenue so as to increase government revenue.

Part VII is amended by amending section 11 and 19 of the Income Tax Act Cap. 332 by adding the following words immediately after the word "distinct mining area.'

or "Projects owned by a single company" and immediately after a word "petroleum area" by adding the following words charging 6 percent windfall gains tax.

Part XIX is amended by adding the following words after the words "Major investors", in mineral resources, gemstones, gas and oil.

Part XXI is amended by removing the 5% charge of development levy on Vocational Education and Training Act (Cap.82) by retaining the 6 percent. The deficit will be recovered from windfall tax change.

Part XIV is amended by removing the proposed amendment and by retaining 200 Tsh. on fuel levy as in principal Act.

Part XXII of the Bill proposes amendments to the VAT Act Cap. 148 by restoring the provisions of item 14 to the Second Schedule of the principal Act.

The revenue so affected by intended amendment shall be recovered by selling part of the Government shares owned in the Airtel Tanzania Ltd.

Dodoma
26th June, 2013

HON. DR HAMISI A. KIGWANGALLA (MB.)
NZEGA CONSTITUENCY

SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. WILLIAM A. MGIMWA THE MINISTER FOR FINANCE AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE FINANCE ACT, 2013"

(Made under S.O. 86 (10)(b))

The Bill entitled "the Finance Act, 2013" is amended-

A: In the ARRANGEMENT OF PARTS by-

(a)inserting immediately after PART II the following: "PART III AMENDMENT OF THE EDUCATION FUND ACT, (CAP.412)"; and

(b) renaming Parts III to XXII as Parts IV to XXIII respectively.

B: By adding immediately after Part II the following new Part:

"PART III
AMENDMENT OF THE EDUCATION FUND ACT,
(CAP.412)

Construction *Cap.412* **5.** This Part shall be read as one with the Education Fund Act hereinafter referred to as the "principal Act".

Amendment of section 13 **6.** The principal Act is amended in section 13 by-

(a) adding immediately after paragraph (a) the following new paragraph:

"(b)excise duty of 2.5% imposed on electronic communication service as provided for under the Excise (Management and Tariff) Act;";

(b) renaming paragraph (b) as paragraph(c).

C: In Clause 8 by deleting the definition of the term "telecommunication service" and substituting for it the following:

““electronic communication service” means a service of any description provided by a person or a company by means of any transmission, emission or reception of signs, signals, writing, images and sounds or intelligible information of any nature, by wire, optical, visual or other electromagnetic means or systems, including-

(a)voice, voice mail, data services, audio text services, video text services, radio paging and other emerging electronic communication services;

(b)fixed telephone services including provision of access to and use of the public switched or non-switched telephone network for the transmission and switching of voice, data and video, inbound and outbound telephone service to and from national and international destinations;

(c)cellular mobile telephone services including provision of access to and use of switched or non-switched networks for the transmission of voice, data, video and Value Added Services inbound and outbound roaming service to and from national and international destinations;

(d)carrier services including provision of wired, optical fiber or wireless facilities and any other technology to originate, terminate or transit calls, charging for interconnection, settlement or termination of domestic or international calls, charging for jointly used facilities including pole attachments, charging for the exclusive use of circuits, a leased circuit or a dedicated link including a speech circuit, data circuit or a telegraph circuit;

(e)provision of call management services for a fee including call waiting, call forwarding, caller identification, multi-calling, call display, call return, call screen, call blocking, automatic call-back, call answer, voice mail, voice menus and video conferencing;

(f)private network services including provision of wired, optical fiber, wireless or any other technologies of electronic communication link between specified points for the exclusive use of the client;

(g)data transmission services including provision of access to wired or wireless facilities and services specifically designed for efficient transmission of data; and

(h)communication through facsimile, pager, telegraph, telex and other electronic communication services."

D: In Clause 9, by-

(a)deleting the term 'telecommunication service" appearing in the proposed subsection (3) and substituting for it the term "electronic communication service"

(b)deleting the term "telecommunication service" appearing in paragraph (b)(i) and substituting for it the term "electronic communication service."

(c)adding immediately after paragraph (d) the following new paragraph:

"(e) by adding immediately after subsection (6) the following new subsections:

"(6A) There shall be charged an excise duty on money transfer through a bank, a financial institution or a telecommunication company at the rate of **0.15**% of the amount transferred for the amount exceeding shillings 30,000/=.

(6B) The excise duty chargeable under subsection (6A) shall not apply to money transfer between banks and financial institutions, government, diplomats and diplomatic mission.

(6C) There shall be charged an excise duty on telecommunication sim card at the rate of shillings **1,000**/= per month."

E: By adding immediately after Clause 9 the following new Clause:

"Amendment of section 125 **9A**. The principal Act is amended in section 125(1) by-

(a) deleting paragraph (d) and substituting for it the following:

"(d) any electronic communication service supplied by electronic communication service provider at the time when such mobile, fixed or wireless phone is in use or when payment is received for the service whichever time shall be the earliest."

(b) by adding immediately after paragraph (e) the following:

"(f) money transfer service by a bank, financial institutions or a telecommunication service provider;

(g) any telecommunication sim card by telecommunication service provider."

F: In Clause 10, by-

(a) by inserting immediately after HS Code 2710.11.20 the following column, row and contents:

	— medium oil and preparations		
2710.19.22	**-— Illuminating kerosene (Ik)**	**Tshs.400.30 per Litre**	**Tshs.475 per Litre**

(b) by deleting the whole of HS Code 2710.19.31;

(c) adding immediately after the word "vehicle" appearing at the end of heading 88.02 the words "for pleasure or sports";

(d)by inserting immediately after the word "aircraft" appearing under HS Code 8802.30.00 the words "for pleasure or sports";

(e) by inserting immediately after the word "aircraft" appearing under HS Code 8802.40.00 the words "for pleasure or sports".

G: In Clause 14 by deleting the reference to section 31(1) and substituting for it the reference to section 31(2).

H: In Clause 16 by-

(a) n the definition of the term "contract area" by adding immediately after the word "contract" appearing in the third line the word "area";

(b) in the definition the term "petroleum agreement" by deleting the word "it" appearing in the third line.

I: By deleting Clause 17.

J: In Clause 20 by-

(a)deleting the reference to subsection (3) appearing in the opening phrase and substituting for it the reference to subsection (4); and

(b) re-designating the proposed subsections (4) and (5) as subsections (5) and (6) respectively.

K: In Clause 24 by deleting the words "subsection (1)" appearing at the end of Clause 24 and substituting for it the words "paragraph (d)".

L: In Clause 27-

(a)by deleting the proposed amendment under paragraph (b) and substituting for it the following:

"(b) in paragraph 3, by renumbering the repeated subparagraph (3) as subparagraph (4)."

(b)in the proposed amendment of paragraph 4(c) by inserting the word "money" between the words "of" and "transfer" appearing in item (iv).

M: In Clause 39, by-

(a) deleting the word "budget" appearing in proposed subsection (2) and substituting for it the words "annual gross revenue";

(b)adding immediately after the proposed subsection (3) the following:

"(4) An Agency, Authority or public institution that fails to remit ten percent of its annual gross revenue as required under this section, shall in addition to such ten percent, pay a penalty of five percent of the amount payable by it under this section.

N: In Clause 41 by adding immediately after the proposed subsection (3) the following:

"(4) All unsolicited private partnership projects shall be procured in the manner prescribed in the Regulations made under this Act."

O: In Clause 44 by deleting the proposed subsection (2).

P: By deleting Clause 65.

Q: By-

(a) renaming Clause 5 to 66 as Clause 7 to 67;

(b) renaming Parts III to XXII as Parts IV to XXIII.

Dodoma, **WAM**

....., 2013 *MF*

FURTHER SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. WILLIAM A. MGIMWA THE MINISTER FOR FINANCE AT THE SECOND READING OF A BILL ENTITLED "THE FINANCE ACT, 2013"

(Made under S.O. 86 (10)(b))

The Bill entitled "the Finance Act, 2013" is further amended by deleting Paragraphs F to K of the Schedule of amendment and substituting for them the following-

"**F**: In Clause 10, by-

(a) deleting HS Code 2710.11.10;

(b) deleting HS Code 2710.11.20 and substituting for it the following column, row and contents:

	—medium oil and preparations		
2710.19.22	**—— Illuminating / kerosene (Ik)**	**Tshs. 400.30 per Litre**	**Tshs.425 per Litre**

(c) deleting the whole of HS Code 2710.19.31;

(d) deleting the whole of HS Code 3304.99.00 and substituting for it the following:

3304.99.00	**—other**	**10%**
	Sunscreen or suntan preparations	**0%**

(e)adding immediately after the word "vehicle" appearing at the end of heading 88.02 the words "excluding commercial aircrafts".

G: In Clause 14 by deleting the reference to section 31(1) and substituting for it the reference to section 31(2).

H: In Clause 16 by-

(a)in the definition of the term "contract area" by adding immediately after the word "contract" appearing in the third line the word "area";

(b)in the definition of the term "petroleum agreement" by deleting the word "it" appearing in the third line.

I: By deleting Clause 17.

J: In Clause 20 by-

(a)deleting the reference to subsection (3) appearing in the opening phrase and substituting for it the reference to subsection (4); and

(b)re-designating the proposed subsections (4) and (5) as subsections (5) and (6) respectively.

K: In Clause 24 by deleting the words "subsection (1)" appearing at the end of Clause 24 and substituting for it the words "paragraph (d)".

L: By deleting Clause 25.

M: By renumbering Clauses 26 and 27 as Clauses 25 and 26 respectively.

N: In Clause 26 as renamed-

(a)by deleting the proposed amendment under paragraph (b) and substituting for it the following:

"(b) in paragraph 3, by renumbering the repeated subparagraph (3) as subparagraph (4)."

(b) in the proposed amendment of paragraph 4(c) by inserting the word "money" between the words "of" and "transfer" appearing in item (iv).

O: By deleting Clause 28.

P: By renumbering Clause 29 to 64 as Clause 27 to 62 respectively.

Q: In Clause 37 as renumbered -

(a)deleting the word "budget" appearing in proposed subsection (2) and substituting for it the words "annual gross revenue";

(b) adding immediately after the proposed subsection (3) the following:

"(4) An Agency, Authority or public institution that fails to remit ten percent of its annual gross revenue as required under this section, shall in addition to such ten percent, pay a penalty of five percent of the amount payable by it under this section."

R: In Clause 39 as renumbered by adding immediately after the proposed subsection (3) the following:

"(4) All unsolicited private partnership projects shall be procured in the manner prescribed in the Regulations made under this Act."

S: In Clause 42 as renumbered by deleting the proposed subsection (2).

T: By deleting Clause 65.

U: By-

(a) renumbering Clauses 65 and 66 as Clauses 63 and 64 respectively;

(b) renaming Parts III to XXII as Parts IV to XXIII."

Dodoma, **WAM**

……., 2013 *MF*

MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, kama ulivyoelekeza jana jioni Kamati ya Bunge ya Bajeti ilikutana kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Timu yake kwa lengo la kupitia na kuchambua mapendekezo ya marekebisho ya Muswada wa Fedha yaliyowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge saba kwa madhumuni ya kuuboresha. Jumla ya majedwali ya marekebisho saba yaliwasilishwa na Waheshimiwa Wabunge wafuatao:-

Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Murtaza Mangungu, Mheshimiwa Ezekia Wenje, Mheshimiwa Margdalena Sakaya, Mheshimiwa John Mnyika na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla. Mapendekezo mengine yaliyowasilishwa ilikuwa ni pamoja na Jedwali la Marekebisho yanayopendekezwa na Serikali na pendekezo la Kamati la kurekebisha baadhi ya vifungu vya Muswada.

Kamati ilipitia Muswada kifungu kwa kifungu ili kutoa fursa kwa wenye hoja za mabadiliko kutoa hoja zao pindi vifungu husika vinapofikiwa. Ilisisitizwa kwamba utoaji wa hoja za marekebisho uzingatie sharti la Kanuni ya 109 Fasili ya pili. Hoja kadhaa ziliwasilishwa na wahusika kupendekeza kufanya marekebisho yaliyokusudiwa. Hata hivyo, kwa baadhi ya hoja zilizowasilishwa Kamati ilipata ugumu wa kukubaliana na baadhi ya mapendekezo ya hatua za kufikia pengo litakalotokana na mabadiliko yanayopendekezwa na kwa baadhi ya hoja Kamati ilipata ugumu kukubali hoja zilizowasilishwa kutokana na uhitaji wa mabadiliko ya Sheria nyingine zaidi ya zile zilizokusudiwa katika Muswada.

Kamati ilitoa mapendekezo stahiki kwa kila hoja ili kuzitendea haki. Zipo pia hoja kadhaa ambazo zilikubaliwa na Kamati pamoja na Serikali na hivyo itaingizwa katika Jedwali la Marekebisho la Serikali. Aidha, wakati wa uchambuzi huo huo mtoa hoja mmoja aliamua kuondoa kwenye Kikao bila kuaga na hakurejea tena. Hivyo Kamati ilishindwa kuendelea na uchambuzi wa hoja zake kwa kuwa pale alipohitajika kutetea hoja zake kwa mujibu wa Kanuni hakuweza kufanya hivyo kwa vile hakuwepo.

Aidha, watoa hoja wengine wawili waliomba kuiachia Kamati iendelee kujadili hoja nyingine ili waweze kujipanga vyema kutetea hoja zao kwa kuwa na takwimu sahihi. Nieleze tu kwa kifupi maeneo ambayo yalijadiliwa. Kwa Mheshimiwa Magdalena Sakaya alijielekeza kifungu cha sita cha Muswada pendekezo la kuondoa *TANAPA* katika kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali asilimia 10 ya mapato ghafi. Eneo hili Kamati haikuliafiki. Mheshimiwa Ezekia Wenje, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na wenyewe katika eneo hili walikuwa na mawazo hayo hayo kama ya Mheshimiwa Sakaya. Mheshimiwa John Mnyika alijielekeza kwenye kifungu cha 8(e) ambalo ni pendekezo kuondoa maneno *co-walking* na *voice manual* katika Muswada unaopendekezwa.

Kamati imeridhisha na uamuzi wa Serikali katika kuongeza wigo wa kutoza kodi katika maeneo haya iwapo mtoa huduma ataanza kutoza tozo ya matumizi kwenye huduma hizo. Katika hili Kamati imezingatia kuwa matumizi ya huduma hizi ni hiari ya mtu kuchagua kutumia au kutotumia. Hivyo imeridhika kuwa zitozwe na kwa maana nyingine sasa Kamati haikuafiki pendekezo la Mheshimiwa Wenje. Pia alitaka kwenye kifungu cha 9(c) ya Muswada kuondoa maneno 25 na kuweka maneno 20 kwa maana kiwango cha ushuru. Mpendekezaji hakuiridhisha Kamati kulingana na Kanuni ya 109 Fasili ya pili. Kwa maana nyingine pendekezo hilo halikuafikiwa na Kamati. Kwa Mheshimiwa Mnyika, kifungu 9 kama kilivyorekebishwa na Serikali. Pendekezo lake la kutaka kiwango cha tozo kishuke kutoka asilimia 0.15 na kiwe asilimia 0.1 hakikuafikiwa na Kamati kwa sababu hakizingatii matakwa ya Kanuni ya 109(2).

Mheshimiwa Jitu Soni, Kifungu cha 10 cha Muswada. Pendekezo la kuongeza ushuru kwenye juice zinazoingizwa kutoka nje ya nchi kutoka shilingi, zinazopendekezwa na Serikali 110 kwa lita kwenda shilingi 200 kwa lita. Pendekezo hili Kamati haikuliafiki. Kifungu cha 10 pendekezo la kuongeza maneno katika *HS Code 33.4.* Maneno yanayopendekezwa yatawasilishwa katika Jedwali la Marekebisho na kwa maana

hiyo Kamati ililiafiki pendekezo la Mheshimiwa Soni.

Kwa upande wa kifungu cha 10. Kulikuwa na pendekezo la Mheshimiwa Serukamba. Kwa upande wa ndege. Pendekezo lilikuwa katika marekebisho ya Serikali imetumia maneno ndege ambazo zitaingizwa nchini kwa matumizi ya michezo na starehe *for pleasure and sports.* Pendekezo la Mheshimiwa Serukamba ambalo Kamati iliafiki ni kwamba tuyafute maneno ya *for pleasure and sports* na tuweke maneno mbadala yatakayosomeka *excluding commercial aircraft* kwenye *HS Code 88.02, 88.02.30* na kwenye *HS Code 88.02.40.00.* Eneo hili, pendekezo hili liliafikiwa na Kamati. Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, yeye alijielekeza kwenye kifungu cha 18 cha Muswada. Pendekezo la Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla lilikuwa ni kuongeza maneno mapya katika kifungu hiki. Kamati imeridhika kuwa pendekezo la marekebisho lililotolewa na Serikali linajitosheleza na hivyo hapakuhitajika kuongeza maneno ambayo Mheshimiwa Kigwangalla alikuwa anapendekeza.

Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla pia alipendekeza kwenye eneo hilo kuongeza kifungu kidogo kipya cha 5 chenye maneno *charging six percent win for gain tax.* Kamati iliona kwamba utekelezaji wa pendekezo hili utakuwa ni mgumu sana. Kwa sababu kwanza ni la kisera na pili linahusisha marekebisho katika Sheria nyingine na katika hatua hiyo Kamati haikuweza kuliafiki.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla pia alikuwa na mapendekezo katika kifungu cha 30, kifungu cha 31 na 32 na 33, 34 na 35. Mapendekezo haya yalifanana na lile la kwanza kuhusiana na tozo ambayo Serikali, uchangiaji ambao Serikali inapendekeza kwa mashirika, taasisi za Serikali na mamlaka ya udhibiti wa asilimia 10 ya mapato ghafi yapelekwe kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.

Eneo hili kwa sababu halikuafikiwa tangu awali Kamati iliendelea kusema lisikubalike katika eneo hilo pia. Lakini Kamati ya Bajeti ilikuwa na maoni katika kifungu cha 25 cha Muswada ambacho kinahusu *transfer pricing* na

ilishauri badala ya kuongeza pendekezo la Serikali la miaka 6 Kamati ilishauri kipindi cha miaka mitatu cha ukomo kiendelee kutumika kama Sheria inavyotaka hivi sasa. Serikali iliiliafiki pendekezo hili na Serikali itawasilisha Jedwali la Marekebisho katika eneo hili.

Kifungu cha 28 Mheshimiwa Serukamba alikuwa na mapendekezo ya kuondoa pendekezo hili kwenye eneo la Muswada na Serikali iliiliafiki na hivyo Kamati imeliafiki pendekezo hilo. Mheshimiwa Mangungu kifungu cha 56 mapendekezo ilikuwa ni kubadili kifungu hicho kwa kuondoa baadhi ya maneno. Pendekezo hilo liliafikiwa na Kamati pamoja na Serikali. Kwa sababu yanayopendekezwa na Serikali yanashabihiana kabisa na yale ambayo Mheshimiwa Mangungu alikuwa anayapendekeza.

Pendekezo la pili la kubakiza tozo la awali katika viwango vya asilimia 90 na 10. Pendekezo hili, Serikali tulikuwa na majadiliano, Serikali ilisema italifanyia tathmini eneo hili mwaka ujao wa fedha ili kujiridhisha na kiasi cha mapato ambacho kinatokana na hatua hiyo na kwa maana hiyo halikuafiwa.

Kulikuwa na pendekezo la kuongeza aya mpya ya (c) katika kifungu cha 56. Lakini Kamati haikuafiki pendekezo hilo. Kwa upande wa Mheshimiwa Soni alikuwa na pendekezo liligusa kwenye sheria la ongezeko la thamani yaani VAT. Kwenye jedwali la 3. Kimsingi mapendekezo ya Mheshimiwa Soni yaliafikiwa. Lakini kwa sababu yanahitaji yafanyiwe kazi na Serikali.

Kamati iliafiki kwamba Serikali iyachukue mapendekezo haya mazuri ya Mheshimiwa Soni kwa sababu uamuzi wa Serikali ulishatolewa huko nyuma lakini utekelezaji wake umekuwa ni mgumu ambao unalenga kuwasaidia wakulima wetu katika vifaa vya kilimo ili wasiweze kutozwa kodi ya ongezeko la thamani. Sasa tunasema uamuzi wa Serikali utekelezwe lakini utekelezwe vizuri na Serikali imelichukua eneo hili wakalifanyie kazi na watakuja nalo

katika Bunge la mwezi wa nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho lilitokana na Kamati ya Bunge lako Tukufu, Kamati ya Bajeti na hili linahusu kubadilisha viwango vya tozo za mafuta kulingana na viwango vilivyopendekezwa na Kamati yako. Sasa tulikuwa na, niseme kabisa Waziri atakuja kulieleza vizuri tu. Lakini tuseme tumekuwa na muafaka mzuri kwenye eneo hili na Serikali imekubali kuleta kupitia Jedwali la Marekebisho uamuzi sahihi unaotokana na mashauriano ya Kamati. Lakini ni habari njema sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Kwa mara nyingine tena, niliwaeleza jamani jana katika maelezo yangu na maagizo yangu. Kazi ya kufanya marekebisho kwenye Muswada wa Fedha siyo maneno ni hesabu. Kwa hiyo, maana tukaita Kamati ile pamoja na Serikali wakatufanyie hesabu. Kwa hiyo, wengine wote wenye Majedwali hawakuwepo. Majedwali yote yamemalizika. Kwa hiyo, sasa namwita Waziri wa Fedha, mtoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote. Awali ya yote napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti pamoja na Kamati yake yote kwa namna ya pekee, Mheshimiwa Mtemi John Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi, pamoja na Kamati yake yote, kwa kukaa na mimi na Wasaidizi wangu mpaka saa 6.00 ya usiku ili kuhakikisha kwamba kazi hii inakamilika vizuri na Waheshimiwa Wabunge wanapata majibu yaliyo sahihi. *(Makofi)*

Vile vile nachukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika, kwa kutupa nafasi kuyafanyia kazi haya yote kwa muda mzuri na kwa usaidizi unaotufanya tufanye kazi zetu vizuri. Aidha napenda kutoa shukrani za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote mliochangia Muswada huu kwa kuzungumza hapa Bungeni na wale waliochangia kwa

maandishi. Nawashukuru kwa maoni na ushauri wenu.

Vile vile nachukua nafasi hii kwamba utekelezaji wa Bajeti tutauzingatia na kuhakikisha kwamba Bajeti inatekelezwa kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge kumekuwa na maswali mbalimbali kabla na baada ya kuwasilisha wasilisho langu. Sasa Mheshimiwa Spika, naomba nielekee katika kutoa majibu ya hoja mbalimbali Waheshimiwa Wabunge mlizozitoa hapa Bungeni kama ifuatavyo:-

Kwanza, kumekuwa na maswali na ombi kwa Serikali kwamba tutazame kodi za mafuta ya dizeli, petroli na mafuta ya taa kwa mwelekeo wa kuzipunguza ili kuleta unafuu na kuzuia mfumuko wa bei unaoweza ukatokana na mabadiliko ya bei za mafuta.

Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge wote jambo hili tumelifanyia kazi pamoja na Kamati ya Bajeti na tumekuja muafaka katika tozo ambazo Serikali itaziweka kwenye mafuta kama ifuatavyo: Ninapendekeza kwa Waheshimiwa Wabunge tukubaliane nazo.

Kwanza kuendelea kutoza ushuru wa bidhaa yaani *exercise duty* kwenye mafuta ya petroli kwa kiwango cha shilingi 333 kwa lita. Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba hii ndiyo iliyopo. *(Makofi)*

Pili, kuendelea kutoza ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya dizeli kwa kiwango cha sasa cha shilingi 215 bila kuongeza hata senti moja kwa kila lita. Hii kukidhi hoja na maombi ya Waheshimiwa Wabunge na kwa kuzingatia hali halisi ambayo Uchumi wetu unatakiwa u-*stabilize. (Makofi)*

*T*atu, kutoza ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya taa kwa kiwango cha shilingi 425 kwa lita badala ya shilingi 400 na senti 30 zinazotozwa kwa dakika hii. Nitatoa maelezo.

(Makofi)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge hatua hizo hapo juu nilizozieleza zinatarajiwa kuondoa tatizo la uchakachuaji wa mafuta unaotokana na uchanganyiaji wa mafuta ya taa na dizeli na kwa hali hiyo ni lazima tuwe na hesabu sahihi ambazo zitasaidia tunaangalia upande wa kupunguza mfumko wa bei na pili tunaangalia tatizo linazoloweza likahamasisha wafanya biashara kuchanganya mafuta na kuingia katika tatizo lililo kubwa zaidi.

Aidha Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote hatua hizi zitaongeza mapato ya Serikali na kuchochea na kuboresha mahusiano ya biashara na nchi zetu jirani ambazo zina-*import* mafuta kupitia bandari ya Dar es Salaam. Hatua hizi nilizozisema za ushuru wa bidhaa zitazuia kishawishi cha kuchanganya mafuta. Kwa hivi hali yetu itakuwa salama. *(Makofi)*

Na nne, kuongeza ushuru wa mafuta yaani *fuel levy* ya *petrol.* Kutoka shilingi 200 kufika shilingi 263 kwa lita. Lengo la hatua hii ni kuongeza mapato ya Mfuko wa Barabara nchini, ili kugharamia ukarabati wa barabara zinazotarajiwa kujengwa mwaka huu na kumalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilisema awali kwamba tumetenga fedha, lakini tunataka fedha yote ikamilike ya *1.22 trillion* ili barabara zile zinazofika vijijini kwa ajili ya kubeba mazao ambazo zimeanzishwa ziweze kumalizika. Ongezeko hili linalenga kwenda kukidhi kumaliza kazi ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tano, kuongeza ushuru wa mafuta yaani *fuel levy* kwa mafuta ya dizeli. Kutoka shilingi 200 hadi shilingi 263 kwa lita. Lengo hili Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na kwamba ni kuongeza mapato vile vile ni kusakidia kugharamia ukarabati wa ujenzi wa mabarabara tena. Fedha hizi tunaelekeza huko.

Mheshimiwa Spika, sita, kuanzisha ada ya mafuta yaani *petroleum levy* hii tumeshaianzisha ya shilingi 50 kwa kila lita kwa mafuta ya *petrol,* dezeli na mafuta yale ya taa.

(Makofi)

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zote nilizozisema kwa pamoja zinatarajia kuiingizia Serikali shilingi bilioni 298.0993. Hizi ni hela zitakazopatikana kutokana na hatua hizi na tutaelekeza kwenye mabarabara tuone zinafanya kazi nzuri pamoja na Mfuko wa *REA. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushuru wa bidhaa kwenye huduma za simu lilikuwa swali la Waheshimiwa Wabunge kwamba lisihusishe huduma za kutuma kwa kupokea fedha kwa kutumia simu.

Mheshimiwa Spika, huduma ya kutumia ya kutuma na kupokea fedha kwa kutumia simu imekuwa kwa kiasi kikubwa sana sasa. Tafsiri mpya ya *electronic communication services* kama ilivyowasilishwa kwenye Kamati ya Bunge ya bajeti ya Mamlaka ya Mawasiliano yaani *TCRA* haimaanishi kwamba ushuru wa bidhaa unatozwa katika huduma za kutuma na kupokea fedha kwa njia ya mtandao na simu. Ushuru huu wa bidhaa utatozwa kwenye huduma nyingine kama vile huduma za kupiga simu. Kutuma ujumbe wa maandishi, picha, milio ya simu na huduma zingine kadhalika.

Kwa hivi hili, linafafanua umuhimu wa kuwa na tafsiri mpya ya *electronic communication services.* Swali lingine la muhimu lilikuwa tutoe tafsiri ya maneno *electronic communication services* kwamba iangaliwe upya ili kuepusha uwezekano wa kuwa na *double taxation.* Tumelitazama Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge. Tumelitazama neno hili au huduma hii kwa minajili ya kuchunguza kama kweli tunaweza kukawa na kodi mbili. Kwa sababu ya mahusiano.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchunguza kwa ndani Kamati ya Bajeti ni kweli ilitushauri kwamba inawezekana kwa namna moja au nyingine kukawepo na utozaji wa kodi mbili au mara mbili yaani *double taxation.* Katika tafsiri hiyo iwapo mtu ataunganishwa na simu kutoka kampuni moja kwenda

kampuni nyingine.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge ushauri huu wa Kamati tumeupokea na tutaangalia upya tafsiri hiyo kwa kulingana tukishirikiana na *TICRA* ili kuepusha uwezekano wa mtu kuchajiwa mara mbili ili inapoweza ikatokea.

Kwa hivi Serikali tutashirikiana na *TCRA* tuone namna ya kulizuia hilo ili mpiga simu au anayetumia huduma hizo za simu kusiwepo na uwezekano wa kuingia kwenye *double taxation.*

Vile vile kulikuwa na ombi kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza kodi za magari chakavu. Ushuru katika magari chakavu. Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba nilieleza kwamba magari chakavu yenye umri wa zaidi ya miaka 10 ya aina mbili yaani magari yasiyo ya uzalishaji yaani *non-utility motor vehicles* kwamba Serikali tulipendekeza ushuru upande kutoka asilimia 20 mpaka 25 kwa sababu zile nilizozieleza za uchakavu unavyoweza ukaathiri hali yetu ya uchumi pamoja na kuharibu mazingira na kuleta gharama ya *maintenance* ya magari yaliyochakaa pamoja na mazingira.

Mheshimiwa Spika, vile vile upande mwingine nilipendekeza kwamba magari yale ya uzalishaji yenye umri unaozidi miaka kumi nayo yamechakaa kwa hivi ushuru tulipendekeza upande kwa asilimia 5. Kwa maana ya ku-*discourage* kutumia magari ambayo tayari kwa kusema kweli yanatuletea matatizo zaidi kiuchumi kuliko kutusaidia.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge kauli hii haikumaanisha kwamba Serikali inapiga marufuku kuagiza magari hayo. Tunasema tunapoagiza magari yaliyochakaa tunaingia katika mgogoro mwingine lakini basi yule anayeagiza walau achangie katika gharama zaidi kwa sababu yanakuja kuharibu *environment* lakini vile vile hatukiuondoa masharti katika magari mapya.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ya tano yenye uzito ni kwamba Waheshimiwa Wabunge waliuliza kama

inawezekana kuangalia upya zile adhabu ambazo tulipendekeza kwa wale ambao hawatatumia *electronic tickets* hawa ni wale wafanyabiashara ambao hawatozwi *VAT*. Kwamba Serikali sasa ili kudhibiti mapungufu au wizi wa fedha zinazotokana na kukwepa ushuru basi tuweze tukatumia walau *electronic tickets* ili kuwa utaratibu wa kuzuia.

Mheshimiwa Spika, tuliweka adhabu tatu, sasa Waheshimiwa Wabunge wengine wakasema kwa nini ziwe adhabu tatu wengine wakasema kwa nini isiwe adhabu moja na wengine waka-*suggest* kwamba mtu wa namna hiyo kwa nini asizuiwe kabisa kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, tumepokea maoni ya Waheshimiwa Wabunge kwa sasa Serikali bado ina amini kwamba adhabu zile tatu kosa la kwanza, kosa la pili mpaka kosa la tatu kwanza tunawapa wafanyabiashara kama nafasi ya kujifunza kwamba kila kosa utaadhibiwa.

Kwa hiyo, tunawapa nafasi ya kujifunza na ku-*comply* ili Serikali iweze kupata kinachostahili kama kodi kwa ajili kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge hoja nyingine ilikuwa ni msamaha wa kodi ya zuio kwa malipo ya ukodishaji wa ndege yanayolipwa kwa makampuni ya nje wakati tunakodi au kampuni za Tanzania zinakodisha ndege ifanye kazi hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu hatuna kiwanda cha kutengeneza ndege au ununue ndege mpya au ukodishe ndege ili uje ufanye biashara ya *aviation* hapa Tanzania. Utaratibu wa biashara za namna hii nilieleza hapa Bungeni kwamba malipo yale kiutaratibu tunatakiwa na sisi tukate *withholding tax* lakini Waheshimiwa Wabunge pamoja na kamati ya fedha kwa hekima zake kamati ya Bajeti ya Bajeti kwa hekima zake tumesikiliza kwamba walau tungesogeza mbele ili wafanyabiashara wa ndege wapate kujitayarisha katika kipindi hiki wakati msamaha ule

tunakwenda kuu-*implement.*

Mheshimimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge azimio hili la kuondoa huu msamaha tumelisogeza mbele mpaka julai mwaka kesho ili kuwe na matayarisho ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko mengine yameshaelezwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa kamati ya Bajeti maelezo ambayo ameeleza kwamba tumekubaliana kiufupi Serikali ndivyo tulivyokubaliana. Tumekubaliana juu ya bei hizi mpya za mafuta na wote tuko kauli moja Serikali na kamati ya Bajeti.

Tumekubaliana juu ya ku-postpone kodi ya zuio kwa ndege ambazo tunakodisha kutoka nchi za nje wote tumekubaliana. Katika haya ni masuala ya msingi na natolea maelezo haya kwa sababu haya ndiyo yalikuwa ya msingi katika mahusiano ya mjadala kati ya Serikali pamoja na Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, tulipokea maombi au ushauri mwingine kutoka Kamati ya Bajeti ukihusu namna tunavyoweza tukapata mapato mbadala kutoka vyanzo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote nachukua nafasi hii kwa dhati kabisa kushukuru Kamati ya Bajeti kwa mapendekezo yao mazuri. Kulikuwa na hoja kwamba kwa sababu ya kuharakisha kupata mapato mbadala tufukie maeneo ambayo tunahitaji mara moja kupata fedha walikuwa wamependekeza mambo karibu matatu.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni kuangalia namna tunavyoweza tukapata fedha kutoka mashudu ili isaidie kama kungekuwa na upungufu unaotakana na bei za mafuta sasa hilo bei za mafuta tumesha *resolve* lakini bado tumepokea hili na kulifanyia kazi na Serikali tunaahidi tunalifanyia kazi suala la mashudu kwa maana ya kuangalia *export levy* inavyoweza tukai-*raise* kutokana mashudu

yanayotokana na mbegu zetu tunazolima hapa, mazao tunayolima hapa nchini.

Pili, kamati ya Bajeti imekuja na mapendekezo ya kuangalia namna gani sasa kuanza kupata mapato sahihi kutoka Mapato kutoka *deep sea fishing*. Uvuvi katika bahari yetu. Tumelipokea pendekezo hilo, kwa mikono miwili kutoka Kamati ya Bajeti. Sisi Serikali tunajipanga kulifanyia kazi na tutakuja na jibu kipindi kinachokuja.

Haya ni mapendekezo makubwa ambayo Kamati Bajeti pamoja na mambo mengine imeletwa ndani ya Serikali tukijumuisha na mapendekezo mengine waliyotupa. Tunatizama kwamba, haya wanayozungumza hasa mawili mashudu pamoja na deep sea fishing, ni vyanzo ambavyo vitakuja kutupa Serikali mapato makubwa. Runaendela vilevile kutazama namna gani, kodi ambazo tunaweza tukapata katika vyanzo vingine vya madini , tunaifanyia kazi. Uwekezaji katika Migodi ya Madini, tunaifanyia kazi katika vipindi vijavyo, Serikali itakuja na mawasilisho ya kazi tunayoifanya.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa na Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kuwashukuru tena kwa namna ya pekee wote mlioshiriki katika kujadili Bajeti na kuhitimisha *Finance Bill* mpaka dakika hii, tulipofikia. Naomba sasa tuelekee mbele tuishughulikie *Finance Bill* katika kuidhinisha, ili kazi sasa ya utekelezaji wa Bajeti ianze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)
(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa kwa mara ya Pili)

SPIKA: Hoja hii imeungwa Mkono, nawaomba wale mnaozungumza na Waziri Mkuu nilishasema wakati wa

maamuzi hatuongei na Waziri Mkuu, kwa sababu mtaleta *embarrassment* humu ndani.

Leo Waziri Mkuu, baadaye itabidi afunge hoja yake, kusudi tupate muda wa kuweza kupitia tena, vizuri hii hoja tunayotaka Mheshimiwa Rais asaini kesho. Kwa sababu, lengo letu ni tarehe 1 Julai, 2013.

Kwa hiyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, Waziri Mkuu *is very polite*, hivi sasa anapitia hotuba yake, watu wanakaa wanaongea naye. Katibu tuendelee!

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2013
(*The Finance Bill, 2013*)

Ibara ya 1
Ibara ya 2
Ibara ya 3
Ibara ya 4

(Ibara zilizotajwa hapo juu zimepitishwa na Kamati ya Bunge bila mabadiliko Yoyote.)

Ibara ya 5
Ibara ya 6

MWENYEKITI: Hizi ibara kwa sababu ya mabadiliko zimekuwa *re-numbered.*

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri twende sawa sawa, ibara ya kwanza, pili, tatu, nne, tano na ibara ya sita hazikuwa *re-numbered*. Ziko kama zilivyo kwenye Muswaada.

(Ibara zilizotajwa hapo juu zimepitishwa na Kamati ya Bunge bila mabadiliko Yoyote.)

Ibara ya 7

(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Kamati ya Bunge bila mabadiliko Yoyote.)

Ibara ya 8

Ibara ya 9

(Ibara zilizotajwa hapo Juu zimepitishwa na Kamatiya Bunge zima pamoja na Mabadiliko yake)

Ibara ya 10

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mimi nilikuwa naomba ufafanuzi kwenye Ibara ya kumi, *item number 84.3.40.90* ukurasa wa 20, unaozungumzia *recorded DVD, VCD* pamoja na *CD*. Kwamba, kanuni *TRA* tayari wameshaziandaa kwa ajili ya *stickers* na zilipelekwa Hazina zikarudishwa kwa Mwanasheria Mkuu, lakini zikarudishwa tena Hazina. Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Waziri atufafanulie kwa sababu hajasaini zile Kanuni, zitatumia Kanuni zipi katika ukusanyaji. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Martha Mlata, sisi hatujaelewa tuko ukurasa wa sita (6).

MHE. MARTHA M. MLATA: Ni ukurasa wa sita lakini Ibara hiyo inaenda mpaka kwenye ukurasa wa 20, ambako kuna item number 84.3.40.90.

MWENYEKITI: Nimemwelewa, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sawa. Ile *HS Code* anayozungumzia Mheshimiwa Mbunge, inahusu *recorded video and audio tapes*, pamoja na *optical media*. Kinachofanywa hapa, ni kwamba, kodi yake ilikuwa shilingi 40 *per unit*, na sasa inakuwa 44 *per unit*, kwa zote mbili. Sasa hizo Kanuni nafikiri ni kitu kingine.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni hizo ndiyo zimeletwa tutazisaini.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. kwenye hiyo Ibara ya kumi kuna *HS Code* 27101922 ambayo inahusu mafuta ya taa.

MWENYEKITI: Ukurasa gani?

MHE. JOHN M. CHEYO: Ni *schedule of amendment*. Nataka kutumia nafasi hii kumwuliza Mheshimiwa Waziri, amekubali kwamba ataangalia mapendekezo ya Kamati kuhusu pesa ambayo tunaweza kupata kwa *deep sea fishing*, pia amezungumza juu ya mashudu.

Hata hivyo nashangaa, kwa nini Waziri anapata kigugumizi kuangalia gharama kati ya *CIF* na *landed cost* ya mafuta, kwa sababu tumemwonyesha kuna tozo ambazo siyo za lazima, mtu anaangalia tu kupima shilingi bilioni moja, kufanya *inspection* shilingi bilioni kumi na mbili na kuna wengine hata hawapo.

Nimeeleza haya mambo na yote yamekuja karibu takribani shilingi bilioni 36 ambazo anaweza akapata na ikiwezekana akaleta *supplementary estimate* mwezi *August*, tukapata pesa za kuweza kuweka katika sehemu mbalimbali zamaendeleo. Sasa nataka kujua ni kwa nini anakigugumizi kwa juu ya hilo sehemu.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, hoja anayoisema Mheshimiwa Cheyo ni hoja nzuri lakini Serikali haina kigugumizi. Jambo hili la tozo kwa *TCRA*, *EWURA* hizo tozo na msululu wa tozo mbalimbali ni lazima sasa tukae nao na *Authorities* nyingine ku-*iron out* yale ambayo tunaweza tukaya *prone* kwa maana hiyo, Serikali inafanyia kazi.

(Ibara zilizotajwa hapo Juu zimepitishwa

na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)

Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13

(Ibara zilizotajwa hapo juu zimepitishwa na Kamati ya Bunge bila mabadiliko Yoyote.)

Ibara ya 14

(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Kamati ya Bunge pamoja na mabadiliko yake.)

Ibara ya 15

(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Kamati ya Bunge bila mabadiliko Yoyote.)

Ibara ya 16

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nina ushauri na nitaomba Mwanasheria anielekeze. Ibara ya 16 pale kuna tafsiri ya maneno mbalimbali. Sasa huku mwanzo katika *amendment* ya *Executive Agencies Act,* kuna neno tumetumia *agency,* kwamba agency zote za Serikali zitakatwa asilimia 10.

Kwa maoni yangu, neno *agency* linapaswa kutafsiriwa kwenye *Executives Agencies Act,* lakini pia kwenye *Incomes Taxes* Act kwa maana , moja wapo ya mapato. Hizo agency zinatofautiana, kuna agency, kuna wakala, kuna mashirika, sasa litafisiriwe kwa kadiri tulivyomaanisha kwenye *Executives Agencies Act*, lakini nilizani ipo haja ika *future* hata kwenye *Income Tax*, maana yake ni moja ya *income*.

MWANSHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa

Mwenyekiti, kama mheshimiwa alikuwa anamapendekezo ya marekebisho angeleta kwa maandishi, huu ni utaratibu. Hakuna haja yaku-*define agency* kwa sababu, kwa sababu kwa mujibu wa Sheria ile *Executive Agencies Act*, imekuwa *defined* kule, na hakuna haja ya kui-*define for purposes of taxation* kwa sababu pia imekuwa *defined* kwenye ile *part*. Ni neno ambalo linaeleweka, *agency* ndiyo huyo huyo wakala.

Ibara ya 17
Ibara ya 18

(Ibara zilizotajwa hapo juu zimepitishwa na Kamati ya Bunge bila mabadiliko Yoyote)

Ibara ya 19

(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Kamati ya Bunge pamoja na mabadiliko yake.)

Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22

(Ibara zilizotajwa hapo juu zimepitishwa na Kamati ya Bunge bila mabadiliko Yoyote.)

Ibara ya 23

(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Kamati ya Bunge pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 24

(Ibara zilizotajwa hapo juu zimepitishwa

na Kamati ya Bunge bila mabadiliko Yoyote)

Ibara ya 25

(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Kamati ya Bunge pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35

(Ibara zilizotajwa hapo juu zimepitishwa na Kamati ya Bunge bila mabadiliko Yoyote)

Ibara ya 36

(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Kamati ya Bunge pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 37

(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Kamati ya Bunge bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 38

(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Kamati ya Bunge pamoja na mabadiliko yake.)

Ibara ya 39
Ibara ya 40

(Ibara zilizotajwa hapo juu zimepitishwa na Kamati ya Bunge bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 41

(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Kamati ya Bunge pamoja na mabadiliko yake.)

Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47
Ibara ya 48
Ibara ya 49
Ibara ya 50
Ibara ya 51
Ibara ya 52
Ibara ya 53
Ibara ya 54
Ibara ya 55
Ibara ya 56
Ibara ya 57
Ibara ya 58
Ibara ya 59
Ibara ya 60
Ibara ya 61

(Ibara zilizotajwa hapo juu zimepitishwa na Kamati ya Bunge bilaya

mabadiliko yoyote)

Ibara ya 62

(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Kamati ya Bunge pamoja na mabadiliko yake.)

Ibara ya 63

(Ibara iliyotajwa hapo juu imepitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake.)

(Bunge lilirudia)

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2013 (The Finance Bill, 2013)

(Kusomwa Kwa Mara ya Tatu)

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima, imepitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2013 yaani (*The Finance Act, 2013).* Kifungu kwa Kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Taarifa hiyo sasa ukubaliwe Rasmi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Simameni muunge mkono. Ahsante. Ilivyotakiwa sasa ilitakiwa Katibu wangu asome *long title*.

Waheshimiwa Wabunge kwa nafasi hii napenda nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kabisa, kumpongeza Waziri wa Fedha, Wasaidizi wake, Manaibu Waziri hawa na

Wataalam wote walioshughulika kwa bidii sana kuweza kufikia *document* tuliyo nayo sasa.

Lakini pia kwa utaratibu tuliokubaliana, huu wa ushirikishwaji, napenda nichukue nafasi, na nadhani Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana na mimi. Kamati ya Bajeti, imefanya kazi kubwa sana. Mfikirie yale majedwali yaliyoletwa hiyo jana, yale Majedwali Karibu nane na wengine hawakusogea, tungeingia humo ndani tungeliona na kwanza isingewezekana? *(Makofi)*

Kama nilivyosema Maswali ya Mjadala wa Fedha ama *amendments* za fedha, sio tu kwamba wewe ungependa hivi haikuwa, na mwingine aseme apende vingine haijakuwa sio hivyo. Ninawashukuru sana wote waliokwenda kule wamekubali maana yake hawakufanya kama jambo la kisiasa.

Tunapoingia katika ngazi ya *Finance Bill,* sio suala la kisiasa. Ni suala la Bajeti hii inakaa vipi. Mimi ninasema ninawashukuruni sana kwa sababu mmefanya na nina hakika na nyinyi wenyewe mmesoma sana huko ndani. Wengi mmepata elimu. Hata ingelikuwa ile Sera ya Waziri wa Elimu ya kutoa *Honorary Ph.D.* kwa watu waliosoma kwa vitendo basi mimi nadhani Kamati yangu ingeshapata hiyo tuzo. (*Makofi)*

Sio siri tulivyoanzisha utaratibu huu, wa kufanya mabadiliko kwanza ya mzunguko wa Bajeti. Hakuna mmoja kati yetu alikuwa na utaalam wowote. Ila tu ni ile fikra kwamba mazoea yale yalikuwa hayana tija. Maana baada ya Waziri wa Fedha tarehe 13, 2013.

Sasa hivi tungelikuwa tunaendelea kupwaga maneno tu. Tunasema hakuna cha kubadili kwa sababu mmeishapiga kura. Lakini utaratibu wetu umetoa fursa ya watu kufanya mabadiliko makubwa sana.

Bajeti hii sio ile iliyokuwa imependekezwa na Waziri,

hata tulipokuwa kule Dar es Salaam kwenye ukumbi wa Mwalimu Nyerere, haikuwa yenyewe. *(Makofi)*

Imekuja kubadilika, sio kwa kiwango tu, na hata katika ubora wake. Lakini jambo kwa kawaida Waheshimiwa Wabunge, jambo jipya lolote huwa haliwezi kukubaliana tu. Kila mtu anapata wasi wasi wa aina yake. Kweli Serikali ilipata wasi wasi sana na *in fact* hawakufikiria kama tunaweza kumaliza. Kwa hiyo, ndugu zangu ningependa kusema haya kabla sijawahoji. Sasa nina wahoji.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2013 Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)

SPIKA: Ninaona wote kwa sababu mmefanya kazi nzuri wameafikiana na ninaomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa ukomavu wenu wote. Ninarudia kusema kwamba Hongera kwa Waheshimiwa wanaostahili. *(Makofi)*

KUAHIRISHA BUNGE

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kama nilivyosema tumeona tuahirishe kipindi hiki cha mchana, kusudi Ofisi yangu iweze kuendelea kufanya haya mabadiliko vizuri na Mheshimiwa Rais, aweze ku-*sign* kabla ya tarehe 30 Juni, 2013 kusudi itakapoanza tarehe 1 Julai, 2013 basi kazi ianze.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, tarehe 9 Aprili, 2013 tulianza Kikao cha Kwanza cha Mkutano wa 11 wa Bunge lako Tukufu. Ni jambo la kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa Rehema kwamba leo tunahitimisha shughuli zote zilizopangwa kwa amani na salama.

Mkutano huu ulikuwa mahsusi kwa ajili ya kuwasilisha, kujadili na hatimaye kupitisha Bajeti ya Serikali na Makadirio

ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara, Mikoa na Taasisi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupitisha Bajeti ya Serikali, katika Mkutano huu Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kufanya Uchaguzi wa Wajumbe kwenye Taasisi na Vyuo vya Elimu ya Juu. Napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini. kuwa Mjumbe wa Bunge hili katika Chuo Kikuu cha Dodoma,

Mheshimiwa Jitu Vrajilal Soni, Mbunge wa Babati Vijijini kuwa Mjumbe katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, kuwa Mjumbe wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia – Mbeya na Mheshimiwa Selemani Said Jafo, Mbunge wa Kisarawe kuwa Mjumbe wa Jukwaa la Kibunge la Nchi Wanachama Kusini mwa Afrika *(SADC – PF).*

Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni kwa kuchaguliwa kuwa Wawakilishi wetu katika Baraza la Chuo Kikuu cha Mzumbe. Matarajio yetu ni kwamba, wote waliochaguliwa watatuwakilisha vyema katika Taasisi hizo muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee, napenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Yussuf Salimu Hussein kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge Mpya wa Jimbo la Chambani kupitia Chama cha Wananchi – CUF. Ni dhahiri kwamba kuchaguliwa kwake ni kutokana na matumaini makubwa waliyonayo Wananchi wa Jimbo la Chambani na kwamba atawawakilisha vyema ndani na nje ya Bunge katika kusukuma shughuli za Maendeleo, Jimboni mwao. *(Makofi)*

Vilevile, nitumie nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Dalali Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga na Mheshimiwa Aeshi Hilaly, Mbunge wa Sumbawanga Mjini kwa kufanikiwa

kurejea tena Bungeni baada ya kushinda rufaa za kesi zao za uchaguzi katika Majimbo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Uongozi wake makini ambao umeendelea kuipatia sifa Tanzania katika ngazi za Kanda na Kimataifa.

Hali hiyo imejidhihirisha wazi kwa matukio ya Kimataifa ambayo yamefanyika hapa Nchini. Miongoni mwa matukio hayo ni Ziara ya Rais Xi Jinping wa China alipotembelea Tanzania tarehe 24 Machi, 2013, na kuhutubia Bara la Afrika akitumia Jukwaa la Tanzania. Hivi sasa pia tunajiandaa kumpokea Mheshimiwa Barack Obama, Rais wa Marekani atakayekuwepo hapa Nchini kuanzia tarehe 1 Julai, 2013.

Vilevile, Tanzania itakuwa Mwenyeji wa Mkutano wa Kimataifa wa Majadiliano ya Ushirikiano kwa Manufaa ya Wote wa Mwaka 2013 (*Global 2013 Smart Partnership Dialogue*) ambao utafanyika kuanzia tarehe 28 Juni, 2013. Matukio yote haya sio tu yametokea hivi kwa bahati tu, bali ni muonekano wa Tanzania Nchi za nje na jinsi ambavyo inaonekana kwa wenzetu tunaoshirikiana nao. Hili ni jambo la kujivunia.

Mheshimiwa Spika, sote tunakumbuka kuwa, wakati tukiendelea na Mkutano huu hapa Bungeni, matukio matatu makubwa ya kusikitisha yalitokea hapa Nchini. Moja ni tukio la Mlipuko wa Bomu katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Joseph Mfanyakazi la Olasiti, Arusha lililotokea tarehe 5 Mei, 2013. Pili ni tukio la vurugu za tarehe 22 Mei, 2013 zilizotokea Mkoani Mtwara baada ya baadhi ya Wananchi wa Mtwara kutopenda kujengwa kwa Bomba la Kusafirishia Gesi kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam.

Tatu ni tukio la mlipuko wa Bomu lililotokea tarehe 15 Juni, 2013 katika Mkutano wa Kampeni za Uchaguzi wa Madiwani katika Kata ya Soweto katika Jiji la Arusha. Wote tunakumbuka kwamba katika matukio yote haya matatu,

Watu wapatao 10 walipoteza maisha na wengine wapatao 155 kupata majeraha na mali za raia kuharibiwa au kupotea kabisa. Kwa masikitiko natoa pole wale wote waliopotelewa na ndugu, jamaa na Marafiki katika matukio hayo. Aidha, nawapa pole majeruhi wote pamoja na wananchi wote waliopoteza mali ikiwemo kuchomewa nyumba na hivyo kuathirika kiuchumi na kisaikolojia.

Mheshimiwa Spika, uzoefu tunaoupata katika matukio yote haya ni kwamba hakuna raia mwema anayeipenda Nchi yake anayetamani matukio haya yatokee ndani ya Nchi yake. Wananchi wengi wamesikitishwa sana na matukio hayo ambayo yamepoteza maisha na mali za ndugu zetu. Tunamwomba Mwenyezi Mungu atuepushe na hila zozote zenye nia mbaya ya kufanya matukio kama hayo kutokea tena kwenye Nchi yetu. Wito wangu kwa Watanzania wote ni kuwaomba tuwe wamoja katika kukemea na kulaani matukio hayo. Ni muhimu tuendelee kuishi kwa upendo, amani na mshikamano, kwa maana huo ndio utamaduni wa Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, wakati wa Mkutano huu, wapo Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki, ikijumuisha wapendwa wao, wazazi na watoto. Wote kwa ujumla wao nawapa pole kwa yote yaliyowafika.

Mheshimiwa Spika, tangu tulipoanza Mkutano huu tarehe 9 Aprili, 2013 hadi leo, jumla ya Maswali 490 ya Msingi pamoja na 1,262 ya Nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Serikali. Vilevile, Maswali 31 ya Msingi na 27 ya Nyongeza yalijibiwa kwa utaratibu wa Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioiuliza Maswali ya Msingi na ya Nyongeza. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri waliojibu Maswali hayo na kutoa ufafanuzi kwa ufasaha mkubwa katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, pia Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kujadili, kurekebisha na kupitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho

ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2013, [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2013*].

Kupitishwa kwa Muswada huo kutatusaidia kama Taifa kuboresha matumizi ya Sheria husika ikiwemo Sheria ya Uchaguzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria na Sheria ya Utumishi wa Umma. Aidha, Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2013 (*The Finance Bill, 2013)* na Muswada wa Sheria wa Kuidhinisha Matumizi ya Fedha za Serikali wa Mwaka 2013 *(Appropriation Bill)* yote ilisomwa kwa mara ya Kwanza na kupitia ngazi zake zote na hivyo kuidhinisha Matumizi ya Serikali ya Mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Miswada ifuatayo ilisomwa kwa mara ya Kwanza:-

(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, 2013 [*The Constitutional Review (Amendments) Act, 2013*];

(ii) Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni wa Mwaka 2013 [*The Referendum Act, 2013*];

(iii) Muswada wa Sheria ya Mfuko wa Akiba kwa Wafanyakazi wa Mwaka, 2013 [*GEPF Retirement Benefits Fund Act, 2013*];

(iv) Muswada wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji, 2013 [*The National Irrigation Act, 2013*]; na

(v) Muswada wa Sheria ya Takwimu wa Mwaka, 2013 [*The Statistics Act, 2013*].

Mheshimiwa Spika, napenda kwa dhati kabisa kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa kutumia muda wote wa Mkutano huu kwa ufanisi mkubwa. Wote mtakumbuka tulianza Mkutano huu kwa changamoto kubwa ya Mabadiliko ya Mzunguko mpya wa kuwasilisha Bajeti ya Serikali (*New Budget Cycle*) na pengine kuwepo hoja na mashaka kuhusu ufanisi wake.

Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tumefanya vizuri sana!! Wote ni mashahidi kwamba Waheshimiwa Wabunge wameweza kujadili kwa kina na kutoa ushauri wao ambao kwa kiasi kikubwa umezingatiwa na Serikali. Tunajivuna kwa kupitisha Bajeti ya Serikali kwa kutumia utaratibu mpya na kwa kuzingatia Kanuni na Taratibu za Bunge lako Tukufu.

Nitumie fursa hii ya kipekee kukupongeza wewe binafsi kwa kubuni na kuridhia utekelezaji wa utaratibu huu. Aidha, nirudie kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri mliyoifanya kwa ajili ya maendeleo ya Taifa hili.

Lakini kipekee kabisa nimpongeze Waziri wa Fedha na Wataalam wake kwa kazi nzuri ambayo imeiwezesha Serikali sikivu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi (CCM) kukamilisha Bajeti hii baada ya kuzingatia ushauri na maoni ya Waheshimiwa Wabunge. Ni kweli kwamba haikuwa kazi nyepesi, lakini wote ni mashahidi kwamba kwa mara ya kwanza tumepata Bajeti nzuri ya Serikali na ya aina yake. Changamoto iliyoko mbele yetu ni kujipanga vizuri kusimamia utekelezaji wake kwa kukusanya Mapato yatakayotosheleza mahitaji yaliyoorodheshwa kwenye Bajeti hiyo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu mpya wa mzunguko wa Bajeti *(New Budget Cycle).* Tumefanikiwa kukamilisha mchakato wa kuandaa, kuchambua, kujadili na hatimaye kuidhinisha Bajeti za Mafungu ya Wizara zote, zikiwemo Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala mbalimbali za Serikali, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka 2013/ 2014.

Hatua hii itatuwezesha kuanza utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ifikapo tarehe 1 Julai, 2013. Wakati wa mchakato huu tumejifunza mambo mengi lakini pia tumeona zipo changamoto mbalimbali ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi. Aidha, tumepata maoni na ushauri mbalimbali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na Wadau mbalimbali kuhusu namna ya kuboresha Bajeti zijazo ili ziwe bora zaidi na zenye maslahi makubwa kwa Wananchi wetu na Taifa

kwa ujumla. Tutazingatia maoni na ushauri huo tuliopata kutoka kwa Wadau wote.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mafanikio ya utaratibu huu mpya ni pamoja na; Kwanza: Kuwezesha Serikali kuanza kutekeleza Mpango na Bajeti mapema kuanzia tarehe 1 Julai, 2013; na

Pili kutoa fursa kwa Serikali kufanya majadiliano mapana na ya kina na Waheshimiwa Wabunge na kuwezesha kuzingatia maeneo muhimu yanayopaswa kuingizwa kwenye Mpango na Bajeti katika mwaka mpya wa fedha kabla Bajeti mwaka haijapitishwa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mafanikio hayo, kwa utaratibu huu mpya tumeweza kutenga fedha zaidi katika Sekta za Maji, Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Umeme Vijijini na kutunisha Mifuko ya Mendeleo ya Wanawake na Vijana. Ni faraja kwamba Serikali imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kufanya maboresho zaidi katika Kodi na Tozo mbalimbali ili kupata fedha za kugharamia mahitaji hayo yaliyojitokeza.

Serikali inaipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Kamati zote za Bunge za Kisekta na Wadau wengine kwa mchango wao wa mawazo wa namna ya kuongeza Mapato ya Serikali ili kukidhi mahitaji hayo ya fedha yaliyojitokeza wakati wa majadiliano ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya 2013/2014. Katika mwaka ujao wa fedha wa 2013/2014, Serikali imejizatiti kutekeleza kwa dhati Mpango wa Maendeleo na Bajeti ya Serikali tuliyoipitisha katika Mkutano huu.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) Mheshimiwa Stephen Wasira (Mb.) pamoja na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa (Mb.) katika hotuba zao na kwenye majumuisho wameeleza kwa

kina na kutoa ufafanuzi wa hatua zitakazochukuliwa na Serikali katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo mazuri ya Waheshimiwa Mawaziri, napenda kutumia fursa hii kutoa msisitizo katika maeneo mawili muhimu. Eneo la Kwanza ni kuhusu utekelezaji wa Vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo na utaratibu mpya wa kusimamia na kufuatilia Miradi ya Maendeleo chini ya *President's Delivery Bureau.* Eneo la Pili ni Kuimarisha Usimamizi wa Ukusanyaji Mapato na Matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo na utaratibu mpya wa kusimamia na kufuatilia Miradi ya Maendeleo chini ya *President's Delivery Bureau.* Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2013/2014 umetayarishwa kwa mantiki kwamba ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa mwaka 2011/2012 - 2015/2016. Hivyo, malengo yake yamezingatia utekelezaji wa vipaumbele vya msingi vya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, ambavyo ni:-

(i) Kuongeza uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme;

(ii) Kuimarisha shughuli za Usafirishaji na Uchukuzi hususan katika Ukanda wa Kati. Hii inajumuisha kupanua Bandari ya Dar es Salaam na kuboresha usafiri wa barabara na Reli ya Kati;

(iii) Kuongeza uzalishaji na tija katika Sekta ya Kilimo, hususan, katika uzalishaji wa mazao makuu ya chakula ili kutosheleza mahitaji ya ndani na kupata ziada kwa ajili ya kuuza nje ya Nchi;

(iv) Kuchochea uwekezaji katika Sekta ya Viwanda, hususan, vile vinavyotumia au kuongeza thamani ya mazao ghafi yanayopatikana hapa Nchini;

(v) Kuendeleza Rasilimali Watu na Ujuzi ikiwa ni

pamoja na kuimarisha ufundishaji wa Masomo ya Sayansi, Ufundi Stadi na Teknolojia;

(vi) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za jamii; na

(vii) Kuboresha huduma za utalii, biashara na fedha.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa Mipango yetu ya Maendeleo, imeonekana kuna umuhimu wa kuimarisha mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini. Katika kuhakikisha kwamba azma hii inatekelezwa, Serikali imefikia uamuzi wa kuanzisha Mfumo mpya wa ufuatiliaji na tathmini unaojulikana kama "Matokeo Makubwa Sasa" (*Big Results Now*) ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016).

Msingi wa Mfumo huu ni uwazi katika kupanga shughuli za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayokusudiwa. Kwa ujumla, Miradi ya Maendeleo na utekelezaji wake inatakiwa isiwe siri kwa Wananchi au jamii inayolengwa. Hivyo, pamoja na kuainisha shughuli zitakazotekelezwa, Mfumo huu unabainisha muda, mhusika, rasilimali zinazohitajika, vigezo vya kupimia mafanikio ya utekelezaji na ni shirikishi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Mfumo huu umeanzishwa ili kumwezesha Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla, kusimamia ipasavyo utekelezaji wa programu na miradi ya kipaumbele ili kuharakisha maendeleo. Hivyo, kazi za utendaji na uratibu zitakuwa chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu, na kusimamiwa na chombo kitakachojulikana kama *President's Delivery Bureau (PDB).* Majukumu ya chombo hicho ni:-

Kuchambua kwa utaratibu wa Kimaabara wa Miradi ya kipaumbele iliyobainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na kuainisha shughuli zinazopaswa kutekelezwa, muda wa kuanza na kukamilika kwake,

malengo yanayotarajiwa na kiasi cha fedha kinachohitajika kwa utekelezaji;

Kutayarisha na kusimamia mikataba ya uwajibikaji wa Mawaziri;

Kutoa ushauri na kusaidia kutatua vikwazo vya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; na

Kufanya tathmini ya utekelezaji na kuishauri Serikali juu ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa na kuwezesha Wizara husika kufikia malengo yaliyowekwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kubainisha kuwa "Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa" si Mpango, bali ni Mfumo. Mfumo huu utawezesha kusimamia vizuri zaidi utekelezaji wa miradi ya maendeleo na majukumu ya Serikali yaliyobainishwa kuwa ni ya kipaumbele katika kufikia malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Mfumo huu, pamoja na mambo mengine, unakusudiwa pia kuimarisha Mfumo wa Upimaji wa Wazi wa Utendaji Kazi Serikalini unaojulikana kama *Open Performance Review and Appraisal System (OPRAS)*, ambao kwa sasa umekuwa hautekelezwi kama ilivyokusudiwa.

Kwa kutumia mfumo huu mpya, sasa Waheshimiwa Mawaziri watakuwa wanawekeana Mikataba ya Utendaji (*Performance Contracts*) na Watendaji walio chini yao. Kwa kuanzia, "*President's Delivery Bureau*" itasimamia utekelezaji wa Awamu ya Kwanza katika maeneo sita (6) yaliyofanyiwa uchambuzi wa kina wa Kimaabara (*Labs*) ambao umekamilika hivi karibuni. Maeneo hayo ni Nishati ya Umeme; Uchukuzi na Usafirishaji; Kilimo; Elimu; Maji; na Ukusanyaji Mapato.

Mheshimiwa Spika, Kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa Mapato na Matumizi ya Serikali. Pamoja na kuanzishwa kwa utaratibu huu Mpya wa kufuatilia Miradi, kipengele muhimu kilichozungumziwa katika Mkutano huu ni

kuhusu kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa Mapato na Matumizi ya Serikali.

Michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge iliyotolewa imesisitiza kwamba Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2013/2014 iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu inahitaji usimamizi makini na mahiri ili kufikia malengo tuliyojiwekea. Kwa mantiki hiyo, Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa Mapato na kuhakikisha kwamba kuna uwajibikaji mkubwa wa matumizi ya Serikali. Miongoni mwa hatua zitakazochukuliwa na Serikali katika mwaka 2013/2014 ili kufikia azma hiyo ni pamoja na zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika Kwanza, kuimarisha uwezo wa Serikali wa kukusanya Mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa misaada kutoka nje na kutegemea zaidi kodi za biashara za Kimataifa na Kikanda. Hatua hizo zitaambatana na kusimamia ipasavyo ukusanyanyaji wa mapato yatokanayo na rasilimali muhimu za Taifa kama vile Madini, Gesi Asilia, Wanyamapori, Misitu, Uvuvi, Ardhi, Vivutio vya Utalii pamoja na kutumia vizuri fursa za kijiografia zinazotokana na Nchi yetu kupakana na Nchi Nane jirani zisizokuwa na bandari.

Pili, sambamba na hatua hiyo, Serikali itayafanyia kazi mapendekezo ya Kamati yako Maalum uliyoiunda inayoongozwa na Mheshimiwa Andrew Chenge, Mbunge wa Bariadi Magharibi, ambayo umeipa jukumu la kuangalia vyanzo vipya vya Mapato ya Serikali. Aidha, Serikali itakamilisha utafiti wake unaoendelea wa kubaini vyanzo vipya na endelevu vya kupata mapato mengi ya ndani. Vilevile, itakamilisha utafiti wa uchambuzi wa misamaha ya kodi ili kuleta mapendekezo mahsusi ya kupunguza misamaha isiyo na tija;

Tatu, Serikali itaimarisha usimamizi na udhibiti wa mifumo yake ya ndani hasa katika eneo la Manunuzi ya Umma. Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara za Serikali zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Umma, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zote Nchini wanakumbushwa tena kuzingatia ipasavyo Sheria, Kanuni, Taratibu na

Miongozo ya kifedha na kiuhasibu iliyopo kuhusiana na Matumizi ya Fedha za Umma.

Hii ni pamoja na kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima kama vile kugharamia Semina na Makongamano, Ununuzi wa fulana na Kofia za Sherehe mbalimbali, ununuzi wa magari ya kifahari, posho mbalimbali, mafuta na matengenezo ya magari ya Serikali kwa gharama kubwa zisizoendana na ubora uliopatikana. Hatua za Kinidhamu zitachukuliwa kwa watakaokiuka maelekezo yaliyotolewa.

Nne, ili kuongeza uwazi na uwajibikaji wa Serikali kwa Bunge na Wananchi, Serikali imeandaa mfumo imara na endelevu wa kuhakikisha kuwa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Taarifa za Kamati za Kudumu za Bunge zinazosimamia Fedha za Umma yaani *Public Accounts Committee - PAC na Local Authorities Accounts Committee-LAAC* zinapewa umuhimu wa hali ya juu na kushughulikiwa kikamilifu.

Tayari, Katibu Mkuu Kiongozi ameunda Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu yenye wajibu wa kuhakikisha kuwa Taarifa hizo zote zinachambuliwa vizuri na majibu sahihi yanatolewa kwa wakati.

Kamati hii inasaidiwa na Kamati Ndogo ya Wataalam ambayo pamoja na mambo mengine inafanya uchambuzi wa awali, na pia kupendekeza kwa Kamati ya Makatibu Wakuu namna bora ya kupunguza uzalishaji wa hoja mpya za ukaguzi.

Tano, ili kuimarisha usimamizi wa rasilimali za Umma pamoja na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi Serikalini, Serikali itaendelea kuhimiza uzingatiaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma pamoja na kuteua na kupanga safu ya Viongozi na Watendaji hodari, makini na wenye sifa stahiki za kitaaluma katika Wizara, Taasisi na Idara za Serikali, Mikoa pamoja na Halmashauri. Watumishi wasio na sifa pamoja na wale wababaishaji hawatavumiliwa hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, Mara kwa mara nimekuwa

nikilitaarifu Bunge lako Tukufu kuhusu hali ya Lishe Nchini na athari zake kwa Wananchi hasa kwa Watoto chini ya miaka mitano na uchumi kwa ujumla. Nimeeleza pia juhudi za Serikali katika kukabiliana na hali ya Lishe Duni. Nichukue nafasi hii kulitaarifu Bunge kuwa Serikali ya Awamu ya Nne imeendelea na juhudi zake za kuboresha lishe na kipekee Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete amekuwa mstari wa mbele katika kuongoza juhudi hizo.

Mheshimiwa Spika, Kutokana na juhudi hizo, Tarehe 15 Mei 2013, Mheshimiwa Rais alizindua Mpango wa Kuongeza Virutubisho kwenye Vyakula kwa kuanzia na mafuta ya kupikia na unga wa ngano. Mpango huo utachangia kwa kiasi kikubwa sana kupunguza utapiamlo kwa Watoto walio chini ya miaka mitano.

Aidha, tarehe 16 Mei 2013 Mheshimiwa Rais alizindua Kampeni ya Kitaifa ya Kuongeza Uwajibikaji Katika Lishe Nchini. Uzinduzi huo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali, Sekta Binafsi, Washirika wa Maendeleo pamoja na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Viongozi hao walipata nafasi ya kutoa na kuthibitisha ahadi zao za kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuboresha Lishe Nchini.

Mheshimiwa Spika, kampeni kama hizo zitaendelea kufanyika katika ngazi za Mikoa, Wilaya hadi Vijijini ili Elimu ya Lishe Bora ienezwe kwa kasi katika ngazi zote. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuwa mstari wa mbele katika kuongoza mapambano dhidi ya utapiamlo Nchini.

Aidha, nitumie fursa hii kuwaagiza Wakuu wa Mikoa kuhakikisha wanaendeleza Kampeni za Elimu ya Lishe katika Mikoa yao na kusimamia kwa karibu kuhakikisha kwamba kampeni hizo zinaendelezwa hadi kwenye ngazi za Wilaya na Vijiji.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nitumie fursa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, tarehe 8 Juni, 2013 nilihudhuria

Mkutano Maalum ulioandaliwa na Nchi Tajiri na zenye Viwanda vingi Dunani (*G8*) kuhusu Lishe Bora na Ukuaji wa Uchumi uliofanyika Jijini London-Uingereza na kuhudhuriwa na Viongozi kutoka Mataifa mbalimbali. Katika Mkutano huo, nilipata nafasi ya kuelezea hatua ambazo Serikali imechukua katika kupambana na utapiamlo hapa Nchini. Aidha, nilieleza bayana malengo tuliyoyaweka ya kupunguza utapiamlo kwa Watoto na akina Mama kama ilivyobainishwa katika Mkakati wa Lishe wa Kitaifa 2011/2012 - 2015/2016.

Malengo hayo tuliojiwekea ni pamoja na kupunguza udumavu kwa Watoto chini ya miaka 5 kutoka Asilimia 42 hadi Asilimia 27, kupunguza ukosefu wa madini joto kwa Wanawake wajawazito kutoka Asilimia 48.5 hadi Asilimia 35 na kuongeza unyonyeshaji pekee wa maziwa ya mama kwa Watoto wadogo bila kuwapa chakula chochote ndani ya miezi sita kutoka Asilimia 50 hadi Asilimia 60.

Mheshimiwa Spika, imani yangu ni kwamba, malengo tuliyojiwekea yatafikiwa iwapo sote tutashirikiana kwa karibu katika utoaji wa Elimu ya Lishe kwa Wananchi wetu katika ngazi zote. Kwa maana hiyo, ninawasihi Waheshimiwa Wabunge kuendelea kushirikiana na Serikali kutoa elimu hiyo katika maeneo yenu ili kutokomeza janga hili la utapiamlo Nchini. Nitumie nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu kuwashukuru kwa dhati Wadau wote wa Maendeleo kwa kuendelea kushirikiana na Serikali katika jitihada za kupambana na utapiamlo Nchini.

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo, hali ya chakula, tathmini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa 2012/2013 na upatikanaji wa chakula katika mwaka 2013/2014 inaonesha kuwa uzalishaji katika mikoa 19 kati ya 25 utakuwa wa kuridhisha na kuna dalili za kuwepo kwa chakula cha ziada katika Mikoa hiyo. Hivi sasa bei za Wastani za chakula hasa mchele na mahindi katika masoko mengi Nchini zimeshuka kufuatia uvunaji wa mazao hayo katika maeneo yanayopata mvua za msimu. Kwa mfano, bei ya mahindi imeshuka kutoka bei ya Wastani ya Taifa ya Shilingi 774 mwezi Februari 2013 hadi kufikia Shilingi 545 katika

mwezi Mei 2013 na mchele kutoka Shilingi 1,825 hadi 1,413 katika kipindi hicho.

Matarajio ni kwamba bei hizo zitashuka kadiri chakula kitakavyoingizwa Sokoni. Ili kujihakikishia kuwa Nchi inakuwa na chakula cha kutosha, Wakala wa Taifa wa Uhifadhi wa Chakula (*NFRA*) itaanza ununuzi wa Tani 235,000 za mahindi na Tani 15,000 za mtama Mwezi Julai 2013.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kupitia NFRA itaendelea na usambazaji wa chakula cha msaada kiasi cha Tani 69,451 kilichoidhinishwa na kutengwa kwa ajili ya kusambazwa kwa watu wenye upungufu wa chakula katika Mikoa na Halmashauri zenye upungufu. Nitumie fursa hii kuwaagiza tena Wakuu wa Mikoa na Wilaya kuwahimiza Wakulima kuhifadhi Chakula cha kutosha kwa mahitaji ya Kaya zao badala ya kuuza Chakula chote na kusubiri Serikali kuwapelekea Chakula. Aidha, Halmashauri za Wilaya muda wote ziweke Mikakati madhubuti ya kuzuia ununuzi holela wa Chakula kutoka mashambani mwa Wakulima.

Mheshimiwa Spika, Uamuzi wa Serikali kuhusu Muundo utakaotumika kutoa Pembejeo za Ruzuku. Katika mwaka 2012/2013, Serikali iliendelea kutoa ruzuku za Pembejeo za Kilimo kwa nia ya kumpunguzia Mkulima gharama za uzalishaji. Ruzuku ya pembejeo imekuwa ikitolewa kwa kutumia Vocha ambapo Mawakala walichaguliwa na Makampuni ya pembejeo.

Hata hivyo, utaratibu huo uligubikwa na changamoto nyingi zikiwemo za Vocha kuchelewa kuwafikia Wakulima kutokana na kutowajibika kikamilifu na baadhi Watendaji wasio waaminifu kuwarubuni Wakulima, na baadhi ya Makampuni kutofikisha pembejeo kwa wakati. Changamoto hii zimelalamikiwa na Wabunge wengi wakati wanachangia hotuba ya Wizara ya Kilimo na Chakula na Ushirika.

Ili kuondokana na changamoto hizo, Serikali imeamua kutumia Mifumo miwili katika utoaji wa ruzuku ya pembejeo za kilimo katika msimu wa kilimo wa 2013/2014. Mifumo hiyo

itahusisha kuendelea na utaratibu wa Vocha na kuanzisha Mfumo wa mikopo kwa uwiano wa Asilimia 80 Vocha na Asilimia 20 mikopo. Aidha, Serikali imeidhinisha Bajeti ya Shilingi Bilioni 112.46 zikiwemo Shilingi Bilioni 19.972 za ufadhili wa Benki ya Dunia na Shilingi Bilioni 92.49 za Serikali kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2013/2014 Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu upatikanaji wa Tani 400,000 za mbolea, Tani 40,000 za mbegu bora, Miche Milioni 40 ya Chai na Kahawa, Tani 2,000 na lita 870,000 za madawa ya pamba na korosho kupitia ruzuku ya pembejeo. Napenda kuwakumbusha Wakuu wa Mikoa na Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri, kusimamia kwa karibu upatikanaji na usambazaji wa Mbegu na Mbolea ili kuwasaidia Wakulima kupata pembejeo hizo mapema. Aidha, nahimiza Sekta Binafsi nayo kuendelea kuingiza Mbolea, Mbegu bora na Madawa mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza Kilimo Nchini.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Kuimarisha Mfumo Wa Stakabadhi za Mazao Ghalani Zao la Korosho. Katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge pia, walizungumzia kwa hisia tofauti Mfumo wa Stakabadhi wa mazao Ghalani. Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani Maghala umeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Stakabadhi Ghalani Na. 10 ya mwaka 2005 kwa lengo la kuwasaidia Wakulima wakiwa katika vikundi au ushirika kuwa na nguvu ya soko, kupata bei nzuri katika mazao ya biashara na kuingia katika soko la ushindani ambalo ingekuwa vigumu kutokana na kukosekana kwa mitaji. Pia, ulianzishwa ili kusaidia kuzuia upotevu wa mazao unaotokana na uhifadhi dhaifu, na pia kuongezea bidhaa thamani kabla ya kuziuza.

Mfumo huu ulianza vizuri ambapo Wakulima walipata malipo ya kwanza, ya pili na ya tatu (Majaliwa). Hata hivyo, kwa sasa Mfumo huo unakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazotokana na upotoshaji unaofanywa na walanguzi na madalali wanaojinufaisha na ununuzi wa mazao kutoka kwa wakulima kwa kutumia mfumo usio rasmi. Vilevile, wapo Watendaji wasio waaminifu wa Vyama vya

Ushirika, wasimamizi wa maghala na Taasisi za fedha wamechangia kudhoofisha mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, Upo ukweli kwamba, mafanikio mengi yamepatikana baada ya kuanzishwa kwa Mfumo huo. Kwa mfano, kumekuwepo na ongezeko la uzalishaji wa Zao la Korosho ikilinganishwa na miaka mitano kabla ya kuanzishwa kwa Mfumo huu kutoka Tani 71.918 katika msimu wa 2001/2002 hadi kufikia Tani 158,439 katika msimu wa 2011/2012.

Aidha, bei ya Korosho iliongezeka kutoka Shilingi 360 kwa kilo katika msimu wa 2003/2004 hadi kufikia Wastani wa Shilingi 1,500 katika msimu wa 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu pia umesaidia Wakulima kuuza mazao yao kwa kutumia Mizani zinazokaguliwa na Wataalamu na kupatiwa bei Dira kwa kilo, tofauti na vipimo visivyo rasmi vinavyotumika nje ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Wakulima katika maeneo yanayozalisha Korosho wanafahamu sana vipimo batili vinavyojulikana kama “Kangomba” ambapo licha ya kipimo hiki kutofautiana kutoka eneo moja hadi jingine; kwa kutumia “Kangomba” Wakulima wanalipwa bei Dira ya ujazo mkubwa kuliko ujazo wa Kilo moja ya kawaida au kulipwa kidogo kulingana na bei Dira iliyopo. Aidha, matumizi ya “Kangomba” yanamkosesha Mkulima malipo ya majaliwa na hata pembejeo za mkopo, maana kipimo hiki hakipo katika Mfumo wa kukopesha Wakulima Pembejeo.

Mheshimiwa Spika,Chini ya Mfumo huu, Mikopo kutoka Mabenki kupitia kwa Vyama vya Ushirika vya Msingi imeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 36.2 katika msimu wa 2007/2008 hadi kufikia Shilingi Bilioni 134.6 katika msimu wa 2011/2012. Kwa upande wa mapato, kumekuwepo na ongezeko la Mapato yatokanayo na Korosho Ghafi kutoka Tani 99,106 msimu wa 2007/2008 hadi Tani 158,439 msimu wa 2011/2012. Thamani ya mauzo imeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 43.1 msimu wa 2007/2008 hadi Shilingi Bilioni 236.1 msimu wa 2011/2012. Aidha, Mapato yatokanayo na ushuru kwa kuuza nje ya Nchi yameongezeka kwa kiasi kikubwa kutoka

Shilingi Bilioni 6.4 msimu wa 2007/2008 hadi kufikia Shilingi Bilioni 35.4 katika msimu wa 2011/2012. Vilevile, Mfumo huu umewezesha upatikanaji wa takwimu sahihi za kiasi cha Korosho kilichozalishwa, kilichouzwa nje ya Nchi na kilichobanguliwa hapa Nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mifano hiyo michache ya mafanikio, napenda kuchukua fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, Wakulima na Wananchi kwa ujumla kuwa, Serikali ina imani na Mfumo huu wa Stakabadhi za Mazao Ghalani, na hivyo hautaondolewa kwa sasa bali Serikali inajipanga vizuri kuondoa vikwazo vilivyofanya Mfumo huu kufanya vibaya. Tutaimarisha usimamizi ili kutoa matokeo yaliyolengwa. Aidha, uamuzi huu wa Serikali unatokana na ukweli kuwa Mfumo huu upo kwa mujibu wa Sheria ya Stakabadhi za Mazao Gahalani Na. 10 ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika mwaka huu Serikali kwa kushirikiana na Wamiliki na wenye Viwanda vya Kubangulia Korosho, itafanya uchambuzi wa kina wa matatizo yanayokabili Viwanda hivi ili viweze kutumika kwa ajili ya kununua Korosho kutoka kwa Wakulima na kuzibangua. Lengo letu ni kuhakikisha kuwa Korosho zote zinazozalishwa hapa Nchini zinabanguliwa na kuongezwa thamani ili Mkulima aweze kupata bei nzuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mikakati ya Kuimarisha zao la Pamba. Katika miaka ya hivi karibuni, uzalishaji wa zao la Pamba umekuwa ukidhoofika kutokana na kukumbwa na changamoto nyingi. Kwa mfano, katika msimu wa Kilimo wa 2012/2013 Kanda ya Magharibi ililenga kulima wa hekta 660,000 lakini iliweza kulima hekta 420,000 tu sawa na asilimia 64 ya lengo. Upungufu huu ni sawa na asilimia 26 ikilinganishwa na hekta 568,000 zilizolimwa msimu wa kilimo 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazokabili zao la Pamba kwa sasa ni pamoja na matumizi madogo ya

pembejeo zikiwemo mbegu bora na viuatilifu visivyokidhi mahitaji; na wakati mwingine vimekuwa hafifu kutokana na mfumo wa kusambaza pembejeo hizi kutosimamiwa vizuri. Aidha, katika Mfumo wa Kilimo cha Pamba cha Mkataba ambao unapaswa kumwezesha Mkulima kupata pembejeo kwa njia ya mkopo nao umeingia dosari nyingi kutokana na kuwepo kwa baadhi ya Viongozi na Wafanyabiashara katika maeneo yanayolimwa pamba kuwashawishi wakulima kuukataa mfumo huo. Imebainika kwamba baadhi ya Viongozi hao wana maslahi binafsi katika biashara ya pamba. (*Makofi*)

Aidha, Taasisi zinazotakiwa kusimamia Zao la Pamba zimekuwa hazifanyi kazi zake ipasavyo, Wakulima kukosa imani na Mfuko wa Kuendeleza Zao la Pamba na Vikundi vya Wakulima kutoandikishwa kisheria hivyo kukosa dhamana ya kufidia wanunuzi endapo watashindwa kurejesha fedha za pembejeo na mikopo mingine waliyopewa ndani ya Mkataba.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba tayari, Mikutano ya wadau inayoshirikisha Wakuu wa Mikoa, Wenyeviti wa Halmashauri, Maafisa Kilimo, Waheshimiwa Wabunge, Wafanyabiashara wa Pamba, Wakulima, Viongozi wa Bodi ya Pamba, Wawakilishi wa Wafadhili na Serikali imeshaanza katika Mikoa ya Mara, Simiyu, Geita na Mwanza. Lengo la mikutano hiyo ni kujadili Changamoto zinazokabili Sekta hii ya Pamba na kuweka mikakati ya kukabiliana nayo. Mikutano kama hiyo inatarajiwa kuendelea katika Mikoa yote inayozalisha Zao la Pamba. Hatimaye tarehe 4 - 5 Julai, 2013 utafanyika Mkutano wa wadau wote wa Pamba ambao utajadili changamoto na kutoa ufumbuzi wake.

Mheshimiwa Spika, Mikakati ya kuimarisha Ushirika Nchini. Vyama vya Ushirika vimeendelea kutoa mchango mkubwa katika Maendeleo ya Wananchi katika Sekta mbalimbali za uchumi. Aidha, idadi ya Vyama imeendelea kuongezeka kutoka 5,424 mwezi Machi, 2012 hadi 5,559 mwezi Machi 2013. Idadi ya wanachama nayo imeongezeka kutoka

917,889 hadi 1,153,248 katika kipindi hicho. Hisa, Akiba na Amana za wanachama zimeongezeka pia kutoka shilingi bilioni 236.8 hadi shilingi bilioni 463.5 katika kipindi hicho. Kadhalika mikopo iliyotolewa na *SACCOS* kwa wanachama wake imeongezeka kutoka shilingi bilioni 703.3 hadi shilingi Bilioni 893.7.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, pamekuwepo na changamoto mbalimbali zinazokwamisha kasi ya ukuaji wa Ushirika Nchini. Baadhi ya changamoto hizo zimeongelewa sana ndani ya Bunge na Waheshimiwa Wabunge. Changamoto hizo ni pamoja na kuwepo kwa Viongozi wanaodhoofisha ushirika kwa kukosa ubunifu na kutowajibika katika kutekeleza majukumu yao.

Kwa mfano, katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2010 hadi Juni 2012, jumla ya Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) 1,844 na Vyama vya Ushirika wa Kilimo na Masoko (*AMCOS*) 2,544 vilikaguliwa. Matokeo ya ukaguzi huo yalionesha kukithiri kwa wizi, ubadhirifu na matumizi mabaya ya madaraka kwenye Vyama vya Ushirika. Vitendo hivyo vimefanywa na Viongozi na Watendaji wa Vyama husika. Kutokana na tabia hiyo, baadhi ya vyama vimeingia katika migogoro na madeni makubwa na hivyo kusababisha hasara za mara kwa mara na kuchangia kukatisha tamaa wanachama kuhusu Ushirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika**,** katika kukabiliana na changamoto hizi, hatua kadhaa zimechukuliwa ambapo Viongozi wabadhirifu wameondolewa katika Vyama vya Ushirika vya *CORECU* (Pwani), *CETCU* (Singida), *MLIMANI SACCOS* (Dar es Salaam), *AIRPORT TAX DRIVERS* (Dar es Salaam), *TUCOPROCO*S (Turiani), UWAWAKUDA (Mvomero), MOCEMA (Morogoro), *TINGATINGA ARTS SOCIETY LTD* (Dar es Salaam), *LUICHE SACCOS* (Dar es Salaam), WAZALENDO SACCOS (Moshi) na WETCU (Tabora).

Pamoja na hatua ya kuwaengua katika nafasi za uongozi, hatua za kuwatoza fidia (*sucharges*) pia zimechukuliwa ili kurejesha fedha zilizofujwa. Aidha, utaratibu

wa kuwachukulia hatua zaidi za kijinai unaandaliwa. Ili kuimarisha ukaguzi na usimamizi, Serikali itaunda timu imara ya ukaguzi zikihusisha Wakaguzi kutoka Halmashauri za Wilaya mbalimbali zitakazoweza kufanya kazi kwa pamoja. Hatua hii itasaidia kupunguza uhaba wa Wakaguzi waliopo sasa na kuongeza kasi ya kufanya ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, Vilevile, pamoja na mipango kadhaa ya kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, Serikali itaendelea kuchambua na kutathmini mienendo ya kiuchumi ya Vyama vya Ushirika katika ngazi zote za Vyama vya Ushirika vya Msingi, Vyama Vikuu, Vyama vya kilele na Shirikisho la Vyama vya Ushirika ili kubaini hali halisi ya Vyama hivyo na uwezo wake. Hatua hii itaiwezesha Serikali kutoa ushauri kuhusiana na wimbi la utitiri wa Vyama vidogo vidogo ambavyo kimsingi havina tija.

Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kuwa, Serikali imebaini kuwa matatizo ya Ushirika yanasababishwa na udhaifu katika usimamizi na kwamba tatizo hili pia limetokana na utaratibu wa Maafisa wa Serikali kuwajibika katika Mamlaka mbili tofauti yaani Serikali Kuu na *TAMISEMI*. Hivyo, Serikali imefanya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003 ili kuongeza mbinu za usimamizi. Pia, Serikali itaanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika na kuweka Mamlaka ya Usimamizi wa Vyama vya Ushirika katika ngazi zote, chini ya Mamlaka ya Tume.

Mheshimiwa Spika, Muswada huo tayari umesomwa kwa mara ya Kwanza na unatarajiwa kusomwa kwa mara ya Pili katika Bunge la Mwezi Agosti 2013. Pamoja na changamoto za Ushirika, yapo maeneo ambayo tumeweza kufanya vizuri na ninaamini tukiyapatia msukumo tunaweza kubadili maisha ya wananchi wetu.

Moja ya maeneo hayo ni katika *VICOBA*. Mfumo wa *VICOBA* umeendelea kushamiri na kuenea katika maeneo mbalimbali Nchini. Wananchi wengi hasa wa kipato cha chini wamejiunga na kunufaika na Mfumo huu. Inakadiriwa kuwa

takriba asilimia 35 ya wananchi wanatumia huduma za fedha zisizo rasmi ambazo ni pamoja na *VICOBA*.

Aidha, taarifa zilizopo zinaonesha kuwa tangu mwaka 2000 hadi sasa, inakadiriwa kuwa *VICOBA* vimefikisha Mtaji wa zaidi ya shilingi bilioni 300. Kwa sasa kasi ya kukua kwa mtaji imekuwa kubwa ambapo mtaji unakua kwa shilingi bilioni 100 kwa mwaka, tofauti na vilipoanza. Serikali inatambua hali hiyo na imejipanga vizuri kusaidia uendelezaji wa *VICOBA* nchini kwani mfumo huu ni rahisi na unasaidia sana upatikanaji wa huduma za fedha kwa watu wa kipato cha chini hasa wananchi wanaoishi Vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ili kutoa msukumo katika suala zima la kuendeleza *VICOBA*, tayari Serikali imeshafanya mambo yafuatayo ili kuimarisha *VICOBA* Nchini:-

(I) Serikali imeshaanzisha Dawati maalum la kushughulikia *VICOBA* katika Baraza la Uwezeshaji wa Wananchi kwa kumteua Ofisa maalum wa kusimamia eneo la *VICOBA*;

(II) Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania *(BOT)* imemteua Mtaalam Mwelekezi (*Consultancy*), Kampuni ya *Johannesburg* ya Afika ya Kusini ili kufanya Utafiti (*Study*) na kuishauri Serikali namna bora ya kuendeleza *VICOBA* Nchini; na

(III) Wizara ya Fedha inaanzisha Idara ya Huduma Ndogo ndogo za Fedha (*Microfinance Deptartment*) ili kusimamia maendeleo ya Sekta ya Fedha na Idara hiyo ndio itakuwa Mlezi wa *VICOBA*.

Mheshimiwa Spika, Pamoja na hatua hizo nilizozitaja, Serikali itaendelea kushirikiana na Wadau mbalimbali ili kuhakikisha huduma za fedha zinapatikana hadi Vijijini. Kila Halmashauri, ihakikishe kwamba, mafunzo yanatolewa kwa

Vikundi vya *VICOBA* na vile vinavyoendeshwa vizuri vipewe fursa zaidi ya kujiendeleza.

Kipekee kabisa napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Devota Mkuwa Likokola, Mbunge, kwa jitihada zake kubwa za kuendeleza *VICOBA* Nchini. Serikali itaendelea kuunga mkono juhudi hizo pamoja na Wadau wote wa *VICOBA* hapa Nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ajira kwa Vijana. Katika Mkutano huu, suala la ajira ya Vijana limezungumzwa sana. Tatizo la ajira bado ni changamoto kubwa inayowakabili Vijana Nchini. Kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Vijana (2007) umri wa Kijana ni miaka 15 - 35 kutokana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, idadi ya Vijana Nchini ni 16,195,370 (Bara na Zanzibar).

Idadi hii ni sawa na asilimia 35.1 ya Watanzania wote. Vijana walioajiriwa katika Sekta ya Umma ni 188,087, waliajiriwa katika Sekta Binafsi ni 1,028,634 na waliojiajiri wenyewe ni 1,102,742. Kwa mantiki hii Vijana waliobaki wapatao 13,200,000 wengi wao wanajishughulisha na Kilimo. Hata hivyo, kwa vile Vijana hao waliopo kwenye kilimo hawafanyi kilimo cha kisasa na chenye tija, wengi wao hawafanyi Kilimo cha kibiashara hivyo wako chini ya kiwango cha ajira kamili kinachofahamika Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kwa kutambua umuhimu wa Vijana katika Nchi yetu, ndiyo maana Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umeboreshwa kwa kuongezewa fedha Bilioni Tatu (3) ili kukuza uwezo wa kutoa Mikopo yenye masharti nafuu kwa Vijana na kuwajengea uwezo wa kuanzisha shughuli za uzalishaji mali au kuziimarisha zile wanazoziendesha.

Kiasi hicho cha fedha ni nyongeza kwa Bajeti iliyotengwa kwa mwaka huu wa fedha. Fedha hizi zitatumika kwa Vikundi vya Vijana waliomaliza Vyuo na Vijana wengine watakaokuwa tayari kuanzisha miradi mizuri inayokopesheka.

Fedha hizi zitaendelea kutolewa kupitia SACCOS za Vijana za Wilaya.

Mwongozo mpya wa Matumizi ya Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umesambazwa kwa Halmashauri zote 151 Tanzania Bara na kwamba Miradi ya Vijana sasa itahakikiwa kwenye ngazi ya Halmashauri, Mkoa na Wizara kabla ya mkopo kutolewa. Naomba kutoa wito kwa Vijana hasa wakiwa katika Ushirika kuchangamkia fursa hii ili waweze kujiajiri wenyewe. Nawasihi wafike katika Mamlaka husika kupata maelezo na kuwasilisha michanganuo ya kazi zao ili waweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Spika, Mgogoro wa Ardhi kwenye eneo la Pori Tengefu Loliondo. Tarehe 19 Machi, 2013, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, ilitoa Taarifa kwa Umma kuhusu kusudio la kupunguza ukubwa wa eneo la Pori Tengefu la Loliondo, kutoka Kilomita za Mraba 4,000 hadi 1,500.

Lengo la Serikali lilikuwa ni kulinda mazalia ya Wanyamapori, Mapito na Vyanzo vya Maji kwa ajili ya ustawi wa Hifadhi katika eneo la Kilometa za Mraba 1,500 lililopendekezwa. Vilevile, ni kuhakikisha kuwa usimamizi endelevu wa Hifadhi za Serengeti, Ngorongoro na Pori Tengefu la Loliondo kwa ajili ya Kizazi cha sasa na kijacho.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa hiyo, Wananchi wanaoishi katika Vijiji vilivyomo ndani ya eneo la Pori Tengefu Loliondo na ambao wamekuwa wakiishi katika eneo hilo kwa muda mrefu, hususan katika eneo la Kilomita za Mraba 1,500 ambazo Serikali iliamua ziendelee kubaki na hadhi ya Pori Tengefu, wamepata hofu ya kuhamishwa na hivyo walituma Wawakilishi mbalimbali kufika Dodoma na Arusha kuniona na kuwaona baadhi ya Wabunge wao ili kupata ufafanuzi wa Tamko hilo.

Mheshimiwa Spika, kimsingi, Sheria ya Uhifadhi wa aina mbalimbali za Wanyama (*Fauna Conservation Ordinance)* Sura ya 302 ya Mwaka 1951 ndiyo iliyoanzisha

Mapori ya Akiba na Mapori Tengefu Nchini. Sheria hii ilianzisha Mapori Tengefu 49 Nchini kwa Tangazo la Serikali.

Mwaka 1974, Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori ilianzishwa na kufuta Sheria ya awali ya *Fauna Conservation* Sura ya 302. Chini ya Sheria hizo mbili, masuala ya malisho na makazi hayakukatazwa katika maeneo ya Mapori Tengefu ikiwemo Pori Tengefu la Loliondo. Sheria hiyo ya Hifadhi ya Wanyamapori iliendelea kutumika hadi mwaka 2009 ambapo Sheria mpya ya Uhifadhi wa Wanyamapori (*The Wildlife Conservation Act*) Namba 5 ya Mwaka 2009 ilipoanzishwa na kufuta ile ya awali ya mwaka 1974. Chini ya Sheria hii mpya ya Mwaka 2009, masuala ya malisho na makazi katika maeneo ya Mapori Tengefu yamezuiliwa, mpaka kwa kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori. Kutokana na masharti hayo ya Kisheria, Vijiji ambavyo awali vilianzishwa katika maeneo ya Mapori Tengefu vimejikuta katika hali ya kuvunja Sheria hiyo ya Mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, ndani ya eneo la Loliondo ambalo Serikali inapendekeza liendelee kubaki na hadhi ya Pori Tengefu la Kilomita za Mraba 1,500 kutokana na umuhimu wake kiuhifadhi, kuna Vijiji sita (6) vilivyosajiliwa na Serikali. Kutokana na Tamko lililotolewa, ni dhahiri kuwa Wananchi waliopo katika Vijiji hivyo watatakiwa kuhama katika maeneo hayo. Hata hivyo, changamoto iliyopo ni kwamba, Vijiji vyote hivi vimeanzishwa na Serikali na kupewa hadhi ya kuwa Vijiji, ingawa kwa mujibu wa Sheria ilibidi ardhi hiyo iondolewe kwenye hadhi ya Pori Tengefu kwanza kabla ya kuanzisha Vijiji hivyo. Vijiji hivi vimekuwa ni makazi ya Watu na vina miundombinu ya kudumu ya kutoa huduma kwa Jamii.

Mheshimiwa Spika, wananchi waishio katika Vijiji ndani ya Pori Tengefu la Loliondo wana hofu ya kukosa eneo la malisho ya mifugo na eneo la kuishi baada ya kuishi hapo kwa miaka mingi kabla na tangu kuanzishwa rasmi kwa Vijiji hivyo. Hofu ya kuharibiwa kwa hifadhi hiyo ipo pia kwa upande wa Serikali, na ndio maana Wizara ya Maliasili na Utalii imekuja na Mpango huu wa kuondoa eneo la Kilomita za Mraba 2,500 ili liwe nje ya Hifadhi na kusimamiwa na

wananchi wenyewe kwa kuzingatia Mpango endelevu wa Matumizi Bora ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kulijulisha Bunge lako Tukufu na Wananchi wa Loliondo kuwa, pamoja na kwamba Tamko la Serikali lilitolewa kwa nia njema ya kuendeleza uhifadhi endelevu, kumejitokeza malalamiko mengi dhidi ya Tamko hilo. Serikali imepokea malalamiko hayo kutoka kwa wadau na Makundi mbalimbali ya Wananchi kutoka Loliondo wakiwemo Viongozi wa Wilaya, Halmashauri, Wazee wa Kimila, akina Mama na vijana.

Mheshimiwa Spika, uko ukweli kwamba, suala hili limeleta changamoto kubwa ambayo inahitaji tafakuri kubwa. Kwa kuzingatia changamoto hizo Serikali kwa sasa inafanya mambo yafuatayo:-

(i) Kupitia upya Tamko lililotolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuzingatia Sheria zilizopo za Wanyamapori pamoja na zile za Ardhi;

(ii) Kubaini miundombinu iliyopo katika eneo linalopendekezwa kubaki na hadhi ya Pori Tengefu;

(iii) Kuangalia changamoto zilizojitokeza kwa pande zote mbili (Wananchi na Serikali) kuhusu eneo hilo la Kilomita za Mraba 1,500 kuendelea kubaki na hadhi ya Pori Tengefu; na

(iv) Kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa kuendeleza uhifadhi katika Pori la Loliondo kwa kuwashirikisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikiendelea na hatua hiyo, ninawaomba Wananchi waliomo ndani ya Pori hilo la eneo la Loliondo waendelee kuvuta subira wakati Serikali ikiendelea kutafuta suluhu ya kudumu ya suala hili. Aidha, nimekwisha toa maelekezo ya awali kuhusu namna ya kushughulikia ufafanunuzi wa suala hili kwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha ili kutoa ufafanuzi stahiki kwa Wananchi wanaoishi ndani ya Pori Tengefu Loliondo. Nawaomba Wananchi wa

Loliondo waelewe nia hii njema ya Serikali ya kuwaondolea wasiwasi uliopo.

Mwisho niwaombe Viongozi wa kisiasa wakiwemo, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro, Waheshimiwa Madiwani wa Kata za Loliondo na Sale na Viongozi wa Serikali wa Wilaya ya Ngorongoro na Mkoa wa Arusha watusaidie kusimamia suala hili ili lishughulikiwe kwa manufaa ya Taifa na wananchi wa eneo hilo kwa ujumla.

Aidha, tuendelee kuhifadhi mazingira ya eneo hili ambalo limepata sifa kubwa Duniani kutokana na kuwa na vyanzo vya maji na mapito ya Wanyama Pori wahamao katika Mfumo wa Ekolojia ya Serengeti. Kwa sasa Dunia inatambua eneo hili kama "Urithi wa Dunia" (*World Heritage*) na mojawapo ya Maajabu Saba ya Asili katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, Matokeo ya Uchaguzi. Tume ya Taifa ya Uchaguzi imefanikiwa kusimamia Uchaguzi Mdogo wa Ubunge Jimbo la Chambani, Pemba na Chaguzi Ndogo za Madiwani katika Kata 26 za Halmashauri mbalimbali Nchini. Vyama vilivyoshiriki katika Chaguzi hizo Ndogo ni CCM, *CHADEMA*, *ADC* na *CUF*. Matokeo yanaonesha kwamba, Wagombea wa Chama cha Mapinduzi wamefanikiwa kushinda katika Kata 16 na *CHADEMA* walipata Kata sita (6) katika Kata 22 ambako uchaguzi ulifanyika. Chama cha *ADC* na Chama cha *CUF* vyote havikupata kura. Kwa upande wa Ubunge katika Jimbo la Chambani, wote tumeshuhudia kuapishwa kwa Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein kuwa Mbunge Mpya wa Jimbo hilo kwa tiketi ya Chama cha *CUF*. Nitumie nafasi hii tena kupongeza Vyama vyote vilivyoshiriki na hasa vile vilivyopata ushindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Ngazi ya Vijiji, Mitaa na Vitongoji Mwezi Oktoba, 2014. Tarehe 10 Aprili, 2013 nilitoa taarifa hapa Bungeni kwamba, uchaguzi wa Viongozi katika ngazi za Vijiji, Mitaa na Vitongoji unatarajiwa kufanyika mwezi Oktoba, 2014.

Ofisi yangu inaendelea kuratibu maandalizi ya awali ya Uchaguzi huo ili kuwezesha uchaguzi huo kufanyika

Kidemokrasia zaidi, kwa uhuru na haki. Kwa mujibu wa Kifungu cha 56 (3) cha Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287 na vifungu vya 4 na 70(c) vya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Miji) Sura 288 matokeo ya 2002, jukumu la msingi la Ofisi yangu ni kuandaa Kanuni za uendeshaji Uchaguzi huo ili kuhakikisha demokrasia inakuwepo.

Mheshimiwa Spika, maandalizi yanayoendelea hivi sasa ni pamoja na kupokea michango na maoni ya awali kutoka kwa Wadau mbalimbali hususan Vyama vya Siasa kuhusu namna ya kuboresha Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kanuni hizo zinatarajiwa kutangazwa katika Gazeti la Serikali mwaka 2014. Maoni yanayokusanywa yatachambuliwa na kisha kujadiliwa katika Vikao vya Wadau vitakavyoitishwa.

Aidha, mapendekezo ya Kanuni hizo yatatangazwa kwenye magazeti ili Wananchi waweze kuzisoma na kutoa maoni yao. Wito wangu ni kuwataka Viongozi wa Vyama vya Siasa, Vyama Visivyo vya Kiserikali na Wananchi kwa ujumla kujitokeza kwa wingi katika kutoa maoni ili hatimaye kuwa na Kanuni za Uchaguzi zitakazosaidia kuwa na Uchaguzi Huru na wa haki.

Mheshimiwa Spika, maandalizi mengine yanayofanywa na Ofisi yangu ni kuhakiki Vijiji na kuvisajili. Kabla ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ngazi za Vijiji, Vitongoji na Mitaa wa mwaka 2009 kufanyika, Vijiji na Mitaa mipya ilianzishwa. Maeneo mapya ya Vijiji yalihakikiwa na kutolewa hati za usajili kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa. Kwa sasa, Ofisi yangu imekuwa ikipokea maombi mbalimbali ya kuanzisha Vijiji vipya. Tayari nimetoa maelekezo kwamba mwisho wa kupokea maombi kwa ajili ya maeneo mapya ya Vijiji ni tarehe 31 Desemba, 2013.

Natoa wito kwa Halmashauri zote zinazotaka kuomba Vijiji vipya kuzingatia Sheria, na tarehe ya mwisho ya kupokea maombi hayo. Aidha, nawaomba kuwashirikisha Wananchi

na Wadau mbalimbali kupitia Vikao vya Ushauri vya Wilaya *(DCC)* na Mkoa *(RCC)* ili tuweze kufanikisha maandalizi ya Chaguzi hizo.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Mazingira. Tarehe 1 - 6 Juni, 2013 Nchi yetu iliungana na Nchi nyingine Duniani kuadhimisha wiki ya mazingira Duniani. Maadhimisho hayo yalifanyika Kitaifa katika Wilaya ya Nkasi Mkoani Rukwa. Ujumbe wa Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani mwaka huu ni: "Fikiri, Kula: Hifadhi Mazingira" au kwa Lugha ya Kiingereza *"Think - Eat - Save"*. Ujumbe huu unamaanisha kwamba shughuli zote zinazofanyika za uzalishaji mali na utoaji wa huduma zizingatie kuhifadhi Mazingira badala ya kuwa chanzo cha uharibifu wake.

Mheshimiwa Spika, juhudi za kukabiliana na uharibifu wa mazingira zinakabiliwa na Changamoto mbalimbali. Baadhi ya Changamoto hizo ni: Ukataji miti kwa ajili ya kuni, mkaa, mbao/ujenzi pamoja na uchomaji moto ovyo. Utafiti unaonesha kuwa takriban Hekta 400,000 zinapotea kila mwaka kutokana na ukataji miti.

Changamoto nyingine inayotukabili ni kuwa na Idadi kubwa ya Mifugo ambayo haiwiani na uwezo wa eneo la malisho hasa katika Mikoa ya Shinyanga, Rukwa Mwanza, Morogoro na kadhalika. Hali hiyo inasababisha Wafugaji kuvamia maeneo ya vyanzo vya maji pamoja na maeneo ya hifadhi, na kuleta mmomonyoko wa udongo na hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira. Uchafuzi wa Mazingira ya Makazi kumekuwepo na mazingira ya uchafu katika makazi ya Watu na hasa maeneo ya Miji kutokana na kukosekana kwa namna nzuri ya uondoshaji wa taka ngumu na laini.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikana na Wananchi imeendelea na juhudi za kupambana na uharibifu wa mazingira kwa kuchukua hatua mbalimbali. Hatua hizo ni pamoja na kuhimiza na kusimamia zoezi la upandaji wa miti kila mwaka; kupanua mashamba ya miti ya Serikali kila mwaka, kusimamia Sheria zinazozuia ukataji miti ovyo, kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaochoma

moto ovyo, kuweka Vituo vya Maliwato kwenye Vituo vya Mabasi na kwenye Barabara Kuu, kutenga maeneo ya kukusanyia taka ngumu na Vimiminika Mijini, kuweka mazingira ya Miji kuwa safi na kuhimiza uchimbaji na matumizi ya vyoo na kadhalika. Napenda kuchukua fursa hii kupongeza Mikoa na Halmashauri mbalimbali ambazo wamekuwa wakifanya juhudi kubwa kuhimiza na kusimamia usafi katika maeneo yao. Nimekuwa nikishuhudia ubunifu mkubwa katika suala hili la usafi wa Miji.

Nawaomba Viongozi kwa kushirikiana na Wananchi kusimamia suala la kutunza Mazingira katika maeneo yao. Tuzidi kuimarisha usafi wa mazingira, tusimamie zoezi la upandaji miti kuanzia kwenye nyumba tunazoishi, Barabara, mashamba, Viwanja na kadhalika. Tutunze vyanzo vya maji, tuzuie uchomaji moto ovyo, tuwaelimishe Wafugaji kupunguza idadi ya mifugo ili iendane na maeneo yao ya kulishia na tuchukue hatua zozote zinazoboresha mazingira ili tuwe na maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Uendelezaji na Kuboresha Miji Nchini (*Tanzania Strategic Cities Program (TSCP*). Tarehe 18 Juni, 2013 nilipata fursa ya kuzindua mradi wa kuboresha Miji Nchini katika hafla iliyofanyika Mjini Moshi. Mradi huu unatekelezwa katika Miji 18 ya Tanzania Bara ikiwemo Miji ya Morogoro, Tabora, Moshi, Sumbawanga, Shinyanga, Songea, Singida, Musoma, Iringa, Njombe, Lindi, Bukoba, Kibaha, Babati, Geita, Korogwe, Mpanda na Bariadi. Mradi huo umetanguliwa na mradi mwingine wa Kuboresha Miji Tanzania (*Tanzania Strategic Cities Programme*) ulioanza mwaka 2010. Katika mradi huo kuna Halmashauri saba (7) za awali ambazo zinatekeleza Mradi huo. Halmashauri hizo ni Arusha, Mwanza, Kigoma, Mbeya, Dodoma, Tanga na Mtwara Mikindani pamoja na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma *(CDA).* Kwa hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi huu umebadilisha sura na Mandhari ya Miji hiyo na kuifanya ivutie kwa uwekezaji na kurahisisha utoaji wa huduma nyingine za Kijamii.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii

kuzipongeza Halmashauri hizo saba (7) pamoja na *CDA* kwa kufanya vizuri katika kutekeleza mradi huo na hivyo kuiwezesha Benki ya Dunia kukubali kugharamia awamu nyingine ya Programu ya kuboresha Miji Nchini kwenye Halmashauri za Miji mingine 18, ambayo nimeizindua hivi karibuni pale Moshi. Benki ya Dunia pia imekubali kugharamia Mradi wa Kuboresha Jiji la Dar es Salaam (*Dar es Salaam Metropolitan Development Project-DMDC*) ambao utaanza kutekelezwa wakati wowote kuanzia sasa. Miradi hii mikubwa ya kuboresha Miji niliyoitaja itagharimu Dola za Kimarekani Milioni 455 kutoka Benki ya Dunia.

Fedha hii inategemewa kutumika katika ujenzi wa jumla wa Miradi Midogo Midogo zaidi ya Kumi (10) itakayojumlisha barabara, mifereji, Mifumo ya Uzoaji Taka, Taa za Barabara, maeneo ya Kuegesha Magari, Masoko, Mipango Miji, Ukusanyaji Mapato ya Halmashauri, Uwajibikaji na Makazi holela. Ujenzi wa barabara katika Jiji la Dar es Salaam unajumuisha pia Barabara za Juu (*Fly Overs*) pale Ubungo. Sote tunakubaliana kwamba miradi hii ikikamilika, Miji hiyo itakuwa na Mandhari nzuri kwa Wananchi na kuwa kivutio kikubwa kwa Wawekezaji kutokana na kuboreshwa kwa madhari za kuweka mazingira ya usafi.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuishukuru Benki ya Dunia kwa kukubali kugharamia Miradi hii. Ni dhahiri tunafanya vizuri na ni wajibu wa kila mmoja wetu kusimamia Miradi hii itekelezwe vizuri kwa ubora unaostahili. Ili kuhakikisha kwamba mafanikio yanapatikana katika miradi hii, niwasisitize Wakurugenzi na Wakuu wa Idara wa Halmashauri kusimamia kwa karibu utekelezaji wa miradi hiyo.

Vilevile, Wakurugenzi wa Halmashauri na Wakandarasi wawajibike ipasavyo ili Mpango huu utekelezwe kwa wakati. Aidha, Halmashauri zote Nchini zijenge tabia ya kutenga Bajeti ya kutosha kwa ajili ya kutunza Barabara zinazojengwa ili ziweze kudumu kwa muda mrefu na kuleta manufaa yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio

yanayoonekana wazi katika miradi hii, changamoto nyingine kubwa tuliyonayo kwenye Mpango huu, wa kuboresha Miji ni kuona Sehemu kubwa ya Miji yetu inaendelea kukua kiholela bila kuwepo kwa mipango makini ya kuongoza ukuaji wa Miji hiyo. Napenda kutumia fursa hii kuziagiza Halmashauri zote Nchini zisimamie kikamilifu upangaji Miji ili kuzuia ongezeko la ujenzi holela na uharibifu Miji, hali inayotugharimu fedha nyingi katika kuipanga upya. Aidha, Wananchi waelimishwe kuhusu umuhimu wa kuzingatia Sheria za uendelezaji Miji kwa mujibu wa Sheria za Mipango Miji. Halmashauri zisimamie kikamilifu Sheria zinazokataza ujenzi holela unaoharibu mandhari ya Miji yetu.

Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni Wadau muhimu wa maendeleo ya Jamii na Taifa letu. Mashirika haya yamekuwa na mchango mkubwa hususan kwenye nyanja za afya ikiwemo maradhi yanayotokana na UKIMWI, huduma za Maji, Elimu, Ushiriki wa Jamii, Mazingira, Utawala Bora, Kilimo, Jinsia na Huduma kwa Yatima na Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Aidha, Mashirika haya yamekuwa yakitoa ajira na fursa za kupata uzoefu wa kujitolea kwa Watanzania. Kwa Mfano katika mwaka 2012 zaidi ya watu 60,700 waliajiriwa au kujitolea kwenye Mashirika haya.

Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali imekuwa ikijenga mazingira wezeshi ili yaendelee kukua na kutoa mchango mkubwa zaidi katika maendeleo ya Nchi yetu. Mazingira hayo ni pamoja kuyawezesha kutambulika kisheria kupitia usajili; pili, kuyalinda tatu, kuwezesha ubia baina ya Serikali na Mashirika hayo na nne, kuyawezesha kujitawala kupitia Baraza la Taifa la Mashirika yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa, idadi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ni kubwa na imekuwa ikiongezeka kila mwaka huku mazingira ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali kufanya kazi hapa Nchini yameendelea kuboreka. Kwa mwaka 2012/2013 pekee Jumla ya Mashirika 443 yalisajiliwa na kufanya idadi ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali hapa Nchini kufikia 5,734. Katika mazingira haya ikiwa kila Shirika lisilo la Kiserikali litatekeleza ipasavyo malengo yake iliyojiwekea kwa mujibu

wa Sheria, ni matumaini ya Serikali kuwa hatua kubwa za maendeleo zitapatikana kwa haraka zaidi chini ya Mashirika hayo. *(Makofi)*

Napenda kutumia fursa hii kuyataka Mashirika yote kufanya shughuli zao kwa uwazi zaidi, kushirikiana na Serikali katika kuiletea Jamii maendeleo. Pia Mashirika hayo yanakumbushwa kuwasilisha taarifa zao za mwaka Serikalini kwa mujibu wa Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Na. 2002 kama ilivyorekebishwa mwaka 2005.

Vilevile, nawasihi kujiepusha na kujiingiza katika masuala ya siasa na uchochezi kwa raia. Kutofanya hivyo, kutayawezesha Mashirika haya kuaminika zaidi katika Jamii na kuiwezesha Serikali kuainisha mchango wao katika maendeleo ya Jamii yetu na Taifa kwa ujumla. Kinachotakiwa ni kila Shirika Lisilo la Kiserikali litimize wajibu wake kwa Wananchi ambao ndiyo walengwa bila ya kujinufaisha yenyewe.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa Na. 5 ya 1992 na Kanuni za Maadili ya Vyama vya Siasa inaelekeza Wadau wote wa Demokrasia kutoa maoni yao kuhusiana na marekebisho hayo kwa lengo la kukabiliana na changamoto za Kisiasa na Ki-utendaji zilizopo na zitakazojitokeza katika masuala ya Siasa Nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa amani inadumishwa Nchini. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imewakutanisha Vyama vya Siasa na Jeshi la Polisi Nchini na kuzungumza juu ya dhima ya Jeshi la Polisi na Vyama vya Siasa katika kukua kwa Demokrasia na amani Nchini. Katika mazungumzo hayo Viongozi wa Vyama vya Siasa wamelaani tabia ya baadhi ya Vyama vya Siasa kujihusisha katika kuvunja amani Nchini.

Mheshimiwa Spika, katika siku za hivi karibuni kumekuwa na matukio mengi ya vurugu yanayohusishwa na Vyama vya Siasa. Sheria ya Vyama vya Siasa na Kanuni zake zinakataza Vyama kujihusisha na vurugu, kuigawa Nchi kwa udini, ukabila, rangi au aina yoyote ya ubaguzi ambayo

itasababisha kutoweka kwa amani ya Nchi. Vilevile, Sheria hiyo imeweka bayana kuwa Chama kitakachobainika kufanya hayo, kitafutwa kwa mujibu wa Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwakumbusha Viongozi wenzangu hasa wa kisiasa kwamba, Demokrasia si kufuta Vyama wala kuvuruga Nchi na kuwagawa Watanzania, bali ni kuwa na Sera nzuri zinazowaunganisha Watanzania na kudumisha amani ya Nchi yetu. Kila Mtu pale alipo ana wajibu wa kulinda amani tuliyonayo na kuhakikisha kuwa Sheria za Nchi zinazingatiwa kwa lengo la kulinda haki za Wananchi wote. Nawaomba sana Wanasiasa na Viongozi wezangu tusijaribu kuweka rehani Nchi yetu kwa kuhamasisha kwa njia moja au nyingine Wananchi wetu kuvuruga amani ya Nchi yetu. Tuwafundishe Wananchi wetu kupendana kuvumiliana na kusaidiana.

Mheshimiwa Spika, amani na utulivu nchini. Nimeongelea kuhusu Vyama vya Siasa kutokana na hali halisi ya matukio yanayojitokeza Nchini. Hivi karibuni pamekuwepo na matukio ya vurugu, fujo na uvunjifu wa amani katika maeneo mbalimbali ya Nchi yetu. Katika kipindi cha mwaka mmoja tu uliopita vurugu zimetokea Arusha, Mwanza, Mbeya, Mtwara, Morogoro, Singida na Iringa. Hofu ya migogoro ya kidini imetokea Zanzibar, Dar es Salaam, Arusha, Mwanza na Geita. Baadhi ya matukio haya yamesababisha Vifo na majeruhi ikiwemo, kujeruhiwa Askari na Wananchi, uharibifu wa miundombinu, uharibifu wa mazingira na mali za Serikali na Watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, matukio mfululizo ya fujo, vurugu pamoja na tukio la kulipua mabomu Kanisani na hivi karibuni katika Mkutano wa hadhara huko katika Kata ya Soweto kule Arusha na katika Mkutano wa Kampeni ya Chama cha Chadema katika Uwanja wa Soweto Arusha yamesababisha hofu kubwa kwa Wananchi na hisia ya uwepo wa tishio la kuendelea kwa vitendo vinavyoashiria ugaidi katika Nchi yetu.

Matukio ya aina hii yakiachwa yaendelee, uchumi wa Nchi yetu utadorora kutokana na ushiriki hafifu kwenye shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ziko dalili ya kuwepo kwa vikundi vya Watu wachache wasioitakia mema Nchi yetu. Vikundi hivi vinataka kupandikiza chuki za kisiasa na kidini miongoni mwa Watanzania na kuleta mapigano na mauaji miongoni mwao. Sina shaka kuwa fujo, vurugu, vitendo vya uvunjifu wa amani ikiwemo mashambulio ya Mabomu Arusha na vurugu za Mtwara ni sehemu ya mikakati hiyo mibovu. Nataka niwahakikishie Watanzania kuwa Serikali haitavumilia hata kidogo kuendelea kupandwa mbegu za chuki na za kidini na kisiasa miongoni mwa Watanzania. Serikali itachukua hatua kali bila huruma kuzimaliza njama hizi mbaya dhidi ya Taifa letu.

Vilevile, hatua kali zitachukuliwa kwa Mtu yeyote atakayebainika kuhusika bila kujali hadhi na nafasi yake katika Jamii.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii tena kuwasihi Viongozi wa Serikali, Kisiasa, Kidini na Wananchi wote kwa ujumla, kila mmoja kwa nafasi yake kuwajibika ili kuhakikisha kuwa Nchi yetu inaendelea kuwa Kisiwa cha Amani na Utulivu. Watanzania wote tushirikiane na Vyombo vya Dola katika kubaini wahalifu hao.

Tuendelee na mshikamano wa kukataa vitendo vya uvunjifu wa Amani katika Nchi yetu. Kila mwenye taarifa za kuwezesha kukamatwa kwa Watu wanaohatarisha amani ya Nchi yetu atoe taarifa kwenye vyombo vya dola au kwa Jeshi letu la Polisi na taarifa hizo zitafanyiwa kazi kwa umakini mkubwa na kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, changamoto kubwa iliyoko mbele yetu baada ya kuwepo hapa Bungeni kwa takriban Siku 78 ni kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali tuliyoipitisha. Sisi kama Wabunge tuondoke hapa kwa lengo

moja la kushirikiana na Wananchi kusukuma maendeleo na Bajeti tuliyoipitisha ikiwa ndiyo kichocheo kikuu. Nchi yetu bado ni nzuri na ina amani.

Wananchi wetu bado ni Watu wazuri, wastaarabu, wavumilivu na wapenda amani. Wananchi wanaelewa na ni watiifu. Twendeni tukasisitize umuhimu wa kuishi kwa amani, upendo na mshikamano. Tukiwasimamia vizuri na kuwaongoza katika matumizi ya rasilimali zilizopo, Nchi yetu itasonga mbele kimaendeleo na maisha bora kwa Wananchi wetu yatapatikana.

Mheshimiwa Spika, napenda nimalizie kwa kuwashukuru wote waliosaidia kufanikisha Mkutano huu. Nikushukuru kwa namna ya pekee wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa kutuongoza vizuri kulingana na Kanuni za Bunge. Aidha, niwashukuru Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mbunge wa Ilala na Mheshimiwa Muhammed Seif Khatib, Mbunge wa Uzini kwa kuongoza vizuri baadhi ya Vikao vya Bunge wakati wa Mkutano huu. Ninawashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu ya dhati na yenye mantiki kwa ajili ya Maendeleo ya Nchi yetu.

Niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, Watumishi na Wataalam wote wa Serikali waliosaidia kujibu Maswali na Hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge zilizojitokeza hapa wakati wa Mkutano huu. Vile vile, nawashukuru Waandishi wa Vyombo vya Habari kwa kuwapatia Wananchi habari kuhusu Majadiliano yaliyokuwa yanaendelea hapa Bungeni. Wote kwa ujumla wenu nawashukuru sana. *(Makofi)*

Kipekee napenda kuwashukuru Madereva wote ambao wamekuwa makini katika kazi ya kuwaendesha Viongozi wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge na Wataalam kutoka sehemu mbalimbali Nchini na kuwawezesha kufika hapa Dodoma kuhudhuria Mkutano huu wa Kumi na Moja. Vilevile, nawashukuru Wananchi wa Mkoa

wa Dodoma, Wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Dkt. Rehema Nchimbi kwa ukarimu wao kwa muda wote tuliokaa hapa Dodoma.

Navishukuru pia Vyombo vya Ulinzi na Usalama ambavyo vimehakikisha muda wote tumekaa kwa Amani na kwa Utulivu mkubwa. Mwisho namshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa huduma nzuri zilizowezesha kukamilisha shughuli zilizopangwa katika Mkutano huu bila matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwaombea safari njema mnaporudi katika maeneo yenu ya kazi, lakini pia niwaombee kheri na Baraka tele Waislam wote ambao katika siku chache zijazo watashiriki katika Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Kila atakayeamua kufanya Ibada hiyo aifanye kikamilifu na kama Kitabu cha *Quran* Tukufu kinavyoelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe hadi tarehe 27 Agosti, 2013 siku ya Jumanne, Saa 3.00 Asubuhi litakapokutana katika Mkutano wa 12 kwenye Ukumbi huu hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, naafiki

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nadhani mtaungana na mimi kwamba maneno mazito aliyoyatoa Waziri Mkuu tutayatengeneza kwenye kitabu kusudi muweze kuyachukua. Hili limekuwa ni ombi la baadhi yenu kwamba ni vizuri tukapata ile hotuba yake kwa sababu ni kama *summary* ya yote tuliyokuwa tunafanya hapa. Maana kuna masuala ya *VICOBA, Micro-Finance* na kadhalika. Kwa hiyo, ni muhimu sana kufanya hivyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini mimi pia nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa kazi nzuri mliyofanya katika

siku zote 78 tulizokuwepo hapa. Nawashukuru kwa sababu mmefanya kazi nzito na nzuri. Mahali pengine tumekwaruzana kwaruzana hivi, na hasa ukikaa hapa mezani. Kukwaruza watu sio kitu cha ajabu. Ukikaa hapa lazima utakwaruza maana unaweza kuona unapendelea, unaonea unafanyaje, lakini ndiyo maana ya kiti kama hiki.

Kwa hiyo, kwa niaba ya wenzangu, *presiding officers* wote Naibu Spika, Wenyeviti na mimi mwenyewe, pale tulipowakwaruza sisi hatukufanya kwa makusudi. Ilikuwa ni kwa bahati mbaya na pengine akili zote hizi uzibebe uziweke hapa kwenye kiti siyo rahisi. Kwa hiyo, mtusamehe na nyie mmetukwazakwaza lakini na sisi tunawasamehe. *(Makofi/ Kicheko)*

Nasema narudia siku zote Mabunge tuliyozoea sisi ni mahali pa kushindana kwa hoja wote mnatoka mnafurahi pamoja. Sio mtoke mmoja katoka kanung'unika, roho yake ina kivimbi, jamani unajisumbua bure. Kwa sababu hapa ndani hata ukifanya hivyo utaumia wewe hakuna mwingine atakayeumia sisi tumemaliza na tumeacha kila kitu hapahapa, tumesahau kila kitu hapahapa.

Kwa hiyo, nawaombeni kabisa Waheshimiwa Wabunge hizo ndizo mila za Mabunge ya Kidemokrasia. Huondoki na kitu chochote kichwani mwako kinachokupa malalamiko na chuki ya roho. Mnajibishana hapa kwa hoja wengine wanashinda, wengine wanashindwa lakini mradi ni hoja na wote mnapongezana tunatoka vizuri.

Hiyo ndiyo inatakiwa sisi tuwaonyeshe wananchi wetu. Kwamba hapa ndani kwenye vyama vingi si mahali pa kupigana wala kuchukizana wala kutengeneza uadui. Tumepitisha hapa kuunda vyama vingi sisi wenyewe haohao. Sasa kama kweli vyama vingi ni chuki hivi kwanini tulipitisha Sheria ya namna ile.

Kwa hiyo tunataka na wananchi wafahamu tuna vyama vingi na tuna wajibu wa kuviheshimu vyama vyetu lakini isiwe sababu ya kuwatenga ama kuwagawa watu. Kwa

sababu kiti kama cha Spika kila siku na waandishi wa habari lazima niseme. Wataandika tu Spika anapendelea, jamani kwa jina la Mungu kazi hiyo haipo.
Maana yake wakati mwingine wanamshawishi Spika afanye vibaya. Sasa kama mimi ninavyofanya hivi napendelea hivi nikipendelea inakuaje, si itakuwa hatari kweli? *(Makofi/ Kicheko)*

Kwa hiyo, mimi napenda sana muamini kabisa sisi tunafuata Kanuni za Bunge na pale tunapopotoka tunasahihishwa. Tafadhali waandishi wa habari acheni tabia ya kudanganya watu kwamba humu ndani tunaendesha Bunge kwa kupendelea siyo kweli. Tungekuwa tunapendelea hapa watu wengine wasingepewa hata nafasi ya kuzungumza. Lakini unajua Bunge ni wote kila mtu ana haki ya kusema kwa mujibu ya Kanuni zetu.

Lakini mnaendesha maneno, nafahamu kuna waandishi wa habari wenye matatizo yao, ondoeni matatizo yenu na mjue pia na Mungu anawaangalia jamani. Taifa lolote lisilomwogopa Mungu ni taifa lililokwisha.

Waheshimiwa Wabunge, mimi naombeni tuamini hilo tufanye kazi kwa nia njema na tuaminiane wote kwa sababu ya mustakabali wa nchi yetu. Amani haiwezi kuja isipokuwa tunapoaminiana. Tubishane kwa hoja, tumalize kwa hoja tukitoka hapa marafikiri na sisi ni Watanzania tukajenge nchi yetu vizuri.

Kwa hiyo, mimi nawashukuruni sana ndugu zangu kwa yote tuliyoweza kufanya pamoja, tumeshirikiana kufanya hapa mabadiliko makubwa pamoja na tumefanya kazi pamoja kwa utulivu na kwa upendo na kwa umakini sana na tumefikia hapa. Hakuna mtu wa kupata sifa mwenyewe peke yake, ni sisi wote kwa sababu mmoja ukifanya kidole kimoja hakivunji chawa.

Kwa hiyo, nimshukuru Katibu wangu na ofisi yake wamefanya kazi kubwa sana. Nawashukuru hawa vijana

wanaotembeatembea hapa, tungewafungia millage sijui wametembea kilomita ngapi humu ndani. Tunawashukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

Nawashukuru sana waandishi wa habari na hasa *TBC. TBC* imefanya kazi kubwa ya kuhabarisha watu ingawa mara nyingine ilikuwa inapata matatizo kwa sababu ya hali yake ya uchakavu nafikiri Serikali pamoja na kutoa kiasi kidogo lakini waendelee kuwaangalia iweze kuimalika vizuri kwa sababu ndiyo mategemeo ya wananchi. Baada ya kusema hayo naomba nimtambue Mheshimiwa Mama Tunu Pinda, Mke wa Waziri Mkuu. Amekuwa na sisi katika maeneo haya. Ahsante sana kwa kutuunga mkono. (*Makofi*)

Lakini nitangaze hapa, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* Mheshimiwa Idd Azzan anaomba niwatangazie Wabunge kwa majina maana kuna kucheza kule Dar es Salaam mpira wa miguu ambao ni Wabunge na wafanyakazi watakaoshiriki katika mchezo wa kirafiki kati ya timu ya Wabunge wa Yanga na Simba utakaofanyika katika Uwanja wa Taifa siku ya tarehe 7 Julai, 2013 na mchezo wa ngumi nao upo. Wachezaji wa Yanga na hapa wananikwaza mara waniambie mimi Yanga mara Simba sasa sijui mimi niko timu gani.

Kwa hiyo, wachezaji wa Yanga ni Mheshimiwa Said Zubeir, Mheshimiwa Abdallah Haji, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Said Mntanda, Mheshimiwa Dunstan Kitatundula, Mheshimiwa Sulemani Jafo, Mheshimiwa Faki Haji Makame, Mheshimiwa Ahmed Ngwali, Mheshimiwa Mwigulu Mchemba, Mheshimiwa Mahamoud Mgimwa, Mheshimiwa Athumani Mfutakamba, Ndugu Mark Tanda, Ndugu Michael Kadebe, Ndugu Christopher Kannonyele na Ndugu Paul Chima. Kapteni wao ni Mheshimiwa Ahmed Ngwali. (*Makofi*)

Sasa nije Simba na majina yao ni Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Amos Makalla, Mheshimiwa Adam Malima, Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Khalifa Suleman Khalifa, Mheshimiwa Joshua Nassari, Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangala, Mheshimiwa Kassim

Majaliwa, Mheshimiwa Eng. Ramo Makani, Ndugu Waziri Kizingiti, Ndugu Abeid Kikula, Ndugu Yona Kirumbi, Ndugu Onesmo Laulau. (*Makofi*)

Kumbe wote hawa wote Simba mbona siku nyingine wanagombana. Halafu kuna mchezo wa ngumi sasa. Watakaocheza huo mchezo ni Mheshimiwa Halima Mdee na Mheshimiwa Ester Bulaya hawa watashiriki mchezo wa ngumi siku hiyo wakipambana na Jackline Wolper na Anti Ezekiel. Mimi siwajui. (*Kicheko*)

Kwa hiyo hayo ndiyo mambo ya tarehe saba sijui saa ngapi. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge mtakaokuwepo karibu mahali hapo basi msogee, ni mchezo ambao unawakusanya vijana pamoja na wakaondokana na tofauti zisikuwa na akili wakawa kama Watanzania vijana wanaoburudisha. Kwa hiyo mimi nawashukuru sana kwa hilo na naomba tusimame kwa ajili ya wimbo wa taifa.

MBUNGE FULANI: Hujahoji kuhusu Kuahirisha Bunge.

SPIKA: Nitawahoji baadaye.

(Hapa Wabunge waliimba Wimbo wa Taifa)

SPIKA: Sasa nitawahoji kuhusu Hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya Kuahirisha Bunge, mpaka tarehe 27 Agosti, 2013.

WABUNGE FULANI: Siyoooo!

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge wasiokubali Kuahirisha Bunge waendelee kubaki humu humu ndani. Lakini mimi Naahirisha Bunge mpaka tarehe 27 Agosti, 2013 hapa hapa Dodoma.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa

(Saa 6.47 mchana Bunge liliahirishwa Mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 27 Agosti, 2013 Saa Tatu Asubuhi, Mjini Dodoma